

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Nne – Tarehe 5 Februari, 2021

(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

Na. 42

Ujenzi wa Vituo vya Afya kwa Nguvu za Wananchi

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE (K.n.y. MHE. ALMAS A. MAIGE) aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Tabora Kaskazini wamejitolea kujenga Vituo vya Afya katika Kata za Ilongulu, Mabama, Shitagena na Usagari katika Kijiji cha Migungumalo:-

Je, Serikali ipo tayari kuanza kuchangia miradi hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mchango mkubwa wa wananchi katika ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Hivyo, Serikali ina dhamira ya dhiti ya kuchangia nguvu hizo za wananchi katika kukamilishaji vituo hivyo ili vianze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa ukarabati na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini ikiwemo kukamilisha maboma ya majengo ya kutolea huduma za afya yaliyojengwa na wananchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambapo ujenzi wake ulisimama kwa kukosa fedha. Hadi kufikia Septemba 2020 jumla ya shilingi bilioni 315.31 zimetumika kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 27.75 kwa ajili ya kukamilisha maboma 555 ya zahanati nchini yakiwemo maboma manne (04) katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui Mkoani Tabora ili kuunga mkono jitihada za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na kuthamini michango na nguvu za wananchi na itaendelea kuchangia nguvu za wananchi katika kujenga na kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini kadri ya upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama liliyo swali la msingi, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwenye Wilaya ya Kyerwa tuna kata 24 lakini tuna vituo vya afya vitatu; Serikali ina mpango gani wa kuongeza vituo vya afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kituo cha Afya Nkwenda ni kituo ambacho tumeanzisha jengo la mama na mtoto ambalo bado halijakamilishwa. Serikali ina mpango gani wa kukamilisha Kituo cha Afya Nkwenda kwenye jengo la mama na mtoto?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Halmashauri ya Kyerwa kuwa na kata 24 na vituo vya afya vitatu tu na Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba halmashauri hiyo inapata vituo vya afya kadri ya maelekezo na sera. Kama ambavyo nimetangulia kusema kwenye jibu la msingi, Serikali imedhamiria kuhakikisha inasogeza huduma za afya karibu na wananchi kwa kuunga mkono ujenzi wa vituo vya afya katika kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa utekelezaji wa miradi hii ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata ni endelevu na ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi bilioni 27.75 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo 555. Pia katika mwaka wa fedha ujao tutatenga bajeti kwa

ajili ya kuendelea kujenga vituo hivyo. Halmashauri ya Kyerwa na kata zake ni sehemu ya halmashauri na kata ambazo zitanufaika katika mradi huu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kituo cha afya kuwa na jengo la wazazi na Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha jengo hilo linakamilika na kutoa huduma. Hilo ni jambo la muhimu sana katika kusogeza huduma kwa wananchi. Kwa sababu Serikali inatambua na ina dhamira ya dhati ya kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga, kipaumbele ni pamoja na kutenga fedha kadri zinavyopatikana kwa ajili ya kukamilisha majengo kama haya. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba pia jengo hilo litakuwa sehemu ya mpango huu ili liweze kukamilishwa na kutoa huduma zinazokusudiwa kwa wananchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Athuman Maige, swali la nyongeza.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kijiji cha Migungumalo, Kata ya Usagari, Marehemu Mheshimiwa Benjamin William Mkapu alizindua zahanati ndogo na aliahidi kwamba pale patajengwa kituo cha afya ili iwe hospitali kubwa ambayo atakuja kuifungua tena. Nilipoingia madarakani tumeanzisha kujenga kituo kile na kwa uchungu sana nilikuwa nimepanga kwenda kumwambia Mheshimiwa Benjamin Mkapu kwamba sasa ajiandae kuja kufungua kituo kile na bahati mbaya Mheshimiwa Mkapu amefariki, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Nimeshamwambia Mheshimiwa Rais juu ya suala hilo...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maige, swali lako la nyongeza?

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, kwa vile kituo kile tunakijenga kwa nguvu za wananchi,

je, Serikali ina mpango gani wa kukimalizia kituo hicho ili heshima ya Marehemu Benjamin Mkapa ihimidiwe?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Tabora Kaskazini kwa kuchangia maendeleo na kuanza ujenzi wa kituo hicho cha afya ambacho lengo ni kupandisha hadhi ya zahanati kuwa kituo cha afya. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Maige kwamba katika bajeti ya Serikali ya kwenda kukamilisha majengo ya zahanati na vituo vya afya ambayo imetengwa katika mwaka huu wa fedha katika halmashauri yake na katika jimbo lake, jumla ya vituo vinne vimetengwa na jumla ya shilingi milioni 200 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo eneo hilo la kituo hicho cha afya ambacho ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, basi tutakwenda pia kuona namna gani tunashirikiana katika bajeti hii, lakini pia katika bajeti zinazofuata, ili tuweze kukikamilisha kiweze kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ngassa, swali la nyongeza.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la vituo vya afya vilivyopo kwenye Jimbo la Tabora Kaskazini ni sawa na lililopo kwenye Jimbo la Igunga, Kata za Isakamaliwa, Kining'inila na Mtungulu. Ni kata ambazo hazina vituo vya afya vya kata

na sisi kama wananchi tumeanza kutoa nguvu yetu kusaidia wananchi kujenga vituo vya kata. Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za wananchi kukamilisha vituo vya hizo kata husika ili tuweze kuwapatia wananchi huduma ya afya? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuunga mkono nguvu za wananchi katika ujenzi wa vituo vya afya katika kata. Katika bajeti ambayo imetengwa lengo ni kuhakikisha kwamba kadri ya upatikanaji wa fedha nguvu za wananchi zitaendelea kuungwa mkono kwa Serikali kupeleka fedha ili kukamilisha vituo vya afya na zahanati zinazojengwa katika maeneo hayo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Igunga kwamba Igunga ni sehemu ya halmashauri na kata zake ni sehemu ya kata nchini kote ambazo zitanufaika na mpango huu wa umaliziaji na ujenzi wa vituo vya afya ili viweze kutoa huduma kwa wananchi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Nape Nnauye kwa niaba yake.

Na. 43

Mlimba Kupewa Hadhi ya kuwa Wilaya

MHE. NAPE M. NNAUYE (K.n.y. MHE. GODWIN E. KUNAMBI) aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ni Halmashauri mpya iliyotoka Wilaya ya Kilombero:-

(a) Je, ni lini Serikali itaipa Mlimba hadhi ya kuwa Wilaya hasa ikizingatiwa umbali mrefu wa takriban Km 200 ambao Wananchi wanatembea kufuata huduma Makao Makuu ya Wilaya?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa majengo ya Halmashauri na kuboresha miundombinu ya barabara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa miongozo na taratibu, uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala unahusisha uhitaji wa wananchi, Viongozi wa Wilaya na Mkoa ambao huwasilisha maombi ya mapendekezo yao kwenye vikao vya Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) na kisha kuwasilishwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa hatua zaidi. Ofisi ya Rais-TAMISEMI, haijapokea maombi rasmi ya Mkoa wa Morogoro kuomba Mlimba kuwa Wilaya. Serikali inashauri utaratibu huu uliowekwa ufuatwe.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba. Mwezi Januari mwaka huu, Serikali imekwisha peleka kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi wa jengo hilo la utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu ya barabara, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imefanya matengenezo ya barabara zenye

urefu wa kilomita 54, imejenga kalvati 22 na madaraja manne (4) kwa gharama ya shilingi milioni 545.87. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali kupitia *TARURA* imetenga kiasi cha shilingi milioni 517.56 kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, tunajua kwamba Serikali ilisitisha uongezaji wa maeneo ya utawala lakini Serikali ilitoa ahadi hapa Bungeni kwamba yale maeneo ambayo hayatakuwa na gharama za uanzishwaji wake na hasa maeneo ya kata, kwa sababu kata zetu hizi ni kubwa mno katika baadahi ya maeneo. Je, Serikali itaanza kutekeleza ahadi hii lini ili kusogeza huduma karibu na wananchi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara hizi ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezitungumzia hapa zimekuwa zikiharibika mara kwa mara na hasa wakati huu wa kipindi cha mvua. Uwezo wa *TARURA* kuendelea kuzikarabati hizi barabara unaonekana unapungua siku hadi siku kwa sababu ya mgao mdogo ambao wanaupata kutoka kwenye fedha za Bodi ya Barabara. Je, Serikali haioni umefika wakati sasa wa kuanzisha chanzo maalum cha fedha kupelekwa kwenye *TARURA* badala ya kutegemea hisani kutoka kwenye Mfuko wa Barabara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya

nyongeza ya Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali ina mpango na dhamira ya dhati ya kusogeza huduma za jamii karibu na wananchi kwa kuanzisha maeneo ya utawala ambayo hayatakuwa na gharama kubwa. Kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, naomba nimhakikishie kwamba dhamira hiyo ya Serikali ipo na utaratibu wa kuomba maeneo hayo unafahamika na nishauri kwamba pale ambapo tunaona kuna kila sababu ya kuanzisha maeneo hayo yanayofuata maelekezo ya Serikali ya kuzingatia kutokuongeza gharama, basi maombi yawasilishwe kwa mujibu wa taratibu Ofisi ya Rais TAMISEMI ili yaweze kufanyiwa kazi kwa kadri ya taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la nyongeza la pili la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye ni kuhusiana na barabara zinazohudumiwa na *TARURA*. Ni kweli Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini ina jukumu kubwa la kuhakikisha miundombinu ya barabara inapitika mwaka mzima. Wakala huyu ana mtandao wa barabara zipatazo kilometa 108,496 ambazo hufanyiwa matengenezo mara kwa mara na pale inapobidi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba bado bajeti ya *TARURA* haitoshelezi lakini Serikali imekuwa ikiongeza fedha mwaka hadi mwaka ili angalau kuendelea kuboresha utekelezaji wa wakala huyu. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, bajeti ya *TARURA* ilikuwa shilingi bilioni 241, lakini kwa mwaka 2020/2021 bajeti ya *TARURA* ni shilingi bilioni 275 ikiwa ni ongezeko la takribani shilingi bilioni 34. Ni kweli Serikali inaona sababu ya kutafuta vyanzo vingine vya kuongezea uwezo *TARURA* ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa zaidi na jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba na mimi niulize swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Sengerema ina halmashauri mbili, Halmashauri ya Sengerema na Halmashauri ya Buchosa. Mimi ni Mbunge wa Buchosa, wakati wa kampeni nilimuomba Mheshimiwa Rais Halmashauri ya Buchosa nayo iwe Wilaya. Kwa hiyo, naomba kujua ni lini sasa Buchosa nao watakumbukwa kuwa Wilaya? Halmashauri hii ina mapato makubwa, ni halmashauri inayojitosheshelea na inafaa kabisa kuwa wilaya ili huduma ziweze kuwasogelea wananchi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Erick Shigongo, Mbunge wa Buchosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tunahitaji kusogeza huduma za jamii karibu zaidi na wananchi na kuanzisha maeneo mapya ya utalawa. Ni sehemu ya kusogeza huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Buchosa ambayo Mheshimiwa Shigongo anaielezea, naomba nimshauri kwamba utaratibu wa kuomba maeneo mapya ya utawala unafahamika na Ofisi ya Rais, TAMISEMI bado haijapata taarifa rasmi kutoka Mkoa wa Mwanza, ukihitaji kuomba Halmashauri ya Buchosa kuwa Wilaya. Kwa hiyo, naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge, wafuate utaratibu huo na Serikali itaona namna gani ya kulifanyia kazi suala hili. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,

Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 44

Wodi ya Wazazi – Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa wodi ya wazazi utanza katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga ni miongoni mwa Hospitali za Rufaa za Mkoa zinazoboreshwa. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Mshauri Elekezi wa Ujenzi wa Wodi ya Wazazi ameshapatikana, ambaye ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, hatua inayoendelea hivi sasa, ni mchakato wa zabuni ya kupata mkandarasi atakayefanya kazi ya ujenzi, ambapo ujenzi huo unategemewa kuanza mwezi Machi, 2021. Mradi huu utatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu yenye matumaini kutoka kwa

Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kabla sijauliza, napenda kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Shinyanga hasa wanawake walioweza kunichagua na chama changu kunitewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza la nyongeza; kwa kuwa ili hospitali iweze kukamilika na kuanza kufanya kazi ni lazima miundombinu yote iwepo kama maabara, *X-Ray* na *mortuary*. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba majengo mengine na miundombinu mingine inakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa tumeanza kuona jitihada nzuri za Wizara ya Afya katika kudhibiti wizi wa madawa na ubadhirifu wa madawa: Je, nini mkakati endelevu wa Serikali kuhakikisha kwamba wizi wa dawa unadhhibitiwa na dawa zinapatikana muda wote? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Mheshimiwa Mnzava ameuliza kuhusu majengo mengine. Kwa bajeti ya mwaka huu 2021 Serikali imetenga shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya majengo mengine ambayo ameyataja.

Vilevile imetenga shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya magonjwa ya mlipuko. Kwa maana kwa bajeti mwaka huu tunaokwenda kuanza, kuna shilingi bilioni 6.4 ambazo zinaenda kuelekezwa kwenye hospitali husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ameuliza ni kwa namna gani tunaenda kudhibiti wizi wa madawa kwenye hospitali zetu. Kwanza, niseme tu kwamba tumepita na tumegundua kwamba watumishi wengi wa Wizara ya Afya

wanafanya kazi nzuri sana lakini kuna wachache ambao wanafanya haya mambo ya ubadhirifu. Vile vile tumegundua kwamba wabadhirifu wamekuwa wakienda Mahakamani aidha, wanaishinda Serikali au kesi zinachukua muda mrefu. Kwa hiyo, tunaenda kimkakati sana kuhakikisha kwamba yeyote atakayepatikana hachomoki, ni lazima awajibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya miezi miwili, mtaanza kuona mkakati wa Wizara wa kuhakikisha moja kwa moja hayo mambo yamefutika, kwa sababu watu wako chini kuhakikisha kwamba tukianza kufanya hiyo kazi hakuna atakayechomoka na tunamaliza hilo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 45

Hospitali Zinazoendelea Kuwatoza Wajawazito

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la hospitali ambazo zinaendelea kutoza fedha akinamama wanaojifungua kwa njia ya kawaida?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Sera ya Afya ya mwaka 2007, Ukurasa wa 19, kifungu 5.3.4 ambacho kinahusu afya ya mama na mtoto na Tamko la Sera Kipengele (c) Sehemu ya (i), inaelekeza kuhusu huduma bila malipo kwa Huduma za Afya ya Uzazi na Watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020 Serikali ilitoa huduma kwa wenye uhitaji bila malipo likiwemo kundi hili, zenye thamani ya shilingi takriban bilioni 880. Hivyo, Wizara inasisitiza watoa huduma wote kuzingatia utekelezaji wa tamko hili la kisera.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa tayari Wizara imewaelekeza na kuwataka Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri ambao ndio wasimamizi wakuu wa utekelezaji wa Sera na Miongozo ya Afya katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri kutimiza kikamilifu majukumu yao kwa kushughulikia haraka kero na malalamiko ya wananchi ikiwemo vituo vya kutolea huduma za afya kuacha kuwatoza fedha wajawazito na watoto wanapofika kituoni kupata huduma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Afya kwa kazi nzuri chini ya Mheshimiwa Dkt. Gwajima, lakini hivi karibuni Mheshimiwa Dkt. Mollel alifanya kazi nzuri pale Mount Meru Hospitali kwa ajili ya kurudisha zile fedha ambazo alitozwa yule mama ambaye alikuwa ametoka kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Hospitali ya Kitete Tabora bado inatoza fedha kwa akinamama ambao wamejifungua *normal delivery* na ushahidi upo. Je, msimamo wa Serikali ukoje ukizingatia katazo ambalo alilitoa

Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akiwa Songwe na hiyo Sera ya Afya ambayo ametoka kuitamka Mheshimiwa Naibu Waziri? Nini msimamo wa Serikali kuhusu kuendelea kutozwa akina mama hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; akinamama ambao wanashindwa kutoa hizo fedha ambazo zinaanzia Sh.30,000/= mpaka Sh.50,000/= katika *normal delivery*, huwa wanazuliwa pale Hospitali ya Kitete Tabora Manispaa. Je, Serikali ina msimamo gani kuhusu wale akinamama ambao bado wanazuliwa na watoto wao wachanga, hakuna kutoka mpaka watoe fedha hizo ambazo ni za kujifungulia? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake huo mzuri kwa ukaribu kwenye eneo hili la Huduma ya Mama na Mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Serikali bado ni ule ule wa kiseru na miongozo na maelekezo ya Serikali, kama ambavyo nilishasema kwamba Waganga Wakuu wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Wilaya wahakikishe wanasimamia utekelezaji wa sera hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini msimamo wa Serikali? Ukienda kwenye hospitali ambayo Mheshimiwa Mbunge anasema, mapato yao kwa mwezi huu wa Januari, 2021 ni shilingi milioni 73; mapato kutokana na Bima ni shilingi milioni 133, lakini Serikali imepeleka *OC* ya shilingi milioni 54 kwa mwezi wa Januari, 2021. Maana yake mapato yao kwa mwezi ni shilingi milioni 260. Ukitoa na matumizi ya akinamama na watoto, hizi za kutoa bure, ni milioni 13 *point*, ndiyo

matumizi yao kwa mwezi Januari, 2021. Maana yake ukitoa matumizi mengineyo ni shilingi milioni 134, ukija ukijumlisha, wanabakia kuingia mwezi huu wa Februari, 2021 na shilingi milioni 120. Kwa maana nyingine hakukuwa na sababu yoyote ya kum-charge mama na watoto pesa yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikipeleka OC ya shilingi milioni 54 kwenye hospitali hiyo kila mwezi, maana yake imeshawalipia hawa akinamama. Ukiondoa shilingi milioni 13 ina maana imebaki fedha nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaondoka pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwenda Kitete, tukae site pamoja tupige hesabu na tuone. Tutakubaliana pamoja, tutakuja na way forward. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuuliza swali langu Na. 46 naomba nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Afya kwa Mpango Maalum walioandaa kuwakamata wale wate wanaohusika na madawa nchini.

Naishauri tu Serikali kwamba wale wezi wote watakaogundulika kuiba madawa, basi waweze kuchukuliwa hatua za kisheria na ikiwezekana wafungwe kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba swali langu Na. 46 lipatiwe majibu ya Serikali.

Na. 46

Mapambano Dhidi ya Malaria

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH aliuliza:-

Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kupambana na ugonjwa wa Malaria, bado ugonjwa huo unaendelea kuwaathiri wananchi wakiwemo watoto:-

Je, Serikali inaweza kutuambia hatua zilizofikiwa za kutokomeza ugonjwa huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikitekeleza afua na kazi mbalimbali za kudhibiti ugonjwa wa malaria nchini na kufanikiwa kupunguza kiwango cha maambukizi ya Malaria kutoka zaidi ya asilimia 40 mwanzoni mwa miaka ya 2000 mpaka asilimia 7.5 mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara inatekeleza Mpango Mkakati wa Malaria (*National Malaria Strategic Plan 2021 – 2025*) ambao umeweka malengo ya kupunguza kiwango cha Malaria kutoka asilimia 7.5 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 3.5 ifikapo mwaka 2025. Lengo mahususi ni kutokomeza kabisa ugonjwa wa Malaria ifikapo 2030.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maida Abdallah, swali la nyongeza.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naipongeza sana Serikali kwa kuweza kuweka mkakati madhubuti...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa uliza swali.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa mapambano dhidi ya malaria nchini Tanzania yalianza toka mwaka 1890; na wengi tunafahamu kwamba suala la malaria linatokana na mbu; kwa vile tunacho kiwanda kinachozalisha dawa ya viuadudu ambayo inamaliza kabisa mazalia ya mbu: Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kuzitaka Halmashauri kutenga bajeti katika bajeti zao ili kuweza kununua dawa hizi kila Halmashauri iweze kudhibiti malaria kupitia kila Halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa wenzetu toka nje ya nchi wanakithamini sana na kuona umuhimu wa kiwanda hiki na dawa hii inayozalishwa Tanzania: Je, Serikali kupitia Wizara hii inatoa elimu gani kwa wananchi kuhusiana na suala la dawa zinazozalishwa na kiwanda hiki kilichoko Kibaha? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Maida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ni namna gani tutakitumia kiwanda ambacho kiko Kibaha kuweza kushirikiana nacho kumaliza tatizo la malaria? Hili tunalichukua. Vile vile ndani ya swali la kwanza ameuliza Halmashauri itafanyaje? Tutaenda kushirikiana na TAMISEMI na hasa kwa sababu kuna tozo ambazo zimekuwa zikitozwa kule Halmashauri zinazotokana na masuala ya afya, fedha hizo zinaweza zikatumiwa asilimia fulani, vile vile kusaidia kugharamia eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili linaonekana linahusu elimu. Nafikiri kwenye *strategic* ya mwaka 2021 – 2025 kwa kweli tutakwenda kuwekeza kwenye eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelishauri. Tunachukua ushauri wake na tutaenda kuufanyia kazi kwa nguvu zote kabisa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 47

Kumpata Mwekezaji Katika Shamba la Chai Kidabaga

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kumpata mwekezaji katika Shamba la Chai la Kidabaga?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nami ni mara ya kwanza leo kusimama katika Bunge lako Tukufu, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye ametujalia mema mengi. Pili, nakishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniadini na kunipa nafasi kuwakilisha katika Jimbo la Mufindi Kaskazini. Tatu, nawashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini ambao waliniadini na kunipa kura nyingi ili niweze kuwa mtumishi wao. Mwisho, kwa niaba ya familia yangu, nawashukuru sana, lakini kwa namna ya pekee mke wangu kwa kunipa ushirikiano ili niweze kuendelea kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kumpata mwekezaji mahiri katika Kiwanda cha Chai cha Kidabaga. Maandalizi ya kumpata mwekezaji huyo yameanza ikiwa ni pamoja na kukamilishwa kwa Andiko linalohusu Viwanda 17 vilivyokuwa vimebinafishwa lakini baadaye kurejeshwa Serikalini, kikiwemo Kiwanda cha Kidabaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, andiko hilo kwa namna ya pekee kuhusu Kidabaga linajumuisha mapendekezo ya muundo mpya wa uendeshaji wa kampuni utakaozingatia maslahi ya wakulima wa chai wa Kidabaga na kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara inaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya viwanda vilivyorejeshwa Serikalini ikiwa ni pamoja na Kiwanda cha Chai cha Kidabaga. Hivyo, Serikali itakamilisha mchakato huo mapema iwezekanavyo ili mwekezaji mahiri aweze kupatikana kwa ajili ya kuwekeza katika shamba hilo la Kidabaga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa ni zaidi ya miaka 30 sasa tangu wakulima wa chai wa Kilolo wapande chai yao na kujengewa kiwanda ambacho hakijawahi kufanya kazi; na kwa kuwa katika muda huo wako Mawaziri kadhaa na Manaibu wameenda kule wakapiga picha kwenye mandhari nzuri za mashamba yale na kuahidi wananchi wale kwamba shughuli hiyo itakamilika mapema iwezekanavyo na hawakurejea tena. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi wa Kilolo kwamba sasa kiwanda kile kilichojengwa na hakikuwahi kufanya kazi, kitafanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa mchakato mingi imepita ya kumpata mwekezaji na mchakato wa mwisho ulikuwa mwaka 2019 na wawekezaji

walijitokeza na wakapatikana na wako tayari, na kwa kuwa uwekezaji huu haukukamilika kutokana na urasimu wa Serikali. Je, Serikali iko tayari kuwawezesha wale wawekezaji kwenda kuwekeza badala ya kuanza mchakato mwingine ambao unaweza ukachukua miaka mingine 30?Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali imefanya jitihada nyingi sana kuhakikisha kiwanda hicho kinafanya kazi. Kwa taarifa tu ni kwamba katika miaka ya nyuma tayari kuna wawekezaji walikuwa wamejitokeza kwa ajili ya kuwekeza katika kiwanda hicho na mmojawapo ni Mufindi *Tea and Coffee Company* chini ya *DL Group*. Hata hivyo, baada ya kupitia mchakato wa upatikanaji wa mwekezaji huyo ilionekana kwamba kuna baadhi ya vipengele vilirukwa lakini pia baada ya kuwa na *due diligence* ya kutosha ilionekana kwamba mwekezaji huyo alikuwa hana uwezo wa kuwekeza katika kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, juhudi hizo bado zinaendelea na kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba sasa tunaandaa andiko maalum ambalo litaangalia namna bora ya uendeshaji wa kiwanda/shamba lile likihusisha ushirikishwaji wa wadau wote kwa maana ya wakulima wadogo, halmashauri ya Kilolo lakini pia na Msajili wa Hazina ambaye ndiye anasimamia kiwanda hicho. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama ilivyo kwa wananchi wa Kilolo, ni

lini Serikali itakiamuru Kiwanda cha Chai cha Katumba kuongeza bei ya chai kwa wakulima wadogo wadogo katika Wilaya ya Rungwe?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya chai katika soko la dunia hivi karibuni iliyumba kidogo. Kwa hiyo, kampuni nyingi za chai zimekuwa na changamoto ya soko katika kuuza chai zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei kwa wakulima wadogo wadogo naamini baada ya kutengemaa kwa soko la chai duniani sasa hivi ni dhahiri shairi kwamba kampuni nyingi za chai ikiwemo hiyo ya Katumba, Mbeya na nyingine zitaweza kuwaongezea bei wakulima kwa sababu sasa kuna uhakika wa soko katika soko la dunia.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tuendeleo na swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 48

Malipo kwa Wakulima wa Tangawizi Same Mashariki

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itawalipa wakulima wa tangawizi Mamba Myamba, Wilaya ya Same Mashariki ambao walifungiwa na *SIDO* mashine zisizo na kiwango cha kuchakata tangawizi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika wa Wakulima wa Mamba Myamba uliopo Wilaya ya Same, tarehe 21/05/2010 uliwapa *SIDO* kazi ya kutengeneza mtambo wa kuchakata tangawizi kupitia Halmashauri ya Same ambao ulikuwa unahusisha hatua tano za uchakataji ambazo ni kuosha, kukata, kukausha, kusaga na kufungasha. *SIDO* iliingia mkataba na Halmashauri ya Same na Chama cha Ushirika cha Msingi cha Mazao na Masoko. Mradi huo ulikuwa na thamani ya shilingi 88,895,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtambo huo ulikamilika na kulisimikwa tarehe 29/10/2012 na ulifanya kazi. Hata hivyo katika ufanyaji kazi wake kulikuwa na changamoto mbalimbali ambazo baadaye zilirkebishwa na mtambo huo tena kusimikwa upya tarehe 27/2/2015.

Aidha, *SIDO* ilinunua tangawizi kutoka kwa wakulima na kufanya majaribio katika mtambo huo ambao ulionekana kufanya kazi vizuri. Mpaka sasa mtambo huo unaendelea kufanya kazi vizuri na wana ushirika wanaendelea na shughuli zao za uchakataji wa zao la tangawizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mkataba ulioingwiwa na *SIDO*, majukumu ya *SIDO* yalikuwa ni kutengeneza na kufunga mtambo kazi ambayo ilikamilika. Hata hivyo, baada ya changamoto zilizojitokeza Serikali imeielekeza *SIDO* ishauriane na Halmashauri ya Same namna bora ya kutatua changamoto ambazo zimejitokeza kwa kushirikiana na Ushirika wa Mamba Myamba ili kuona changamoto walizonazo zinatatuliwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwanza napenda kusema kwamba Serikali imepotosha Bunge lako Tukufu kwa kusema uongo ambao haukubaliki. Je, Waziri anajua kwamba TAMISEMI chini ya Waziri Jafo waliunda Kamati ya Uchunguzi (*fraud*) mwaka 2018 na Kamati hii ilitoa mapendekezo kuonesha jinsi *SIDO* ilivyowaibia wakulima pamoja na Halmashauri ambayo haikufanya kazi yake vizuri kuwasahauri wakulima na michango ambayo ilitolewa na Rais wakati huo Kikwete, karibu shilingi milioni 300 haikutumika vizuri na akaomba hatua madhubuti zichukuliwe na *SIDO* ilipe hela zile za wakulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri ana habari kwamba kutokana na kutofanya kazi kwa mitambo ile ndiyo maana sasa hivi *PSSF* imenunua mitambo mipya na inaifunga kwa kuona kwamba mitambo ile iliyofungwa ilikuwa batili? Inakuwaje Waziri...

NAIBU SPIKA: Umeshauliza maswali mawili tayari. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kaboyoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme hakuna uongo ambao umesemwa katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba *SIDO* baada ya kuingia mkataba ule na kuweza kufunga mtambo ule kulikuwa na changamoto mbalimbali na hasa kwenye upande wa ukaushaji katika mchakato ule. Baada ya kujadiliana na Halmashauri ya Same ikaonekana kwamba wakulima wale walikuwa hawaridhishwi na utendaji wa mitambo ile kwa hiyo *SIDO* ilishirikiana na mradi wa *Market Infrastructure, Value Addition And Rural Finance - MIVARF* kuagiza mtambo mpya

ambao ulikuwa na gharama ya shilingi milioni 29 na *SIDO* walichangia katika mtambo huo mpya shilingi milioni 9 na ukafungwa kama nilivyosema tarehe 27/02/2015 na ukaendelea kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hasara au gharama ambazo zilikuwa zimeingiwa na wakulima wale baada ya kuwa mtambo ule haufanyi kazi vizuri, kama nilivyosema tunaelekeza *SIDO* waweze kufanya mashauriano na Halmashauri ili waone namna gani ya kuwafidia wakulima wale ambao walipoteza mazao yao kipindi kile ambapo mtambo ule ulikuwa haufanyi kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtambo uliopo sasa hivi unafanya kazi vizuri na yeye atakuwa ni shahidi. Wakulima wale wameridhika na wanaendelea kufanya kazi zao za kuchakata zao la tangawizi.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kaboyoka, naomba ukae. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. (*Makofi*)

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi ndiye niliyeshirikiana na wananchi wale tukajenga kiwanda hikina juzi hapa ndani ya Bunge hili nimekiri kwamba kulikuwa na udhaifu kwenye kiwanda kile. Ndugu zangu ni bora kufanya jambo bovu kuliko kutokufanya chochote ndani ya miaka mitano. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Aaaaaa.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kile kisingejengwa pale kikawa na ubovu ule, *PSSF* asingekuwa kuwekeza na sisi kutatua tatizo lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema hivi, naomba suala la Kiwanda cha Tangawizi waachiwe Halmnashauri ya Wilaya ya Same na Mbunge aliyeko madarakani na *PSSF*. Ahsante sana. (*Makofi/Vigelegele*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hilo halikuwa swali ulikuwa ushauri. (*Makofi*)

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 49

Ujenzi wa Barabara ya Bigwa - Kisaki

MHE. HAMISI S. TALETALE aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Bigwa – Kisaki itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mwaka 2020 – 2025 inavyoelekeza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Bigwa – Mvuha – Kisaki ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilometa 133.28 ambapo kilometa 18.4 ni za lami na kilometa 115.14 ni za changarawe. Barabara hii ni kiungo muhimu kwa Mkoa wa Pwani na Morogoro na pia ni barabara inayoelekea katika Mradi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere katika Mto Rufiji ambalo ujenzi wake unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii ilikamilika mwezi Novemba, 2017 chini ya Kampuni ya Uhandisi ya *UNITEC Civil Consultants Ltd* ya Tanzania kwa ushirikiano na Kampuni ya *Multi-Tech Consult (Pty) Ltd* ya Gaborone, Botswana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Wakati Serikali inatafuta fedha za ujenzi, imeendelea kutenga fedha za matengenezo mbalimbali ili barabara hii iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 1,492 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara husika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, swali la nyongeza.

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza samahani, kwa kuwa leo ni siku yangu ya kwanza na mara yangu ya kwanza kuongea, napenda niwashukuru ndugu zangu wa Morogoro Kusini Mashariki. Pia nishukuru familia yangu, mama yangu mzazi na marehemu mke wangu popote alipo, Mungu amlaze mahali pema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majibu ya Serikali na kwa kutambua ufinyu wa bajeti na kuzingatia umuhimu wa barabara hii, je, Serikali iko tayari kushirikiana nami kutafuta mkandarasi wa *building and finance?* (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nimemuelewa vizuri kwamba Serikali itashirikiana naye kutafuta mkandarasi,

utaratibu wa kutafuta wakandarasi ni utaratibu ambao uko kisheria na ni utaratibu ambao unatekelezwa na Serikali kupitia mamlaka husika.

Mheshimiwa Maibu Spika, kwa kuwa tumeahidi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais katika hotuba yake barabara anayoizungumzia ameahidi, hivyo, nimhakikishie tu kwamba itajengwa na kukamilika katika kipindi hiki cha miaka mitano ambayo Ilani hii itakuwa inatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nadhani sehemu ya swali lake kuhusu kushirikiana naye yaani huo ushirika unakuwa kwenye ile hoja ya kutafuta mkandarasi ambaye atajenga na kuwapa barabara, sio ule utaratibu wa kawaida. Ndiyo swali lake lilikuwa hapo lakini hilo ni jambo ambalo mnaweza mkalitazama kama Serikali kwamba ni jambo linalowezekana kufanya hivyo kwenye ujenzi wa barabara pia. Yaani apewe mtu ajenge, a-*operate* barabara halafu baadaye atoe kwa watu waendeleo na matumizi yao. Nadhani ndipo hoja yake ilipokuwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna maswali mengi sana hapa yanayohusu barabara. Napata wakati mgumu lakini watapata wachache wetu pamoja na kwamba nawaona mmesimama wengi sana. Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Makete naomba kuuliza kuhusu ujenzi wa barabara ambayo ipo kwenye Ilani ya kutoka Chimala – Matamba – Kitulo kilometa 51, ilikuwa ni ahadi ya Waziri Mkuu mstaafu, kwa muda wa miaka 10 hadi sasa haijatekelezwa. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI, UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara anayoizungumzia Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete ni kati ya barabara ambazo zimetajwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuanzia ukurasa wa 72 – 76. Pia katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Rais ameeleza kwamba katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii pamoja na ahadi alizozitoa atahakikisha kwamba anajenga na kukamilisha barabara zote ambazo zinaendelea zenye urefu wa kilometa 2,500 lakini pia ataanza ujenzi na kukamilisha barabara zenye urefu wa kilometa 6,006 na barabara hii ya Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete ni kati ya barabara ambazo zimetajwa ama zimetolewa ahadi na mwenyewe Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nimpe uhakika kwamba barabara hiyo itajengwa na kukamilika.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara ya Bugeme – Nkwenda – Isingiro mpaka Mrongo yenye urefu wa takribani kilometa 135 ikiunganisha Wilaya ya Kyerwa na Karagwe, lakini Kyerwa na Uganda. Swali, ni lini Serikali itakamilisha, ni lini Serikali itajenga hii barabara kwa kiwango cha lami kwa kuzingatia umuhimu wa hiyo barabara na hasa wakazi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anatropia swali lako lilivyoisha nilikuwa nimekata maneno. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge ambaye ameelezea barabara yenye urefu wa

kilometa 135 ambayo ni ya Kyerwa – Karagwe, lakini pia inakwenda Uganda:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika swali la nyongeza Mheshimiwa Rais amesema atakapokuwa anakamilisha barabara zote za kilometa 2,500 na kilometa 6,006 tutakuwa tumeunganisha wilaya zote za Tanzania kwa kiwango cha lami, mikoa yote ya Tanzania kwa kiwango cha lami, lakini pia na barabara kuu zote (*trunk roads*) ambazo zinaunganisha nchi na nchi kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimpe uhakika Mheshimiwa Mbunge aliyeuiliza kwamba, barabara hiyo ni kati ya barabara ambazo zitatekelezwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali.

Na. 50

Ujenzi wa Barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga

MHE. FRANCIS L. MTEGA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga (kilometa 151) utaanza kwa kuwa upembuzi yakinifu umekamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga yenye urefu wa kilometa 152.1 ni Barabara ya Mkoa ambayo ipo chini ya Wakala wa Barabara

(*TANROADS*). Sehemu ya barabara hii, yani Rujewa hadi Madibira yenye urefu wa kilometa 97.1, inahudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Mbeya na sehemu iliyobaki kipande cha Madibira hadi Kinyanambo chenye urefu wa kilometa 55, kinahudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Iringa. Barabara hii ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 na ahadi za Viongozi Wakuu wa Nchi kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii ambayo inapita katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya mpunga na mahindi, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara ilifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara hii. Wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi, Wizara kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) inaendelea kufanya matengenezo ya barabara hii ili ipitike majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2020/2021, barabara hii imetengewa kiasi cha shilingi milioni 757 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali na shilingi bilioni 3,380,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Francis Mtega, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, pamoja na *TANROADS* kujitahidi kukarabati barabara ile, lakini nyakati za masika imekuwa ikikata kabisa mawasiliano; na kwa kuwa, amekiri kwamba, ni muhimu sana kwa kusafirisha mazao na isitoshe wananchi wale wanaitegemea sana barabara ile kwa huduma mbalimbali za kijamii kupeleka wagonjwa hospitali, lakini bidhaa mbalimbali za matumizi ya kila siku. Je, Serikali haioni

kwamba, sasa ipewe kipaumbele ili ujenzi wa barabara ile kwa kiwango cha lami uanze haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mkoa wa Mbeya tuna uwanja mkubwa wa ndege wa kimataifa na Mheshimiwa Rais amenunua ndege kubwa, *Dreamliner* na barabara ile inapita kandokando mwa lango kuu la Kusini kuingia Hifadhi ya Ruaha (*Ruaha National Park*), sasa watalii wangepitia lango lile la Kusini kwa urahisi kabisa. Je, Serikali haioni kwamba inakosesha pato la Taifa hasa pesa za kigeni? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kwa sababu ya umuhimu wa hiyo barabara ndio maana tayari taratibu za kuanza kujenga kwa kiwango cha lami zimeshaanza na zimeshatengwa tayari bilioni 3.38 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali kwamba, kwenye bajeti zinazofuata nina hakika barabara hii itatengewa fedha zaidi, ili iweze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya umuhimu huu kama alivyosema kwenye swali lake la pili kuhusu uwanja wa ndege nasema ndio maana tayari hii barabara kwa Serikali kutambua umuhimu wake ikiwa ni kupokea wageni kutoka uwanja wa Songwe, lakini na kuwapeleka kwenye mbunga, ndio maana tayari taratibu za Serikali zimeanza za kukamilisha ama kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imefanya kazi nzuri ya kujenga barabara kwenye Jiji la Arusha na hasa ukizingatia kwamba, barabara ya mzunguko ya *bypass* ambayo imesaidia sana kwa watalii na wananchi wa Jiji la Arusha, lakini bado kuna kipande cha Kata ya Moshono ambacho kinatoka eneo la kona ya Kiseliani kuunganisha barabara ya *bypass* maarufu kama barabara ya *TPackers* Osunyai kama kilometa saba. Je, Wizara ya Ujenzi haioni sasa ni wakati sahihi wa kumalizia kipande hiki ili kupunguza msongamano na kuweka mazingira mazuri zaidi ya utalii pamoja na wananchi wa Kata ya Moshono?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye ukurasa wa 77 barabara za *bypass* kwa ajili ya kupunguza msongamano zimeainishwa zikiwemo Miji ya Dar-Es-Salaam, Mbeya na Arusha ni kati ya miji ambayo zitanufaika na barabara hizi za mzunguko kwa ajili ya kupunguza misongamano. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha kwamba, barabara hii aliyoitaja ni moja ya barabara ambazo zitatekelezwa katika kipindi hiki tutakachoanza bajeti katika kipindi hiki cha miaka mitano. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mbozi napenda kuuliza swali kuhusu Barabara la Mlool – Kamsamba mpaka Kilimamatundu na kutoka Utambalila mpaka Makao Makuu ya Wilaya ya Momba, Chitete, kilometa 145. Kwa kuwa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeshakamilika; na kwa kuwa nyaraka za tenda ziko tayari.

Je, ni lini barabara hii itatengewa fedha na kutangazwa ili ijengwe kwa kiwango cha lami kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi na kama Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi inavyoelekeza kwa mwaka 2020 - 2025?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara anayoisema ya Mbozi – Mtambalila mpaka Kamsamba ni barabara ambayo, kama alivyosema imeshafanyiwa usanifu na ni kati ya barabara ambazo zimeahidiwa kwanza kwa bajeti zinazokuja zitajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mwenisongole kwamba, barabara yake iko kwenye mpango na zitaendelea kujengwa barabara kadiri ya fedha itakavyopatikana katika kipindi hiki cha kuanzia mwaka wa fedha wa 2021/2022 mpaka 2025/2026, asante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza kwa kuwa Barabara ya Rujewa – Madibira inafanana na ile barabara ya Arusha – Simanjiro – Kiteto pamoja na Kongwa kilometa 430 ambayo imeahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 - 2025 pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Rais. Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu langu la msingi na bado natambua kwamba, barabara anayoulizia, kama mwenyewe alivyosema, iko kwenye Ilani lakini pia iko kwenye ahadi ya Rais, lakini pia iko kwenye hotuba ya Rais.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hiyo pia, kadiri Serikali itakavyoendelea kutafuta na kadiri fedha zitakavyopatikana ni kati ya barabara ambazo tunategemea kuzikamilisha ili tuweze kuunganisha wilaya zote, mikoa yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuelekee Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 51

Soko kwa Zao la Pareto

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uzalishaji wa zao la pareto ambalo mahitaji yake duniani ni makubwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya maua makavu ya pareto duniani ni wastani wa tani 11,000 na yanatarajiwa kuongezeka kwa asilimia mbili hadi kufikia tani 14,000 kwa mwaka ifikapo 2025. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa matumizi ya viuatilifu na bidhaa za tiba kwa kuwa, *pyrethrin* ni halisi kwa maana ni *organic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zinazoongoza kwa uzalishaji wa pareto duniani ni Australia, Tanzania, Rwanda na Papua Guinea ambapo Tanzania inazalisha wastani wa tani 2,400. Bei ya pareto inategemea kiwango cha sumu kinachopatikana kwenye pareto na kwa sasa mkulima anapata malipo ya awali ya Sh.2,500 kwa kilo na hadi mwisho wa kukamilika kwa mzunguko wa mauzo inafikia hadi Sh.4,000 kwa kilo kutegemea kiwango cha sumu inayopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya pareto duniani malengo ya awali ni kuongeza uzalishaji wake kutoka wastani wa tani 2,400 kwa mwaka hadi kufikia tani 3,200 ifikapo mwaka 2025. Aidha, kufikia malengo hayo Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuanzisha mashamba ya pamoja, kwa maana ya *block farming*, kwenye halmashauri zinazozalisha pareto ikiwemo Halmashauri za Mbulu na Mufindi ambazo zimeonesha utayari wa kutenga maeneo ya mashamba ya pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mikakati mingine tumeanzisha mfumo wa uendelezaji wa zao wa kanda (*zone*) unaowashirikisha wawekezaji na wadau wote kwa mnyororo wa thamani. Ili kudhibiti ulanguzi wa pareto tumeelekeza halmashauri zote zinazolima pareto kuanzisha na kuimarisha vituo rasmi vya ununuzi wa pareto badala ya kuuza pareto majumbani na kwenye maeneo ya maficho. Vilevile katika kuhakikisha mkulima anapata bei nzuri kulingana na ubora wa pareto, Serikali imeanzisha utaratibu wa kuweka mtaalam wa maabara wa Serikali kutoka *TARI/Uyole* kwa ajili ya kuhakiki viwango vya sumu kiwandani badala ya kutegemea viwango vinavyotumiwa na wanunuzi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa majibu yake mazuri na mkakati uliopo, lakini ukiangalia mkakati wa kuongeza uzalishaji kutoka tani elfu mbili, elfu tatu, elfu mbili mia nne kufika elfu tatu na mbia mbili hiyo bado ni asilimia 25 tu ya mahitaji ya dunia. Sasa kwa vile pareto inatumika kwa ajili ya kuuwa wadudu na hasa dawa za kuhifadhi mazao ambayo itapunguza *cost, post harvest loss* kwa nafaka zetu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri agizo lake alilolitoa kuhusu taasisi yetu ya *TARI* ili waweze kuanza kufanya utafiti wa kuzalisha dawa kwa ajili ya kuondoa hii *post harvest loss*, lakini vilevile na dawa kwa ajili ya kuuwa wadudu wa mbu, ni lini hilo agizo lake litaanza kutekelezwa? Nafikiri ni muhimu sana tukichukulia ushindani ulioko kwenye nchi zetu za Afrika Mashariki wenzetu Kenya pamoja na Rwanda kama ulivyosema wewe mwenyewe wameshaanza huo uzalishaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia kuhusu *zoning* ambayo hairuhusu wanunuzi wengi kwenye eneo moja. Hiyo limekuwa ni changamoto kwa bei ya pareto kuwa ndogo sana kwa vile kunakuwa na *monopoly* ya hao wanunuzi. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuna umuhimu wa kuruhusu wanunuzi wengi kwa kila eneo ili kuwepo na bei ya ushindani? Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyingeza ya Mheshimiwa Njeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza agizo ambalo tumelitoa mwaka jana Serikali na sekta ya kilimo inatumia

zaidi ya bilioni 150 kwa mwaka kwa ajili ya kununua *input* kwa maana ya gharama za viuatilifu na vitu vya namna hiyo. Ni kweli kwamba, pareto ni moja ya zao ambalo linaweza kutupunguzia gharama kwa kiwango kikubwa cha uagizaji wa viuatilifu. Wizara ya Kilimo mwaka jana tumewapa agizo watu wa *TARI*, hivi sasa tunavyoongea utafiti unaendelea ukihusisha sekta binafsi pamoja na kampuni ya *PCT* ambayo ndio kiwanda pekee kinacho-*process* kwenda kwenye *crude level* uzalishaji wa maua haya kwa ajili ya kupatikana dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwahamasisha sekta binafsi ya Tanzania, ni *commitment* ya Serikali kuanzia taasisi zetu kama *NFRA* na *CPB* kuanza kutumia unga unaotokana na pareto kuzuwua wadudu waharibifu wanaoingia katika mazao kama mahindi na hii itatuongezea soko la ndani. Sisi kama Wizara tunatoa *commitment* kama kuna muwekezaji yeyote ambaye atazalisha kiuatilifu kinachotokana na pareto kwa ajili ya matumizi ya viuatilifu ndani ya nchi yetu tutampa *contract* ya kuhudumia zao na taasisi ambazo ziko chini ya Wizara ya kilimo. *This is a commitment* na tuko tayari kwa hiyo, tunahamisha sekta binafsi kuwekeza. Namfahamu Mheshimiwa Njeza ni mdau katika sekta hii na Mheshimiwa Rais alisema mabilionea karibu Wizara ya Kilimo tujadiliane juu ya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *zoning*. Hatuwezi kuondoa *zoning* kwenye suala la uwekezaji. Ni *unfair* mwekezaji kampatia huduma mkulima, kampa mbegu, kampa dawa, kampa ugani, halafu umruhusu mtu ambaye hajawekeza aende akanunue zao ambalo mwenzake kawekeza. Tutaendelea ku-*protect zoning* katika eneo hili, lakini tutafungua milango kwa yeyote anayetaka kuja kuwekeza kwenye sekta ya pareto, ili tuweze kuwapa thamani wakulima wetu na sisi ndani ya Wizara ya kilimo *we are open for this*. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

Na. 52

**Ukarabati wa Skimu za Mnazi Kwemkwazu na
Mng'aro – Kitivo- Mlalo**

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kukarabati miundombinu ya Skimu za umwagiliaji za Mnazi – Kwemkwazu na Mng'aro – Kitivo ambazo zimeharibiwa kabisa na mvua?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Jimbo la Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua athari zilizosababishwa na mvua zilizonyesha msimu 2019/2020 na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya umwagiliaji na baadhi ya mito kuhama ambapo takriban skimu 70 za umwagiliaji nchini ziliathirika zikiwemo skimu za Kwemkwazu – Mnazi na Kitivo - Mng'aro katika Jimbo la Mlalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha miundombinu ya umwagiliaji inarejea katika hali ya kawaida, Serikali imeanza kukarabati miundombinu hiyo katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo eneo la Ruaha Mbuyuni, Mlenge na Magozi Iringa Vijijini. Aidha, Serikali itaendelea kukarabati miundombinu ya skimu nyingine kwa haraka zikiwemo skimu za Mnazi na Kitivo, Mng'aro katika Jimbo la Mlalo na zitapewa kipaumbele ili kuhakikisha zinakamilika na kurudi katika hali yake ya kawaida na hivyo kuwahudumia wakulima wa maeneo hayo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Shangazi swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri na Serikali wamekiri kwamba takriban skimu 70 zina changamoto na kule Mng'aro hivi tunavyozungumza ni msimu wa mpunga lakini wanashindwa kwenda mashambani kwa kuwa skimu haiwezi ikaririsha maji kuelekea mashambani. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka sana kuhakikisha kwamba skimu hii ya Mng'aro inatiririsha maji kuelekea mashambani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kulikuwa na maelekezo ya Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Chama alipotembelea Mkoa wa Tanga kwa maana kwamba Wizara ya Kilimo itembelee ikaone skimu hizi. Kwa sababu kuamini ni kuona, je, Waziri yuko tayari sasa kutenga muda na nafasi kwenda kuziona skimu hizi ambazo ni muhimu sana kwa uzalishaji wa mpunga katika Mkoa wa Tanga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya ngonyeza ya Mheshimiwa Rashid Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Wizara ya Kilimo kwenda Mlalo, hivi karibuni tulikuwa Mkoa wa Tanga na Mheshimwia Waziri Mkuu lakini bahati mbaya hatukuweza kufika Jimbo la Mlalo. Nakata nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa mimi mwenyewe niko tayari tukutane tupange ili tuweze kwenda pamoja katika maeneo ya Mlalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu suala la kukarabati skimu hizi tatu tulizozitaja, kwanza *practically* sasa hivi ni kipindi cha mvua kwa hiyo ukarabati itakuwa ni vigumu sana kuufanya. Nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumetenga fedha kupitia Tume ya Umwagiliaji kiasi cha shilingi milioni 30 kwa ajili ya kurekebisha skimu za Mlalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada tu ya msimu huu wa mvua kuisha Wizara ya Kilimo tutatumia mfumo ambao

tumeutumia kama majaribio maeneo ya Ruaha na Jimbo la Mheshimiwa Lukuvi kwa kutumia *force account* kufanya marekebisho ya skimu hizi na wala hatutumia wakandarasi, tutatumia vifaa vyetu wenyewe. Tutaenda kufanya hivyo *immediately* baada ya msimu wa mvua kuisha na tumetenga fedha kwa ajili ya skimu zake tatu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Daudi Protas Venant, Mbunge wa Igalula sasa aulize swali lake.

Na. 53

Mpango wa Kupeleka Umeme Vijiji 46 – Igalula

MHE. VENANT D. PROTAS aliuliza:-

Jimbo la Igalula lina jumla ya vijiji 58, ambapo Vijiji 12 vimepata umeme na vijiji 46 bado havijapata umeme:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika vijiji 46 ambavyo havijapata umeme?

(b) Je, gharama za kuunganisha umeme kwa kila mwananchi ni kiasi gani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daud Protas Venant, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vilivyobaki 46 katika Jimbo la Igalula vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* awamu ya III mzunguko wa pili unaoanza katikati ya mwezi Februari 2021. Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miezi

18 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, 2022. Kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huo, kutafanya vijiji vyote katika Jimbo la Igalula kupatiwa umeme.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya kuongeza kasi ya kutoa huduma ya umeme nchini mwaka 2019, Serikali kupitia *TANESCO* ilipunguza bei ya kuunganisha huduma ya umeme kwa wananchi wanaoishi vijijini na maeneo yanayofanana na hayo kutoka wastani wa shilingi 725,000/= kwa mita za njia tatu (*three phase*) hadi shilingi 139,000/= ikiwa ni punguzo la asilimia 80. Vilevile kwa mita za njia moja (*single phase*) kutoka wastani wa shilingi shilingi 177,000/= hadi shilingi 27,000/= sawa na punguzo la asilimia 84.75. Kwa ujumla, gharama hizo ni tozo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daud Protas Venant, swali la nyongeza

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri Nishati lakini nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri ya Wilaya ya Uyui hasa Jimbo la Igalula tuko nyuma sana katika kuunganishiwa nishati ya umeme. Wakati wa kampeni Mheshimiwa Waziri alikuja tukazindua mradi mkubwa lakini mara baada ya kuondoka yule mkandarasi hakuendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa kupeleka umeme kwenye kata zaidi ya sita zilizoko katika Jimbo la Igalula na vijiji vyake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa umeme jazilizi katika vijiji vya kata ya Goeko Msasani, Igalula Stesheni na Kigwa Majengo Mapya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine, umeme umekuwa changamoto sana ...

NAIBU SPIKA: Umeshauliza maswali mawili Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Protas Venant wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kujibu kwenye jibu la msingi kwamba vijiji vyote 46 vilivyobaki katika Jimbo la Igalula vitapatiwa umeme kuanzia mwezi Februari kwa miezi 18 kwenye mradi wa *REA III* mzunguko wa pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili ambalo nadhani ndilo la nyongeza alikuwa anasema kwamba mwaka jana Mheshimiwa Waziri alizindua mradi wa umeme jazilizi (*Densification*) awamu ya pili, *Densification 2A*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Igalula, Mkoa wa Tabora ni mojawapo ya mikoa 9 inayonufaika na *Densification 2A* ambayo ilianza mwaka jana na tayari ilishazinduliwa kwa Mkoa wa Tabora. Mkandarasi anayefanya kazi katika Mkoa wa Tabora anayo *Lot* moja ambayo ina mikoa miwili; Tabora na Singida na atafanyakazi hiyo kwa shilingi bilioni 9.7. Tayari *mobilization* imeshaanza, ameshafanya *survey* katika Jimbo la Igalula na amekamilisha na tunatarajia muda wowote kufikia mwezi wa nne atakuwa tayari ameanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge kwamba amekuwa akifuatilia hata ofisini kuulizia *Densification 2A* itaanza lini kwenye Jimbo lake, tunamhakikishia kabla ya mwezi Aprili upelekaji wa umeme kwenye vitongoji vilivyoko katika Jimbo la Igalula utakuwa umeanza.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 54

Huduma za Umeme katika Wilaya ya Muleba

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO aliuliza:-

Ofisi ya *TANESCO* Wilaya ya Muleba inazidiwa na wingi wa wateja kutokana na miradi ya *REA*.

Je, ni lini Wilaya hiyo itapewa hadhi ya Mkoa wa *TANESCO* ili iweze kutoa huduma kwa wakati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Umeme nchini (*TANESCO*) limekuwa likiweka ofisi za Mikoa katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ongezeko la shughuli za kiutendaji za Shirika na mahitaji ya umeme pamoja na wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusogeza huduma kwa wateja karibu Wilayani Muleba, *TANESCO* imefungua ofisi ndogo (*sub-office*) eneo la Kamachumu na imeshaanza kutoa huduma kwa wateja wa Kamachumu katika Jimbo la Muleba Kaskazini na maeneo mengine ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *TANESCO* inatarajia kufungua ofisi ndogo (*sub-office*) nyingine eneo la Kyamyorwa na Bulyage ili kusogeza karibu zaidi huduma kwa wateja wa maeneo hayo na jirani. Ofisi hizo zitakuwa na wafanyakazi pamoja na vitendea kazi vyote vinavyohitajika ikiwa ni pamoja na usafiri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Wizara, ninayo maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, wakati wananchi wa Muleba wakisubiria hizi hatua ambazo Wizara inazichukua, je, Serikali iko tayari kuiongezea nguvu Ofisi ya *TANESCO* iliyopo kwa sasa kwa kuiongezea wafanyakazi na vitendea kazi ili wakati tunaendelea kusubiria iendeleo kutoa huduma stahiki kwa wananchi wa Wilaya ya Muleba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Wilaya ya Muleba inavyo visiwa 39 na kati ya hivyo, visiwa 25 vinakaliwa na wavuvi ambao wanachangia pato la taifa. Je, Wizara na Serikali ni lini itavipelekea umeme wa uhakika na wa bei nafuu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TANESCO* imeendelea kutoa huduma kwa wananchi na kuhakikisha kwamba huduma ya umeme inapatikana kwa uhakika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwamba tutaendelea kupeleka huduma ya umeme kwa wananchi na kuhakikisha kwamba ofisi ya *TANESCO* Muleba lakini na maeneo mengine yote nchini zinafanya kazi vizuri kabisa. Serikali tayari imeshaongeza nguvu kazi katika maeneo mbalimbali kwa kupeleka watumishi na vifaa mbalimbali ikiwemo vitendea kazi na magari. Tunaahidi kwamba tutaendelea kuboresha utendaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili, kama nilivyokuwa nimetangulia kusema kwamba miradi inayopeleka umeme visiwani ni miradi inayoitwa *off grid*, maeneo ambapo Gridi ya Taifa haijafika na Muleba ni mojawapo ya maeneo ambayo ina visiwa vingi vinavyokaliwa na watu vinavyohitaji kupata huduma ya umeme. Tayari wako watu ambao walikuwa wanapeleka umeme huko ikiwemo kampuni ya JUMEME lakini gharama yake ilikuwa ni kubwa na Serikali ilitoa maelekezo kwamba gharama hiyo ya unit 1 kwa Sh.3,500 ishuke na kufikia shilingi 100. Maelekezo hayo tayari yameshaanza kutekelezwa. Kama bado kuna tatizo katika maeneo hayo basi tunaomba taarifa hiyo itolewa ofisini ili tuendeleo kusimamia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Serikali inao mpango wa kufikisha umeme wa *TANESCO* katika maeneo hayo kwa kadri bajeti itakavyoruhusu au kuweza kusimamia ile miradi ili iweze kutoa umeme wa uhakika na kwa gharama nafuu kwa wananchi wote wanaoishi visiwani.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 55

Sheria Kandamizi kwa Wanawake

MHE. ZAINAB A. KATIMBA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha baadhi ya Sheria kandamizi kwa Wanawake ili ziendane na wakati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu nasimama mbele ya Bunge lako kwa mara ya kwanza. Pia niwashukuru wananchi wa Kavuu kwa kunidhinisha kuwa Mbunge wao. Vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniona nafaa kuwakilisha Wizara hii ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum kupitia Mkoa wa Kigoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kabla ya kujibu swali la msingi, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali haina sheria kandamizi. Sheria zote zinazotumika nchini zilitungwa na Bunge lako Tukufu ambalo halijawahi kutunga sheria kandamizi. Aidha, Serikali kwa kuzingatia mahitaji ya wakati na watu wake, imekuwa ikiwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuziboresha sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wakati tulionao na mahitaji ya sasa, Serikali imeanzisha mchakato wa kuzipitia baadhi ya sheria ili ziweze kufanyiwa marekebisho kuendana na wakati. Hivi sasa, Serikali kupitia Wizara imeandaa Muswada wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Ndoa utakaowasilishwa katika Bunge lako Tukufu ili kuiboresha, kwa lengo la kulinda makundi ya wanufaika na sheria hii. Aidha, Serikali inaendelea na hatua mbalimbali za kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mirathi na Sheria za Kimila. Hatua hizo zikikamilika, Muswada wa Mapendekezo ya kuzirekebisha sheria hizo utawasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu ili Wabunge wapate nafasi nzuri ya kujadiliana na kuyapitisha marekebisho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ipo katika mabadiliko makubwa ya kuhakikisha kunafanyika maboresho makubwa ya sheria zetu ikiwemo kuzitafsiri kwa Kiswahili lakini pia kuweka vipengele kwenye sheria hizo vya kutoa hukumu kwa lugha ya Kiswahili

jambo ambalo litaleta tija kubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Tunawaomba Wabunge kuunga mkono juhudi za Serikali katika eneo hili kwa lengo la kuimarisha utawala wa sheria na upatikanaji wa haki nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Aidha, nina swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile Serikali ilivyoona umuhimu wa kuanzisha Mahakama kwa mfano za Kazi (*Labor Courts*) au Mahakama za Mafisadi (*Economic Crimes Courts*) au *Commercial Courts* (Mahakama ya Biashara) kwa ajili tu ya kutengeneza mazingira wezeshi ya kiuchumi lakini pia ya uwekezaji. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuanzisha Divisheni ya Familia (*Family Division*) katika Mahakama itakayoshughulika na masuala ya ndoa, talaka na mirathi ili kuharakisha mashauri haya na kuwaondolea wanyonge adha wanayopata ya kuchelewa kwa mashauri haya katika mfumo wa kawaida wa mahakama na hasa ukizingatia wanyonge hao ni wajane? Sisi tunajua kuna *legal maxim* ambayo inasema *justice delayed is justice denied* (haki iliyocheleweshwa ni sawasawa na haki iliyonyimwa). (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zainab, Mbunge Viti Maalum kutoka Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wake ni mzuri sana na chombo hiki ndiyo chombo chenye kazi ya kutunga sharia kwani sheria zote zinatungwa hapa Bungeni. Tusema tu tumepokea wazo lake na tutalipitisha katika mamlaka mbalimbali za kuangalia ile *modality* ya kuanzisha chombo

kama hiki ili tuweze sasa kufikia maamuzi halisi. Naamini Bunge lako Tukufu litapata nafasi ya kupitia na kutoa maoni mbalimbali juu ya muundo utakaowezesha kutoa haki kwa makundi husika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumalizie na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Fredrick Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli, sasa aulize swali lake.

Na. 56

Mradi wa Maji wa Bn 520-Arusha

MHE. FREDRICK E. LOWASSA aliuliza:-

Mradi wa maji wa BN 520 una ziada ya lita milioni 100 kwa mujibu wa wataalam na Mheshimiwa Rais alikubali ombi la ziada hiyo kujumuishwa kwenye mradi:-

Je, ni lini utekelezaji wa ahadi hiyo utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fredrick Lowassa, Mbunge wa Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa BN 520 katika Jiji la Arusha, ujenzi wa tanki la maji eneo la Mlima wa Ngorbob Kisongo umeshakamilika. Tanki hili litahudumia Kata ya Mateves, Olmoti na Monduli (Meserani, Kambi ya Sokoine, TMA na Monduli Mjini).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imefanya upembuzi yakinifu wa mradi wa kupeleka maji katika Kata

ya Mateves na Monduli (Meserani, Kambi ya Sokoine, TMA na Monduli Mjini). Mradi huo umepangwa kutekelezwa katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inajipanga kutekeleza mradi huo, Wizara kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha inatekeleza miradi miwili ya Lolomsikio na Komolonike ili kuboresha huduma ya maji Mjini Monduli. Miradi hiyo inatarajia kuongeza upatikanaji wa maji Mjini Monduli kutoka mita za ujazo 1,430 ya sasa mpaka 2121 na inatarajwa kukamilika mwezi Februari, 2021.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fredrick Edward Lowassa, swali la nyongeza.

MHE. FREDRICK E. LOWASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri. Ni kweli kwamba Wananchi wa Jimbo la Monduli wanamwamini sana Mheshimiwa Rais na wanaimani kubwa sana na ahadi yake, lakini ni kweli pia tunaamini uongozi wa Wizara ya Maji ukiongozwa na ndugu yangu Mheshimiwa Juma Awesso, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; tayari Monduli kuna miradi ambayo ipo ya maji lakini inasuasua, tunaomba kauli ya Serikali kuhusu mradi na mpango ambao mmejipanga nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tunaomba kuhakikishiwa usimamizi mzuri juu ya ahadi hii ya Mheshimiwa Rais. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Lowassa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miradi ambayo inasuasua mpango wa Wizara ni kuhakikisha kwamba miradi yote inakamilika kufikia wiki ya maji mwaka huu mwezi Machi na tayari wataalam wetu wanaendelea kufanyia kazi kwa maana ya miradi ambayo imetekelezwa kwa kutengeneza miundombinu lakini maji hayako bombani, tunatarajia kufikia mwezi Machi, Wiki ya Maji miradi hiyo itaanza kutoa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa ahadi ya Mheshimiwa Rais, wote tunafahamu ahadi ni deni na ahadi hii ni ya Mheshimiwa Rais, naomba nimpe amani Mheshimiwa Mbunge kwamba miradi hii tutakwenda kusimamia na nafahamu alikuwa na ahadi na Mheshimiwa Waziri kwenda jimboni kesho lakini ile safari imeahirishwa kwa sababu ya msiba mkubwa uliotokea pale ofisini kwa Mkuu wa Mkoa kwa hiyo hali itakapotulia kwenye Mkoa wa Arusha, Mheshimiwa Waziri atakwenda na kuhakikisha usimamizi unafanyika vizuri. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa tumalizie na swali la Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini.

Na. 57

Mradi wa Maji Njombe Mjini

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa kusambaza maji Mji wa Njombe kutoka Mto Hagafilo utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipata mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya *Exim* India jumla ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika miji 28 Tanzania Bara na Zanzibar. Moja ya miji itakayonufaika na mkopo huo ni Mji wa Njombe, kwa sasa mradi upo katika hatua za manunuzi na tunatarajia Wakandarasi watakuwepo eneo la mradi kwa ajili ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi ifikapo mwezi Aprili, 2021 na ujenzi wa mradi utachukua miezi 24.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa mradi huu kama alivyosema yeye mwenyewe utachukua miezi 24, miaka miwili na wananchi wa Njombe wakati huo wataendelea kupata tabu na kuteseka hasa wakati wa kiangazi maji yanapopotea kabisa. Je, Serikali itakuwa tayari kutekeleza miradi mingine midogo midogo ambayo baadhi imekwishabuniwa na inafahamika na mingine inaweza kubuniwa, kwa vile Njombe tumezungukwa na mito kila upande?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali ilishatekeleza mradi mdogo katika Mji wa Kibena pale Njombe, kwa kupeleka maji mpaka Hospitali ya Wilaya ya Njombe na kuna tanki kubwa sana wamelijenga pale na tanki hilo lina maji mengi na saa nyingine yanabubujika na kumwagika. Kwa bahati mbaya wananchi wa eneo la Kibena ambao wanaishi maeneo yale bado hawana. Je, Serikali haioni kama itakuwa ni busara na jambo jema badala ya maji yale kuwa yanabubujika na kumwagika sasa wakatoa pesa na kuweka mradi mdogo wa kutawanya maji ili wananchi wa Kibena wapate kuwa na maji ya uhakika? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwanyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la hofu kwa sababu mradi utaanza mwezi Aprili na yeye anapenda visima ama miradi midogo midogo, nipende tu kumwambia kwamba tayari Wizara inafanya mchakato huo na hili linashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mradi ambao unapeleka maji kwenye hospitali ya Kibena pale kwa kuhitaji *distribution* tayari Wizara imetoa maelekezo kwa mameneja walioko pale wanafanyia upembuzi yakinifu ili kuona namna gani kama *distribution* itawezekana. Naomba kukupa amani Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu ambao tunauanza mwezi Aprili, tutaenda kuufanya kwa kasi nzuri na tutaweza kutawanya maji kadri mradi unavyokamilika hatutasubiri mradi ukamilike mpaka mwisho, ukifika hata asilimia 40 wale ambao wanapitiwa na lile eneo ambalo miundombinu imekamilika maji yataweza kutoka. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Philip Mulugo, swali la nyongeza.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwanza napenda kupongeza Wizara ya Maji, Mheshimiwa Waziri Aweso na Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca ya kutembelea Mikoa yetu ya Kusini, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi na Njombe, kazi nimeiona, mmefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu moja la nyongeza, pale Mkwajuni Makao Mkuu ya Wilaya pana mradi mkubwa wa maji wa milioni 760 toka mwaka 2018. Mkandarasi ametumia fedha zake binafsi karibuni asilimia 80 anakamilisha mradi, lakini anakwamishwa na malipo ya Serikali baada ya kumaliza zile kazi, *certificate* anapeleka lakini halipwi. Galula pana mradi wa maji, Kapalala pana

mradi wa maji. Hii miradi mitatu kwenye jimbo langu imekuwa ni kero sana kwa wananchi na wale wakandarasi wameshamaliza lakini wanasubiri certificate ili waweze kulipwa. Je, ni lini Serikali itawalipa fedha zao ili miradi ya maji ikamilike?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, malipo yote ambayo wakandarasi wamefanya kazi na kazi zinaonekana malipo yote yanaendelea kushughulikiwa na hivi karibuni Serikali itawalipa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha sana nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo hapa mezani, tutaanza na wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Kwanza ni wageni watatu wa kwangu mimi kutoka Jiji la Mbeya, yupo Sheikh Ibrahim Bombo, ndugu Augenia Ndelwa na Ndugu Jamila Dagan. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni 86 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni wasanii mbalimbali maarufu nchini wakiongozwa na Katibu Mkuu na Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Hassan Abassi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 25 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni walimbwende wa shindano la ulimbwende lijulikanalo kama *Miss Jungle* Tanzania wakiongozwa na Afisa Utamaduni wa Jiji la Arusha ndugu Elizabeth Ncheya. Haya karibuni sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mmewaona hapo wasanii wetu, mmeona walimbwende, nadhani mtapata fursa ya kupiga nao picha hapo nje. Mkumbuke tu jana

Mheshimiwa Spika alitoa tangazo ambalo lilikuwa linatoka kwa Mheshimiwa Waziri Innocent Bashungwa kuhusu jambo ambalo hawa watu wamekuja kufanya hapa Dodoma. Naamini sisi kama Wabunge tutawapa ushirikiano wa kutosha kabisa leo watakuwa pale *Royal Village* wasanii wote, walimbwende watakuwepo pia lakini wasanii wetu watatuongoza na pia siku ya kesho tayari kwa ajili ya Serengeti *Festival*, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mkumbuke tangazo alilositiza sana Mheshimiwa Spika na hawa wote waliokuja ni wapiga kura wenu na wanawatarajia muwaunge mkono. *(Makofi)*

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni Maafisa kutoka *TANAPA* Mkoa wa Arusha wakiongozwa na ndugu Pascal Shelutete. Karibuni sana mnafanya kazi nzuri *TANAPA*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni 12 wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni wanafunzi wa *UDOM* wanaotokea Jimbo la Liwale wakiongozwa na ndugu Emanuel Mwangoka. Karibuni sana nadhani mmemuona Mbunge wenu alipokaa, yupo humu ndani ametulia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na huyu ni mgeni mmoja kutoka Jiji la Dar es Salaam anaitwa ndugu Dickson Elisha na yeye amekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi zake. Sijui amekaa upande gani ama hakupata fursa ya kuingia karibu sana. Wageni wetu tunawakaribisha sana.

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo lingine hapa; mnatangaziwa kuwa Watumishi wa Shirika la Hifadhi la Taifa *TANAPA* watakuwa kwenye viwanja vya Bunge kuanzia leo tarehe 5 Februari, hadi tarehe 12 Februari, 2021, kwa lengo la kufanya maonesho ya kuhamasisha utalii wa ndani kwa Waheshimiwa na Watumishi wa Ofisi ya Bunge. Pia shirika litaandaa na kuratibu safari za gharama nafuu za kutembelea Hifadhi za Taifa zilizo jirani na Jiji la Dodoma, ikiwemo Hifadhi ya Taifa Tarangire. Hivyo Waheshimiwa

Wabunge wote mnakaribishwa katika Banda la *TANAPA* katika viwanja vya Bunge ili kupata maelezo ya kina kuhusu utalii wa ndani katika hifadhi za Taifa pamoja na kufanya *booking* kwa watakaopenda kutembelea hifadhi.

Waheshimiwa Wabunge nadhani mmewaona viongozi wa *TANAPA* tumeshawatangaza hapa ndani na wao wapo kwa ajili ya zoezi hapo na sisi wenyewe kwenye majimbo vipo vivutio vya utalii, kwa hiyo ni muhimu kwenda pale na kama wao hawavifahamu, basi waambie ili waone namna ya kuhamasisha watalii wengine wanaokuja hapa nchini waje huko kwenye majimbo yetu. Pia sisi wenyewe tuoneshe mfano mzuri wa kuhamasisha utalii wa ndani, twende tukatembelee mbuga zetu na hawa wenzetu wamejiongeza kwa kuja kwa wawakilishi ili sisi tuweze kupeleka ujumbe huo kwa wananchi wote ambao tunatamani waende kutembelea hifadhi zetu na pia vivutio vyetu ili wafahamu nchi yetu imebarikiwa kiasi gani. Hapa kuna watu wengine wanatoka hapa kwenda nchi zingine halafu wanakwenda kwenye mbuga za wanyama huko wakati hapa sisi tunazo nyingi kabisa. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa wazo hilo na sisi Wabunge tutawaunga mkono.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho, linatoka kwa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambaye ni Katibu wa Wabunge wa CCM anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi na wale ambao sio wanachama wa Chama Cha Mapinduzi lakini wangependa kukiunga mkono Chama Cha Mapinduzi katika sherehe yake ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi miaka 44 iliyopita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba sehemu ile ya mzambarauni ukitokea geti la Waziri Mkuu saa nane kamili mchana shughuli hii ndio itakuwa sehemu hiyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi na Wabunge wa Mkoa wa Dodoma wanatarajiwa kutokukosa hapo wanahimizwa sana kuwepo. Kwa hiyo, mnaalikwa Wabunge wote kwenye hilo zoezi siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo hayo tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Katibu subiri kidogo kuna mwongozo Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nasimama kwa kutumia kanuni namba 53(1) ambapo inazungumzia Waziri ambaye hakujibu swali langu kwa usahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la msingi lilikuwa lini wakulima wa Tangawizi watalipwa hela zao. Swali hili lilitokana na Kamati iliyoundwa na Waziri Mheshimiwa Jafo ambalo lilisimamiwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, kwenda kuchunguza matatizo ya wakulima kuhusu kudhulumiwa hela zao. Ripoti ile ilionesha wazi kwamba wakulima hawa waliibiwa fedha zao kiudanganyifu. Ni ripoti ambayo iko *very comprehensive* ya 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa majibu ambayo ofisi ya Waziri wa Viwanda anatoa yanakinzana na ripoti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, niombe kiti chako kiwaagize Mawaziri hao wawili, Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Viwanda wakae wapitie ile ripoti ambayo ni *more recently* waone kwamba swali hili langu lilijibiwa sahihi au sio sahihi na kama sio sahihi lijibiwe kwa usahihi. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka akiomba Mwongozo wa Kiti hapa kuhusu swali lake namba 48 na majibu ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Naamini kwamba vishikwambi vyenu mnalo swali hilo, majibu yaliyotolewa hapa Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka anasema swali lake halijajibiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naghenjwa ni maswali ya nyongeza au swali la msingi ndiyo ambalo halijajibiwa kikamilifu?

MHE. NGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la msingi.

NAIBU SPIKA. Majibu ninayo hapa lakini kwa hiki alichokiomba na kwamba majibu hayafanani na swali lililokuwa limeulizwa, nitatoa Mwongozo wangu hapo baadaye baada ya kupitia yale maswali ya nyongeza yaliyolizwa na majibu yaliyotolewa na hili swali la msingi halafu nione namna ya kutoa hicho ambacho amekiomba kwa sababu ameomba Mawaziri wawili wakakae. Ukiomba Mwongozo maana yake kuna jambo ambalo limefanyika kinyume na utaratibu ulioko hapa ndani au kinyume na kanuni ambazo tumejiwekea. Kwa hiyo, lazima niangalie hiyo sehemu kwanza halafu sehemu ya pili itafuata. Nitatoa Mwongozo wa jambo hili baadaye leo. Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**HOTUBA YA MHESHIMIWA RAIS DKT. JOHN POMBE JOSEPH
MAGUFULI ALIYOITOA WAKATI WA UFUNGUZI WA BUNGE LA
KUMI NA MBILI TAREHE 13 NOVEMBA, 2020**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na hapa nimeshaletewa majina ya Waheshimiwa Wabunge kutoka kwa viongozi wao wa Vyama ambavyo vinawakilisha hapa ndani. Tutaanza na Mheshimiwa Judith Kapinga atafuatia na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mheshimiwa Self Khamis Gulamali ajiandae.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu

Mwenye Rehema, kwa kutujalia wote kuweza kuwepo hapa siku ya leo. Kipekee na kwa dhati ya moyo wangu...

NAIBU SPIKA: Samahani Mheshimiwa Mbunge kidogo. Waheshimiwa dakika ni tano na kengele itagongwa moja. Karibu Mheshimiwa Judith Kapinga.

MHE. JUDITH KAPINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kama nilivyotangulia kusema, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwenye Rehema kwa kutujalia kuwepo hapa siku ya leo. Kipekee na kwa dhati ya moyo wangu, napenda kumshukuru Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli kwa maono makubwa aliyonayo kwa taifa letu la Tanzania. Namwombea afya zaidi, nguvu zaidi na hekima zaidi ili aweze kutuongoza katika utekelezaji wa maono haya kwa kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli imeeleza nia ya dhati ya Serikali kuboresha mfumo wa elimu ili kuleta tija kwa wahitimu. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa unaoendelea katika sekta ya elimu, mfumo wetu wa elimu bado unalalamikiwa sana. Sababu kuu ni moja, bado haujaweza kumzalia matunda kijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia taifa letu lina vijana wengi wenye talanta ambao iwapo mfumo wa elimu ungeboreshwa na kuzingatia teknolojia wangeweza kujiajiri, kuajiri vijana wengine lakini pia wangeweza kuchangia kikamilifu katika pato la taifa. Ndiyo maana leo napenda nijielekeze kuchangia ni kwa namna gani mfumo wa elimu unaweza kuboreshwa na kuzingatia teknolojia ili tuweze kufikia ajira milioni 8 ambazo tumeahidi katika Ilani yetu ya Chama Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tulipokaa hapa ukiangalia ulimwengu matajiri kumi wakubwa duniani saba kati yao wamepata utajiri aidha kwa njia ya mtandao (*internet*) ama kwa njia teknolojia bandia, sidhani kama ni Kiswahili sahihi ila wenzetu Wazungu wanasema *artificial*

intelligence ama kupitia TEHAMA. Nikitoa mifano michache, ukimwanguka Jeff Bezos tajiri wa kwanza duniani amepata utajiri wake kupitia mtandao wa Amazon wa kununua na kuuza bidhaa anaingiza bilioni 127 kwa saa moja na amejiri watu si chini ya laki moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia na matajiri wengine ambao ni wadogo, Mark Zuckerberg tajiri mdogo kuliko wote duniani amejiri watu 52,000 anaingiza mamilioni ya shilingi kupitia mitandao ya jamii tunayoitumia hapa kama *WhatsApp*, *Facebook* na *Instagram*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia matajiri wengine wadogo kabisa Larry Page, Sergey Brin wote wanaingiza mamilioni ya shilingi kwa saa moja na wameajiri siyo chini ya watu 135,000. Siwezi kuwaelezea wote lakini taswira hii inatuambia teknolojia ndiyo mwarobaini wa changamoto za ajira za vijana wa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai kwa Serikali ya chama changu kuweza kuangalia upya mifumo yetu ya elimu ili kuboresha masomo ya sayansi. Ubunifu unaanzia kwenye kujua ABCs za *computer*. Lazima tuboreshe masomo yetu ya sayansi yazingatie mafunzo ya *computer* kuanzia elimu ya msingi kwa sababu huko ndiko ubunifu unakoanzia na siyo kusubiria kuwafundisha watoto vyo vikuu wakati vichwa vyao tayari vimekomaa. Matajiri wote hawa walipata mafanikio kwa sababu mifumo ya elimu iliwaandaa, iliwakua kiubunifu na iliwasaidia na ndiyo maana wengi wao walivyofika chuo kikuu waliweza kubuni program hizi ambazo zinatatua changamoto za dunia za teknolojia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia leo vijana wetu wanaomaliza *form four* na *form six* mfumo wa elimu umewasaidia vipi? Mfumo wa elimu unapaswa kumsaidia kijana kwa ujuzi wa kujitegemea kwa ngazi yoyote anayoishia. Kinachosikitisha zaidi vijana wetu wa chuo Kikuu...

(Hapa kengele *illia* kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JUDITH KAPINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mheshimiwa Salum Mohamed Shafi ajjandae.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai. Nishukuru sana wana Maswa kwa kunichagua kwa kura nyingi sana, nimepata ushindi mkubwa kuanzia kwa Rais, Ubunge hadi kwa Madiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niendeleo kutoa pongezi sana kwa Mheshimiwa wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa aliyofanya hasa kukusanya maduhuli na kuhakikisha kwamba matumizi ya fedha inayokusanywa na Serikali inafanya kazi iliyotakiwa. Kwa kweli usimamizi umekuwa ni mzuri sana kwa Serikali na matokeo tunayaona kwamba fedha inayokusanywa na Serikali inatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita kwenye jambo moja muhimu. Mheshimiwa Rais wakati anatoa hotuba alisema kwamba jambo ambalo atalipa kipaumbele au Serikali italipa kipaumbele ni kulinda na kudumisha tunu ya taifa letu yaani amani, umoja na mshikamano wa uhuru wa nchi yetu. Nazungumza hili kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna janga kubwa la *corona* ambalo limeitikisa dunia. Naomba nikuambie kitu kinachompeleka mtu hospitali siku zote, nazungumza hili ili watu waweze kunielewa, cha kwanza huwa ni maumivu (*pain*). Jambo la pili linalompeleka mtu hospitali huwa ni hofu. Hofu ziko mbili; ya kwanza hofu ya *disability* yaani kupata ulemavu na hofu ya pili huwa ni ya kifo. Haya ni mambo

makubwa yanayompeleka mwanadamu hospitali kwenda kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetengenezwa hofu na hofu hii ni ya kifo, dunia imetengenezwa hofu ya gonjwa la corona, taarifa zimekuwa *exaggerated as if*kwamba corona ni gonjwa jipya litakwenda kuangamiza dunia hii. Ni mwamba mmoja tu Dkt. John Pombe Magufuli amesimama imara na kupingana na hofu hii. Naomba Watanzania na Waheshimiwa Wabunge tuungane na juhudi za Mheshimiwa Rais wetu kuondoa hofu hii ambapo ni janga kubwa linakwenda kuleta vifo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa yalikuwepo mengi, kuna ugonjwa ulikuwa unaitwa *smallpox* (ndui), ulikuwa *eradicated* mwaka 1977 kwa chanjo na ulikuwa unasababishwa na *virus*. Kuna ugonjwa mwingine wa surua uliwa watoto wengi, ulipatiwa chanjo na sasa hivi umekuwa *controlled*. Kuna tatizo kubwa la malaria, tunapata *infection* ya malaria milioni 200 kila mwaka, hawa watu wangekuwa wanatupenda ugonjwa wa malaria wangeukomesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya nyuma, kuna Profesa mmoja Mjerumani alileta *genes* ambapo angeweza kuwasambaza kwa mbu wote na wangebadilisha *behavior* ya kutafuta damu kwa kwa ajili ya ku-*nourish* mayai yao kutoka kwa binadamu kwenda kwa wanyama na mbu hao wasingesababisha malaria ingekuwa historia kama walivyofanya kwenye *chickenpox* au *smallpox*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ugonjwa wa *HIV* umeanza toka mwaka 1981 na wanamjua huyu *retrovirus* yupo *type one* na *type two*, wanajua *behavior* yao, biashara ipo kwenye *antiretroviral*, hapo ndipo wanapokunywa maziwa. Wameanza na vidoge vingi kwa wagonjwa wameenda kwenye kidonge kimoja na sasa hivi wanakwenda kwenye *innovation* ya sindano moja kwa miezi sita. Biashara hii inaenda kwisha kwa sababu muamko umeeleweka, vifo vimepungua kwa asilimia 60 na

maambukizi yamepungua kwa zaidi ya asilimia 40 na Tanzania tumepambana nayo vizuri sasa *deal* imeisha kwenye *HIV, the deal now is corona. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna ugonjwa huu wa *corona* umetambulika China *type* ya kwanza na *type* ya pili ambayo wanasema imetokea South Africa wanakuja na chanjo wanasema hii ndiyo chanjo ambayo inakwenda ku-*solve corona*, chanjo ya *HIV* ya toka mwaka 1981 iko wapi? Kwenye malaria nimedokeza biashara ipo kwenye vimelea vya malaria, neti, antimalaria na ugonjwa huu ni biashara kwao na ndiyo maana wanaendelea kuufuga. Kuna Waitaliano wameleta *genes* wanasambaza, mbu wamembadilisha anakuwa na jinsia mbili; anakuwa hana mdomo wa kunyonya damu, badala ya kumng'ata binadamu anakwenda kufa kwa sababu hawezi kumng'ata binadamu na *spread* ya malaria inaisha. Aliyegundua hizi *genes* alikufa mazingira ya kutatanisha kisa biashara ya *antimalaria* na neti na wanaotutengenezea net bure tunawajua. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kengele imeshagonga.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Seif Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi, Mheshimiwa Humphrey Polepole ajiandae.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii adhimu kuweza kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Bungeni mwaka 2020 lakini na ile ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Manonga kwa kunipa kura nyingi lakini

pia kumpa kura nyingi Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na kwa kukichagua Chama cha Mapinduzi. Kama unavyotambua leo ni tarehe 5 Februari, Chama cha Mapinduzi, chama adimu, chama kikongwe Barani Afrika na duniani kinakwenda kutimiza miaka 44 toka kuzaliwa kwake. Chama hiki kina heshima kubwa sana siyo tu ndani ya nchi bali na Afrika kwa ujumla. Ni chama ambacho kinajihuisa kila baada ya miaka mitano na tunatarajia mwakani kitajihuisa tena. Kwa hiyo, ni chama pendwa na kinafanya kazi ambayo Watanzania wanakitarajia na wanakitegemea kwa asilimia kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo na kukitakia *happy birthday* Chama cha Mapinduzi, nijielekeze kwenye hoja ya msingi. Kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa hotuba zenye maono na mwelekeo wa nchi yetu tunataka kwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya mwaka 2015 alionyesha upingaji mkubwa wa ufisadi, rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. Alizungumzia pia masuala ya kufufua Shirika letu la Ndege, ujenzi wa reli na mambo mbalimbali. Leo tumeshuhudia ufufuaji wa Shirika letu la Ndege, tuna zaidi ya ndege 8, ujenzi wa reli ya kisasa ya umeme ambayo itakuwa bora katika Afrika Mashariki na Kati, lakini pia ujenzi wa Bwawa kubwa la Stiegler's lenye uwezo wa kuzalisha umeme zaidi ya *megawatt* 2,115.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake amezungumzia kutengeneza ajira zaidi ya milioni 8. Naomba kuchangia kwenye ajira na niwaombe watu wa Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Elimu na Wizara ya Ajira waungane kama timu moja kutengeneza ajira za vijana wetu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizi ajira milioni 8 niwaombe watengeneze ajira milioni 1 nje ya Tanzania. Watengeneze fursa za Watanzania kufanya kazi nje ya nchi yetu. Yapo mambo ambayo tunaweza tukanufaika nayo kupitia ajira hizi ambazo Wizara itazitengeneza. Kupitia Balozi

zetu ambazo zipo nje wanaweza kutengeneza mfumo ambao ukawatengenezea vijana wa Kitanzania waliomaliza vyuo vikuu wakapata kazi *formal* na *informal* katika katika nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira inaleta ukuaji wa uchumi katika nchi. Mfano nchi kama Philippine wananchi wake zaidi ya milioni 12 wanafanya kazi nje ya nchi na wanapata faida kubwa sana. Mfano tukitengeneza ajira milioni moja wakachangia kila mwezi ndani ya nchi yetu dola mia moja tu wakarudisha kuwapa wazazi wao, tutatengeneza dola milioni 100 zitakazolingia kila mwezi ndani ya nchi yetu. Dola milioni 100 kwa mwezi uki-*multiply* by miezi kumi na mbili tutapata zaidi ya dola bilioni 1.2, hili ni soko ambalo tunatakiwa tulitumie.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapi tunaweza tukaanzia? Sisi tuna Kiswahili, hii ni bidhaa adimu ambapo nchi nyingine hawana na kama wanayo lakini si kwa undani wake. Tutumie nafasi hii kukitangaza Kiswahili, tufanye *lobbying* katika nchi kama *South Africa* ambao wanataka kuanzisha kufundisha Kiswahili katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Nje iongee na *South Africa* tupeleke vijana wetu wakafanye kazi kule, tupeleke vijana wetu Namibia, Zimbabwe, hata kama tukitoa *offer* katika vijina 100, 20 tutawalipa sisi itaweza kutengeneza ajira kwa vijana wetu. Badala ya kuzagaa mitaani wataweza kupata fursa ya kufundisha Kiswahili ndani ya Afrika lakini pia hata Marekani ikiwezekana kwa sababu viko vyuo vikuu Marekani wanafundisha Kiswahili badala ya kuliacha suala hili liwe la mtu mmoja mmoja ambapo walimu wanajitafutia ajira wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika sekta ya afya tuna uwezo wa kutengeneza ajira za madaktari wetu. Inawezekana tukawa na uchumi mdogo wa kuajiri wanafunzi wote lakini tunaweza kutengeneza ajira za vijana wetu katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu siyo rafiki sana, napenda kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi, atafuatiwa Mheshimiwa Humphrey Polepole, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo ajiandae.

MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia leo kuwepo katika Bunge hili Tukufu. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru wale wote waliosababisha kwa namna moja ama nyingine nami kuwa Mbunge wa kuchaguliwa Pemba. Nawashukuru sana wananchi wangu wa Chonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais. Miongoni mwa mambo aliyoyajadili Mheshimiwa Rais ni suala zima la kudumisha Muungano. Muungano huu umeunganisha nchi mbili; ulikuwa ni Muungano uliunganisha Tanzania Bara na Tanzania Visiwani Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wanzanzibar, sisi Watanzania tunahitaji Muungano wa haki, usawa na wa kuheshimiana. Naomba ifahamike sisi Zanzibar tunayo Mahakama Kuu ambayo ina mamlaka ya kusikiliza kesi zinazohusu masuala ya Zanzibar. Nilikuwa najiuliza maswali na kupata ukakasi mkubwa sana iweje leo kesi inayopaswa kusikilizwa Zanzibar ihamishiwe Tanzania Bara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi tuna kesi kadhaa, natolea mfano kesi ya uamsho. Hili dai liko mahakamani linaendelea, sipendi kuingilia Mhimili wa Mahakama, lakini najiuliza sasa ni takribani miaka nane, kesi hii bado iko kwenye upelelezi, bado hajjakamilika ushahidi wake. Je, hakukuwa na mamlaka kwa Mahakama Kuu ya Zanzibar kusikiliza kesi hii mpaka iletwe Tanzania Bara? Hebu tunaomba Serikali mtuambie nini shida watu hawa hadi leo; tunahitaji tuwatendee haki Wanzanzibari wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumwomba Rais huyu, Rais msikivu, Rais mtetea wanyonge, Rais anayesema aombewe, nimwombe Mheshimiwa Rais; kama walivyoachiwa wale Waethiopia na hawa Wazanzibari na wao tuwaachie. Kama walivyoachiwa Waethiopia wale, Wazanzibari hawa na wao Mheshimiwa Rais awahurumie, atumie nafasi yake ya Urais kuhakikisha Wazanzibari hawa na wao tunawatendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende katika suala la mchakato wa Katiba Mpya, ni sehemu ambayo Mheshimiwa Rais aligusia. Katiba hii tutakapoipata tutatatua changamoto na matatizo mbalimbali yanayotuhusu Wazanzibari na yanayotuhusu Watanzania.

Leo najjuliza, iweje *referee* anachezesha ndani ya uwanja halafu yeye huyo huyo anakuwa ndiye mchezaji wa mpira, anakuwa ndio muamuzi; kweli tutakuwa tuna Tume huru? Tunahitaji Tume huru ili tuwaaminishe Watanzania chaguzi hizi zinavyofanywa ni uchaguzi huru na haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu leo sote kila mmoja anafahamu ni namna gani alivyoingia humu. Sote tunajuana humu; waliongia kushoto wanajua, waliongia kulia wanajua, kila mmoja na siri yake. Uchaguzi ulikuwa ni uchaguzi wa shida, ulikuwa ni uchaguzi mtihani. Leo humu wengine ukiwauliza, aah kwani bado mimi ni Mbunge? Ni mtihani mtupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme Taifa hili tunasema tuliombe, hatuwezi Mungu akatupa mafanikio makubwa kama dhuluma inatawala ndani ya nchi hii. Dhuluma ni adui wa haki. Tutakuwa tunadhulumu lakini mafanikio hatuyapati.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, Kanuni.

MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI: Naomba niendeleo kusema. *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa uliyekuwa unataka kutoa taarifa uniwie radhi, sikuona uko upande gani, kwa hiyo kengele imeshagonga.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Humphrey Polepole, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza ajiandae.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza namshukuru sana Mungu wa Mbinguni kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kunipa heshima ya kuwa sehemu ya Bunge hili tukufu, nami nawaahidi Watanzania lakini pia Bunge hili kuendelea kuchapa kazi ili tuweze kufikia malengo ya Watanzania kama ambavyo wanatarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba aliyoitoe Mheshimiwa Rais katika Bunge hili la Kumi na Mbili lakini nikirejea hotuba aliyoitoe katika Bunge la Kumi na Moja na nitajielekeza katika mambo matatu. La kwanza ni kuhusu viwanda vidogovidogo, vya kati na vikubwa. Mheshimiwa Rais ameeleza katika hotuba yake umuhimu wa viwanda na mchango wake mkubwa katika kutengeneza ajira zaidi hapa Tanzania na tukitazamia ajira milioni nane ambazo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi inalenga kuzitengeneza katika miaka hii mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali; tukiunganisha viwanda vidogo vidogo na vya kati na Sekta ya Kilimo kuna faida kubwa sana na tutaweza kuona tija ya

viwanda hivyo. Natoa mfano mmoja; mahitaji yetu ya mafuta ya kula hapa Tanzania sasa hivi ni wastani wa tani laki tano na uzalishaji wetu wa ndani wa mafuta ya kula ni wastani wa tani laki mbili na nusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ikifanyia kazi yenyewe na kwa kushirikiana na Sekta Binafsi pale inapowezekana na pale isipowezekana Serikali yenyewe ichukue dhamana hii kushirikiana na wananchi kutengeneza viwanda vidogo vidogo na vya kati katika maeneo wanapolima alizeti na mawese, ili wakulima ambao wamekosa fursa ya kuuza mazao haya ya alizeti na mawese kwa muda mrefu wawe na soko la uhakika kwa sababu kuna viwanda vya kuchakata alizeti na mawese na kutengeneza mafuta na hatimaye mafuta haya yatapata soko kwa sababu mpaka sasa hivi tuna nakisi ya mafuta ya kula wastani wa tani laki tatu. Maana yake wakulima watapata fedha yao, viwanda hivi vilivyowekeza na Serikali vitarejesha fedha yake na kujijendesha kwa faida, lakini pia walaji watapata mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu; ingependeza sana baada ya kuwa tumefikia kiwango kikubwa cha kuzalisha mafuta nchini, kama zilivyo nchi zingine ambazo zina sera za kulinda masoko ya ndani, (*protectionist policies*), tuseme marufuku sasa kuagiza mafuta kutoka nje kwa sababu tunazalisha hapa hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni kuhusu uvuvi; Mheshimiwa Rais ameeleza vizuri sana kuhusu uvuvi wa bahari kuu na katika maziwa yetu makuu ikiwemo ununuzi wa meli, vifaa vya kufanyia uvuvi wa kisasa na kadhalika. Rai yangu kwa Serikali; tulitazame sana Ziwa Victoria na tufanye uvuvi wa kisasa wa vizimba (*aquaculture fish farming*). Serikali kupitia halmashauri zetu zishauriwe wawekeze kwenye uvuvi wa vizimba (*aquaculture fish farming*), ni uvuvi wenye faida kubwa na tija kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mahitaji yetu ya sato hapa nchini bado ni pungufu. Tukiwekeza katika Ziwa

Victoria kwa vizimba na tukafuga samaki sato wengi zaidi si tu tutaongeza mapato ya wale ambao wamewekeza wakiwepo watu wa halmashauri, tutaongeza lishe kwa watu wetu wa Tanzania lakini pia tutaauza nje sato hao kwa sababu hata katika eneo la maziwa makuu, bado uwekezaji katika ufugaji wa samaki kupitia vizimba haujafanyika vizuri sana. Kwa hiyo tutaongeza pia fedha za kigeni kwa maana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni ufugaji. Hapa niseme tu kwa ufupi kwamba kazi nzuri imefanyika. Sisi tunaongoza kwa kuwa na ng'ombe wengi Afrika na hili limeelezwa vizuri sana katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Rai yangu mimi, kitu kimoja hatujafanya vizuri; ufugaji wa sasa ni wa kuhamahama, unafanya tija ya ng'ombe ishuke. Kama tukiwekeza kwenye mashamba ya kulima majani, chakula cha ng'ombe (*hay*) ambapo sasa hivi kwa utafiti niliyofanya kuna mashamba mawili tu, nafikiri moja liko kule Mbeya. Kama tukilima *hay* tukawapatia wakulima, ng'ombe wao hawatahitaji kutembea kila mahali na kuleta migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Hata hivyo, *hay* ikilimwa vizuri hapa Tanzania tukaweka mashamba mengi zaidi ya *hay*, *hay* ni fursa kubwa na uwekezaji huu utaweza kutuwezesha sisi kuuza *hay* kwenda nje ya nchi kwa sababu ni zao ambalo linahitajika sana, si tu hapa Tanzania lakini nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo matatu nigusie moja ambalo limesemwa na wengi, lakini nami niongezee tu kwa uzito. Mwaka 2000 kiongozi wa *UAE*, *Al-Maktoum* alifanya uamuzi wa kununua ndege 59 za Shirika la *Emirates*. Mwaka kati ya 2000...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mchango wangu nitauwasilisha kwa maandishi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, atafuatiwa na

Mheshimiwa Agnеста Lambert Kaiza na Mheshimiwa Sylvia Sigula ajiandae.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa ridhaa yako kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia kukishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kunipa ridhaa ya kupeperusha bendera katika Jimbo la Newala Vijijini. Pia nipongeze na kuishukuru familia yangu kwa *support* wakati wote wa uchaguzi hadi sasa. Kipekee pia niwashukuru wapigakura wa Jimbo la Newala Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja na hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa Novemba, 2020 pamoja na ile ya 2015. Ni hotuba ambazo nimepitia zote, hotuba ambazo zina maono, hotuba ambazo kwa namna ya kipekee, hasa ile ya 2015, ilipotekelezwa pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ilikifanya Chama Cha Mapinduzi kutembea kifua mbele wakati wa Uchaguzi wa Mwaka 2020. Nina imani hotuba hii ambayo ameitoa 2020 tukiitekeleza hivi inavyotakiwa 2025 itakuwa ni kuteleza kama kwenye ganda la ndizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amefanya mambo mengi, tumeyaona. Amesimamia vizuri miundombinu katika nchi hii kuanzia afya, barabara, elimu na sekta nyingine zote. Tunampongeza sana kwa kile ambacho amekifanya kwa kusaidiana na wasaidizi wake ambao ni Mawaziri wetu. Hata hivyo, zipo changamoto kadhaa ambazo zikisimamiwa na kutekelezwa ipasavyo nadhani nchi hii itasonga mbele sana zaidi ya hapa ambapo tupo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Mtwara wanazalisha kwa kiasi kikubwa zao la korosho, zao ambalo linaipatia nchi hii uchumi na fedha nyingi za kigeni, lakini kuna changamoto ya barabara yetu ya kiuchumi, barabara ambayo inatumika kupitisha zao la korosho kutoka kwenye maeneo ya wakulima kuelekea bandarini. Barabara ile imeshaombewa muda mrefu lakini haikamiliki. Ni barabara

ya kutoka Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala – Masasi hadi Nachingwea. Barabara ile hadi sasa imekamilishwa kwa kiwango cha lami kwa kilometa 50 tu. Niombe wenzetu wa Ujenzi kuharakisha ukamilishaji wa barabara ile ili mazao ya wakulima yapate kusafirishwa kwa urahisi kuelekea bandarini, lakini pia kuvinusuru vyombo ambavyo vinasafirisha mazao hayo kuelekea bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Newala ambayo ipo Jimbo la Newala Vijijini imehamia mwaka jana katika eneo lake jipya la utawala. Eneo lile halina jengo la utawala na kwenye hotuba tumeelezwa na kusisitizwa suala la utawala bora. Utawala Bora ni pamoja na kuwepo na maeneo ya watumishi kutendea kazi, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Newala haina jengo la Utawala. Niombe wahusika na wasimamizi wa masuala ya utawala kwa maana ya TAMISEMI watuangularie kwa jicho la pekee ili watumishi wale wapatiwe jengo la utawala nao wafanye kazi katika mazingira yaliyoboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Newala Vijijini kuna changamoto ya maeneo ya kutolea huduma ya afya. Zipo kata 22 lakini ni kata tatu tu ndizo ambazo zina vituo vya afya. Naomba Mheshimiwa anayesimamia afya atuangalie kwa jicho la kipekee tupate vituo vya afya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Agneta Lambert Kaiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvia Sigula na Mheshimiwa Shangazi ajiandae.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa nafasi hii adimu ambayo umenipatia ili niweze kusema machache kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuchangia nitumie fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima, lakini pia kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili niweze kujadili masuala mazima yanayohusiana na hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo mengi ambayo Mheshimiwa Rais alizungumza katika hotuba yake ni pamoja na nchi yetu kuingia katika uchumi wa kipato cha kati. Hii ni habari njema kwa Taifa na ni jambo la kujisifia kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa ni kweli Serikali yetu imetuingiza katika uchumi wa kipato cha kati, kuna mambo ya msingi sana ambayo yanapaswa au yalipaswa ku-*reflect* moja kwa moja kwamba sasa Tanzania tumeingia katika uchumi wa kipato cha kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mbele ya Bunge lako tukufu nijikite katika masuala makuu manne ambayo yanaashiria moja kwa moja kwamba ni ama tumedanganywa kama nchi kwamba tumeingia katika uchumi wa kipato cha kati au Serikali imedanganya kwamba sasa hivi imekuwa ikikusanya mapato makubwa sana ambacho ni kiashiria cha ukuaji wa uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, wewe ni shahidi kwamba Serikali imekopa pesa nyingi kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mfano *NSSF*; Serikali imechukua, au imekopa fedha ambazo Serikali ilitarajiwa irudishe ile mikopo ndani ya ule muda ambao masharti yanasema ili mwisho wa siku sasa wastaafu, mama zetu, mashangazi zetu, wajomba zetu ambao walitumikia nchi hii kwa uaminifu mkubwa sana na baadaye wakastaafu sasa waweze kupewa...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kaiza, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza. Anataka kujenga hoja kwamba Serikali bado haijalipa fedha ambazo ilikuwa inadaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilipe taarifa Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeshafanya kazi hiyo na mpaka sasa zaidi ya trilioni 1.2 ambazo Mfuko wa *PSSSF* ulikuwa unaidai Serikali, fedha hizo zimekwisha kurudishwa na Mheshimiwa Mbunge ni shahidi wakati tulipokuwa kwenye kikao cha Kamati, mimi mwenyewe na watendaji wa Mfuko tulishatoa taarifa hiyo kwenye Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mengine ambayo Serikali bado inaendelea kufanya uhakiki. Utaratibu wa Serikali sasa hivi katika madeni yaliyobakia haiwezi kulipa bila kufanya uhakiki, kwa hiyo kila baada ya uhakiki Serikali imeendelea kuwa inalipa madeni hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, labda nitakapokuja jioni ama wakati wa kuchangia Mpango tutatoa taarifa ya wastaafu wangapi wamekwishalipwa mafao yao na kwa nini labda kumekuwa na kuendelea kuwalipa wastaafu mafao kwa utaratibu mmoja na mwingine. Kwa hiyo maeneo haya tutayatolea maelezo lakini *justification* ya malipo ya Serikali tunayo na Serikali imelipa na tunaendelea kuhakiki na tunaendelea kulipa yale yaliyokwisha kuhakikiwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agneta Lambert Kaiza, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikiri kwamba mama yangu, dada yangu, rafiki yangu mpenzi, anafanya kazi nzuri sana, lakini itoshe kusema kwamba hayo aliyoyasema kwamba Serikali haijalipa ndiyo hayo ambayo nayaongelea mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasema tayari imetuingiza kwenye kipato cha kati. Kama tumeingia kwenye kipato cha kati na tayari kuna wastaafu ambao waliitumikia nchi hii kwa uaminifu mkubwa sana hawajalipwa, itoshe kusema kuna tatizo. Sasa nimshauri dada yangu na rafiki yangu achukue ushauri wangu huu, kwamba pamoja na kazi nzuri anayoifanya, hili linaitia doa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja katika ajenda yangu ya pili inayohusiana na Serikali kuchelewesha malipo kwa makandarasi. Ikiwa kweli Serikali hii imetuingiza katika kipato hiki cha kati, ilipaswa moja kwa moja kitu cha kwanza kabisa iwe inalipa *on time* fedha za makandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe umesikia jana, leo, juzi, wachangiaji wengi katika Bunge hili wamekuwa wakilalamika kuhusiana na ujenzi wa barabara. Kwa hiyo, unaposikia kuwa...

T A A R I F A

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kaiza, kuna taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, hii itakuwa taarifa ya mwisho kwa sababu muda wetu ni mfupi. Mheshimiwa Charles Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimweleweshe msemaji kwamba hivyo vitu anavyovizungumza haviendani na hoja anayotaka kutoa ya

kusema kwamba tuko kwenye kipato cha kati. Kipato cha kati hakiendani na mambo ya Serikali kukopa au Serikali kutokulipa, hayo ni mambo tofauti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vinavyotumika ni wastani wa pato la mtu mmoja. Unachukua pato la Taifa unaligawanya kwa idadi ya watu, unapata huo wastani. Kwa hiyo, hiyo haihusiani na mambo ya Serikali kutokulipa au kufanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwelekeza kwamba hilo analozungumza ana hoja nyingine pengine lakini siyo hiyo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kaiza, unaipokea taarifa hiyo?

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza taarifa hiyo siipokei, lakini nakuomba wewe na Kiti chako unilindie muda wangu wa dakika tano vizuri sana, nakuomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anadai kwamba ninachokiongelea hapa siyo sehemu ya hiyo dhana nzima ambayo nimetoka kuisema. Hata hivyo, ikiwa pato la Taifa hali-reflect maisha ya wananchi ya kila siku, tusijidanganye kwamba tumeingia katika uchumi wa kati. Mfano, makandarasi wanashindwa kwenda kulipa fedha kwenye...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kaiza, nilikupa sekunde 30 kwa sababu kengele ilishagonga. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Sylvia Sigula, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Abbas Tarimba ajiandae.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuongea katika Bunge hili tukufu, nianze kwa kumshukuru Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuendelea kutupa kibali kuiona siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee sana, nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi kinachoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kutuamini vijana na kutupa uwakilishi katika Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nimepata bahati ya kuipitia hii Hotuba ya Mheshimiwa Rais zaidi ya mara tatu. Naomba nikiri katika Bunge hili Tukufu, kama kuna hotuba nilizowahi kuzisoma ambazo ni bora, hii ni hotuba nambari moja. Hotuba hii imebeba dira, maono, matarajio na matamanio makubwa sana ya vijana na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukianza ukurasa namba moja mpaka ukurasa wa 41, utaona kabisa Mheshimiwa Rais amegusia sekta zote na zote hizo anamlenga kijana. Unapozungumzia viwanda, unazungumzia wanufaika ambao ni vijana; unapozungumzia nishati, wanufaika wa kwanza ni vijana; unapozungumzia mikopo, wanufaika wa kwanza ni vijana. Kwa hiyo, wakati Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake anazungumzia utengenezaji wa ajira zaidi ya milioni nane, naona ni jambo ambalo linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijielekeze katika ukurasa wa 37 ambapo Mheshimiwa Rais ameelezea kukuza sekta ya sanaa, michezo na utamaduni. Ni wazi kabisa tunafahamu michezo ni ajira na ni kipato; katika kuelezea sekta hii Mheshimiwa Rais amesema kabisa kwamba ataanzisha mfuko ambao utawawezesha wasanii kimafunzo na mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hapa; kwanza naipongeza Serikali kwa kuanzisha Taasisi ya Sanaa

ambapo zamani kilikuwa ni Chuo cha Sanaa Bagamoyo. Taasisi hii inatoa kozi, lakini kozi zinazotolewa pale ni chache. Tukisema tuwezekeze katika sekta ya sanaa tutatengeneza ajira nyingi sana kwa vijana. Tunajua sanaa ipo kwa upana wake mkubwa lakini tunaona sanaa hizi zinawatoa vijana wengi na kuwatengenezea kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mdogo tu. Juzi tulitembelewa na vijana hapa, tunaweza tukawatengeneza vijana wa aina ile zaidi. Tunaweza tukawatengeneza akina Manula na Boko wengi kutoka kwa vijana wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa huu wa 37 naomba kunukuu. Rais anasema: "Tutahuisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kuwasaidia wasanii wetu ikiwemo kupata mafunzo na mikopo." Napenda nijikite hapa, kipengele hiki ni kikubwa sana na kama tutakifanyia kazi vizuri, basi tutatengeneza ajira nyingi kwa vijana. Kwa sababu sekta ya sanaa tukisema tuwekeze kwa nguvu kubwa, itaweza kuwainua vijana wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mdogo tu wa mkoani kwetu Kigoma. Tunaelewa kabisa Mkoa wa Kigoma ndiyo kitovu cha sanaa za hapa Tanzania. Ndiyo maana ukifanya tathmini ya wasanii wengi wa Tanzania utaona wengi wanatokea Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali, naiomba sana Wizara husika ione ni namna gani ya kuboresha na kuwekeza katika sekta hii ya sanaa. Sawa tumeanzisha Taasisi hiyo ya Sanaa lakini bado tuna vijana wengi wa Kitanzania wenye vipaji ambao wakipewa fursa wanaweza wakafanya vizuri. Changamoto katika sekta hii ya sanaa, vijana wengi hawana mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tuna chuo hicho kimoja lakini naiomba Serikali kama itawezekana tuweze kuongeza vyuo hivi hata kwa *level* ya kanda. Itakuwa rahisi kuwahudumia vijana wengi kwani watapata mafunzo pale,

lakini hii mikopo ambayo ameisema Mheshimiwa Rais ikawasaidie hawa vijana wajiendeleze. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda umeisha.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana lakini mada yangu nitaiwasilisha vizuri kwa sababu iko katika mapana yake. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Tarimba na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyoko mezani ambayo ni Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika vipindi viwili kwa maana ya wakati anafungua Bunge la 2015 na Bunge hili la sasa la 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita zaidi katika eneo la diplomasia ya uchumi. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, ametembea katika maono na dira ile ambayo ameizungumza katika hotuba zake mbili na kuonyesha umahiri na ujasiri mkubwa wa kusimamia kile ambacho anakielekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitano, 2015 - 2020 Tanzania imeweza kufungua Balozi nane ambazo zinafikisha Balozi takribani 43 duniani kote. Ongezeko hili la Balozi nane kwa kipindi kifupi cha miaka mitano inaonyesha dhamira ya wazi kabisa kwamba Mheshimiwa Rais anataka sasa aipeleke Tanzania huko duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake nini? Maana yake sasa ni kwamba Wizara za kisekta zinatakiwa zifanye

kazi mahsusi ili hizi Balozi ambazo tumezifungua zikawe fursa za kibiashara na fursa nyingine kutoka kwao kwa maana ya kutuletea teknolojia pamoja na mitaji. Kwa mfano, sasa hivi tumefungua Ubalozzi kule Havana, Cuba, tunajua wenzetu wale ni wajuzi sana wa kilimo hasa cha umwagiliaji. Kwa hiyo, tunatarajia kuiona Wizara ya Kilimo ikifungamanisha sasa uanzishwaji wa Ubalozzi Havana, Cuba pamoja na kusaidia sekta ya kilimo hapa nchini kwa maana ya kubadilishana utaalam na ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo hilo la diplomasia ya uchumi, Mheshimiwa Rais ameahidi kwamba tunanunua ndege ya mizigo kwa ajili ya kusafirisha mazao hasa ya mbogamboga na matunda. Hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba ni lazima sasa tujiandae kwamba hayo mazao tunayotaka yaende kwenye ulimwengu mwingine, tumeyaandaa kwa kiasi gani? Ndiyo hiyo hoja ambayo alikuwa anaizungumza Mheshimiwa Humphrey Polepole hapa kwamba ng'ombe wetu tutaendelea kuwaacha wazurure huko halafu baadaye tuseme kwamba wanaweza kwenda kushindana kwenye masoko mengine ya dunia? Ni lazima sasa Wizara zichukue hii kama changamoto ili ndege hii isije ikapaki *airport* haina shughuli za kufanya. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lugha ya Kiswahili. Sasa hivi lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha 10 zinazozungumzwa zaidi ulimwenguni. Hapa kuna haja ya dhati kabisa kwa Wizara ya Elimu kupitia mtaala upya. Tunataka kukipeleka Kiswahili katika nchi za Kusini za Afrika (*SADC*), nchi 16. Huwezi ukapeleka Kiswahili hiki ninachozungumza hapa kwenye nchi ambazo zilikuwa zinatawaliwa na Mreno. Maana yake ni kwamba ni lazima sasa tutengeneze mtaala mpya, tuandae wataalam mbalimbali wa kusoma lugha, wawe na ujuzi wa kujua Kireno, Kifaransa, Kiingereza, Kiarabu, Kichina na lugha nyingine zote ili watakapokwenda kuipeleka bidhaa ya Kiswahili katika hayo maeneo, basi kusiwe na shida ya kuwa na ukalimani. Kwa hiyo, nawafumbua macho Mawaziri kwamba ikishazungumzwa kwenye Hotuba ya Rais sisi turudi katika

sekta zetu kuchakata na kuweka hiyo mipango ili mambo haya yaweze kwenda vile ambavyo tunakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu biashara. Wizara ya Mambo ya Nje ina mpango wa kufungua Ubalozi Mdogo pale Lubumbash, hili ni eneo la kibiashara. Tumeona nchi yetu tunajitahidi sana katika uzalishaji, tunatakiwa tutumie fursa hii ya Balozi tunazozifungua na Balozi Ndogo kuhakikisha kwamba mazao ya Watanzania yanapata masoko. Siyo ya Watanzania tu na bidhaa zinazotoka nchi za wenzetu na zenyewe ziweze kuja hapa kwetu na kutunufaisha katika maeneo yote ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaposema diplomasia ya kiuchumi, hili ni jambo kubwa tunalotakiwa tulitazame kwa jicho la kimkakati. Balozi hizi nane ambazo zimeanzishwa, zote ukizipitia ni za kimkakati. Tukizungumza mahusiano yetu na Uturuki, ni eneo la kimkakati la kibiashara; tukizungumza na Algeria, ni eneo la kimkakati; tukiwaangalia Jamhuri ya Korea Kusini nalo ni eneo la kimkakati. Tusibweteke, tutumie fursa hii, tupitie upya Hotuba ya Mheshimiwa Rais, kila sekta ambayo imeguswa, basi ifungamanishe kila jambo linalopatikana kwa kuzipitia upya sera zetu na miongozo yetu mbalimbali kuhakikisha kwamba tunakwenda kuipeleka Tanzania katika uchumi huo wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abbas Tarimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, maana nilishakata tamaa, nilijua leo sipati nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana-huwataala* kwa kutuwezesha kuwepo hapa. Nakishukuru chama changu kwa kunipeleka mbele ya wananchi wa Kinondoni na hatimaye wakanichagua kwa

kura nyingi sana. Nawaambia wananchi wa Kinondoni niko imara, nina nguvu, nina akili ya kuwatumikia kwa nguvu zangu zote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu Latifa Hasnal Faizal na dada yangu kipenzi Zera Abbas Muhammad Ali ambao kwa kipindi chote wamekuwa ni silaha kubwa katika kuniwezesha kusimama nikawa imara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati akizindua Bunge hili la Kumi na Mbili, yenyewe inatosha kuwa ni dira ya vipaumbele kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu hili kwa kipindi cha miaka mitano inayokuja. Hata wataalam wa mipango wanaweza wakafyonza humo ndani na wakapata vitu ambavyo Watanzania wengine watavipokea kwa mikono miwili. Siyo rahisi kuandika hotuba kama ile, Rais lazima atakuwa ni mtu mwadilifu, ambaye amemweka Mungu mbele kuangalia Watanzania wanahitaji nini, awafanyie nini na nchi yake iko wapi na anataka aione iko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu ni mtu ambaye anaongozwa na hofu ya Mungu. Hii inanifanya niseme kwamba viongozi wa Serikali wawe ni wateuliwa Mikoani au Wilayani, Serikali Kuu wawe na hofu ya Mwenyezi Mungu katika kufanya kazi zao. Hapo tutafanikiwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nisome maneno ya Mwenyezi Mungu ambayo ameyasema. Aliwauliza binadamu lakini akajibu mwenyewe; iko katika *Surat Azuma* aya ya 9, nitaosoma kama ilivyo, anasema: "*Hal astawi?* (Anauliza, wanafanana?) *Aladhina yaalamuna waladhina laayaalamuna.* (Yule anayeijua na yule ambaye hajui, hawa watu wamoja wanafanana hawa?) Akajibu, Mwenyezi Mungu hakusubiri watu wamjibu, akasema, balaa (hapana)." Maana yake imekusudiwa mtu mwenye hofu ya Mwenyezi Mungu ni mtu ambaye amepata daraja kubwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu. Tushukuru kwamba tuna

Rais ambaye ana hofu ya Mwenyezi Mungu na ndiyo maana mipangoyake inakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, sisi Wabunge wote humu tumekuja hapa kwa niaba ya wananchi wa Tanzania, tunapozungumza humu ndani hatuzungumzi kwa utashi wetu, ni utashi wa wananchi waliotutuma. Wananchi wakitueleza kwamba nendeni Bungeni kazungumzieni suala fulani, kaiambieni Serikali yetu suala fulani, Serikali ni ya wananchi na Bunge ni la wananchi, wapi tunakinzana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kila Mbunge akisimama anaongelea kuhusu *TARURA*; Spika anazungumzia *TARURA*, kila mtu anazungumzia *TARURA*, jamani sasa ifike wakati Serikali msikie hili. Huo ndiyo uadilifu ninaouzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi humu ndani tukizungumza, maana yake ni kauli ya Mungu, ni kauli ya wananchi na hapo ndipo tutapata mafanikio. Kuna *options* nyingi tu ambazo zimewahi kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *TANROADS* hatuwezi tukapunguza fedha zake, iunganisheni na *TARURA* iwe ni kama *division* ya *TARURA*, wawe na mfuko mmoja mkubwa, wafanye kazi pamoja. Siyo lazima tuwe na utitiri wa vyombo, hapana, vyombo vinaweza vikawa vichache, kazi zikawa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Magufuli *is alone*, anasaidiwa na watu wachache lakini anafanya kazi kubwa, *it is possible!* Kwa nini hatumuigi Mheshimiwa Rais? Mbona kaitembelea Tanzania nzima? Wote humu ndani tumepata fadhila zake, tumetumia jina la Mheshimiwa Magufuli katika kupita. *Aljazaul-ihisani ilal-ihisani* (Anayekufanyia wema, mrudishie wema). Mheshimiwa Dkt. Magufuli katufanyia wema mkubwa katika Taifa hili. Tumrudishieni basi wema kwa kuwatumikia wananchi wake. *(Makofi)*

(Hapa kengele iligonga kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nisije siku nyingine nikaomba habari za Kinondoni Waheshimiwa mkanikatalia, lakini nataka ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kengele imeshagonga. Ahsante sana.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Basi nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex ajiandae.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mmoja wa wajumbe wa Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda niwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Kilwa Kaskazini kwa kuniwezesha kuwepo ndani ya Bunge hili kwa kunipa kura nyingi wakati wa Uchaguzi Mkuu uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujikita kwenye maeneo matatu katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais iliyosomwa wakati wa ufunguzi wa Bunge letu hili la Kumi na Mbili. Maeneo hayo ni sekta ya utalii, sekta ya afya na michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la michezo, kwa kuwa halijazungumzwa na Mbunge yeyote ndani ya Bunge lako hili, napenda unipe upendeleo angalau wa dakika mbili za nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 23 - 25 sekta ya utalii imefanunuliwa vizuri na kwa hakika kuna malengo mengi mazuri yametolewa.

Napenda niseme tu kwamba katika Wilaya yangu ya Kilwa kuna vivutio vingi vya utalii kama magofu Kilwa Kisiwani; kumbukumbu nyingi za kale kule Songo Mnara; mapango makubwa na madogo katika Wilaya yetu ya Kilwa; mabwawa yenye viboko wengi wenye tabia tofauti na maeneo mengine katika Bwawa la Maliwe katika Kijiji cha Ngeya kule Mitole na pia Mto Nyange kule Makangaga; Kumbukumbu za Vita vya Majimaji katika Kata ya Kipatimu, Tarafa ya Kipatimu, Kijiji cha Nandete; na pango kubwa ambalo linasadikiwa kuwa ni la pili kwa ukubwa Barani Afrika linalojulikana kwa jina la Nang'oma lililopo katika Kijiji cha Nandembo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naiomba Wizara yetu tushirikiane kuhakikisha kwamba tunavitangaza vizuri vile vivutio ili kuongeza vivutio vya utalii katika nchi yetu ambavyo vitatuhakikishia mapato mengi kwa ajili ya Serikali yetu. Yale mapango ya Nang'oma ni mapango yana historia kubwa na watafiti wengi kutoka nchi mbalimbali kama Italia, Ujerumani na Uingereza wamekuwa wakija mara kwa mara, lakini kuna changamoto kubwa katika hivyo vivutio nilivyovitaja kwenye suala la miundombinu ya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara haziko katika hali nzuri, kwa mfano ukitaka kufika kule ambako vita vya majimaji vilianza Nandete au kule kwenye pango la Nang'oma ambako inasadikiwa kwamba wakati wa vita vya majimaji akinamama na watoto walikwenda kujificha kule wakati akinababa walipokuwa wanaendelea na vita vya majimaji. Ningeomba miundombinu iboreshwe kwa barabara ya kutoka Tingi pale Kijiji cha Njia Nne kwenda Kipatimu lakini vile vile barabara ya Nangurukuru – Liwale ambayo ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM basi ifanyiwe taratibu za haraka ili kuweza kuhakikisha kwamba inaboreshwa na vile vile barabara inayokwenda Makangaga – Nanjilinjji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex na Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete ajiandae.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi uliyonipatia ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote nipende kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye amenijaalia uzima na afya njema hatimaye nimekuwa mmoja wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mbeya kwa namna ambavyo wamenipatia kura nyingi ambazo zilisababisha jina langu kupelekwa kwenye Kamati Kuu Taifa. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu ambaye ndiyo Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi Taifa. Namshukuru yeye pamoja na Kamati Kuu kwa kupendekeza jina langu nami nimekuwa Mbunge sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikupongeze wewe kwa kuwa Mbunge wa Mbeya Mjini. Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu hongera sana kwa kuwa Mbunge wa Mbeya Mjini na Mbeya Mjini sasa imetulia kama lilivyo jina lako. Napenda vile vile kuwashukuru sana wananchi wa Mbeya Jiji na wananchi wa Mkoa wa Mbeya wote kwa ujumla kwa namna ambavyo waliweza kukichagua Chama Cha Mapinduzi kwa kura nyingi za heshima. Napenda kuwashukuru Watanzania wote kwa ujumla. Tanzania yetu sasa inapendeza, imekuwa ni ya kijani na ina amani ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa nzuri anazozifanya ambapo Tanzania yetu sasa inatambulika dunia nzima na inaheshimika

dunia nzima kwa namna anavyoleta maendeleo kwenye nchi yetu. Nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa nafasi zao hizo. Natambua ni watu makini na ni mahiri sana watazitendea haki kwa maana ya kuisaidia Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mbeya katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, namshukuru sana Mheshimiwa Rais alisema kwamba kwenye hotuba ile atavipa vipaumbele sana vikundi tofauti tofauti kwenye mikopo kwa maana ya kwamba viendeleo kusonga mbele. Naomba sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba hii awape kipaumbele wanawake wa Mkoa wa Mbeya na Tanzania yote kwa ujumla, maana akiwezesha mwanamke, mwanamke ndiyo kila kitu, mwanamke ndiyo mama ambaye anajali familia, anasaidia Watoto, anamjali hata baba pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuomba asilimia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Naibu Spika, kengele imenikatili, lakini nitaandika kwa sababu napenda sana kuongelea habari za wanawake namna gani waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, atafuatiwa na Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kabla sijaendelea naomba niunge mkono hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa upendeleo mkubwa alionipatia na kuweza kuingia tena ndani ya Bunge hili ambalo mimi ni mara yangu ya pili, Bunge la Kumi na Mbili. Pia naomba nitumie nafasi hii kukishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi kwa kuweza kutenga nafasi maalum kwa kundi la watu wenye ulemavu, nafasi ambazo zilikiwezesha chama kunichagua mimi kuwa Mbunge wa Bunge hili la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana akinamama wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa jinsi ambavyo wameendelea kuniamini, pia akina mama wa UWT, Baraza Kuu ambao wameniwzesha tena kuingia ndani ya Bunge hili niweze kuwakilisha wanawake, watu wenye ulemavu pamoja na Watanzania wote kwa ujumla. Ahsanteni sana akinamama, nawaahidi ya kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuishukuru sana familia yangu, lakini pia watumishi wa Mungu ambao wamekuwa wakiniombea mchana na usiku, maombi ambayo yameniwzesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo kila iitwapo leo. Naomba niendeleo kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufuli, jembe letu, tingatinga kwa ushindi mkubwa ambao ameupata katika uchaguzi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kuwaza kwa sauti, hivi Watanzania tungekuwa ni watu wa aina gani na kwa kweli niseme hata shetani angeweza akatushangaa kumnyima kura Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa hospitali hizi alizotujengea, lakini kwa umeme huu aliotuletea, barabara na pia kwa jinsi ambavyo alihakikisha kwamba kizazi chetu kinasimama imara kwa kukomesha dawa za kulevya. Kwa jinsi ambavyo ameweza kusimamia vitendo vya rushwa na kutokomeza kabisa rushwa ndani ya Taifa letu. Hakika shetani angeweza kutushangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengi ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya, lakini katika hotuba zake, nimesoma hotuba yake vizuri, nimeirudia tena hotuba yake ya mwaka 2015 na ya 2020. Hotuba hizi zimejieleza vizuri na zinaonesha kabisa ni kwa jinsi gani Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amedhamiria kulitoa Taifa letu kutoka sehemu moja na kulipeleka sehemu nyingine lakini pia ameweza kuonesha kwa vitendo katika awamu yake ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana tukiwa kama Watanzania, lakini pia kwa kundi la watu wenye ulemavu hatuna budi kuendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa jinsi ambavyo ameendelea kuyasimamia masuala ya watu wenye ulemavu na kuhakikisha kwamba kundi la watu wenye ulemavu na lenyewe linapata heshima katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri mambo mawili kwa upande wa kundi la watu wenye ulemavu na hasa kwenye eneo la matibabu. Wakati wa kampeni niliweza kutafuta kura pia kwenye kundi la watu wenye ulemavu na changamoto mojawapo ambayo waliiongelea ilikuwa ni changamoto ya matobabu ambapo hapo kabla kulikuwa na utaratibu ambao ulikuwa unatumika, utaratibu wa utambulisho. Yaani mtu mwenye ulemavu anapoumwa yule ambaye hana uwezo, basi anaenda kwa mtendaji wa Kijiji ama Mwenyekiti wa Kijiji na hatimaye anaweza kutibiwa. Waliweza kuniambia kwamba utaratibu huu sasa hivi hauko vizuri sana, kwa hiyo suala la matibabu kwao inakuwa ni changamoto. Niiombe Serikali sana iweze kuuhuisha utaratibu huu wakati tunasubiri sasa ule mfumo wa Bima ya Afya kwa watu wote ili sasa kundi hili la watu wenye ulemavu liweze kunufaika na utaratibu wa matibabu kwa wale ambao hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nitumie nafasi hii kuweza kuishauri Serikali na kuiomba na kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kwenye eneo la *TARURA*.

Tumeona kwamba mabadiliko ya tabianchi yameendelea kutuathiri sana na hivyo mvua za mara kwa mara zimekuwa zikiathiri miundombinu yetu. Kwa hiyo, niiombe Serikali iweze kuipa nguvu kubwa *TARURA* ili sasa hii miundombinu yetu iweze kuwa vizuri wakati wote. Mara nyingi tunapokuwa tunawasiliana na *TARURA* kama Wabunge wanalalamikia changamoto ya bajeti, kwa hiyo niiombe sana Serikali iweze kuliangalia hili na kulipa kipaumbele ili sasa miundombinu yetu iweze kuwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuendeleo kumwomba Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ili aendeleo kuliongoza Taifa letu na Mwenyezi Mungu aendeleo kumpa hekima na maarifa ya kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko na Mheshimiwa Kiswaga Jackson jiandae.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyeweza kunipa uhai leo nimesimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee zaidi naomba niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Mara walioweza kunichagua mimi kuwa mwakilishi wao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuweza kuiteua mimi kuwa Mbunge. Pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi leo nimesimama kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nimpongeze Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi kubwa aliyoyifanya ya

kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 – 2020. Mheshimiwa Rais wetu mpendwa amefanya kazi kubwa sana katika nchi yetu. Kikubwa zaidi Mheshimiwa Rais wetu katika Mkoa wangu wa Mara amejikita kufanya mambo mengi makubwa sana ambayo yamesababisha nchi yetu imepiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite katika suala la afya. Mheshimiwa Rais wetu mpendwa katika Mkoa wangu wa Mara amefanya mambo makubwa katika Sekta ya Afya hasa upande wa hospitali, amejenga zahanati takriban 45 mpya, lakini pia vituo vya afya 13 vipya, amejenga hospitali za wilaya saba mpya. Kipekee kabisa Rais wetu ameweza kutupatia takriban zaidi ya bilioni 15 kuhakikisha tunajenga hospitali ya rufaa maarufu kwa jina la Kwangwa iliyokuwa imekaa zaidi ya miaka 40 sasa inafanya kazi katika kitengo cha mama na mtoto. Mheshimiwa Magufuli apewe sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi naomba niende kuchangia katika hotuba aliyotoa ya ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili. Mheshimiwa Rais wetu aliongea hotuba ambayo ilisababisha sisi kutupa dira, maono na mikakati mikubwa ya mstakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Mheshimiwa Rais wetu kwa hotuba hii ambayo Rais aliitoa imegusa kila eneo la Taifa hili ambayo naomba nielekee katika kundi la wanawake, lipewe fursa kubwa kwenye taasisi za kifedha kama mabenki. Nina Imani ili akinamama hao ambao wamekuwa ni sehemu kubwa mama zetu hawa ambao wamekuwa ni sehemu kubwa katika kulijenga Taifa letu waweze kupata fursa kubwa katika kupunguziwa masharti ya kupewa mikopo ya nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uhakika nilionao niwaombe masuala ya kuhakikisha wanawake wanapata fursa ya kukopeshwa, naamini watakaoweza kukopeshwa wataweza kuonekana katika ujenzi wa Taifa hasa katika suala la Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua mama zangu wana changamoto kubwa hasa katika masuala ya kiafya. Nijikite kwenye kusema kwamba masuala ya tatizo la kiafya hasa ugonjwa wa akinamama wa kansa ya matiti na ya kizazi, hawa akinamama wanapata tabu sana hapo bada ya kuwa wanakosa huduma pale ambapo Madaktari wanakuwa hawapo pale. Sasa naomba niishauri Serikali...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Kiswaga Jackson na Mheshimiwa Aleksia Kamguna ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii nami kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza kabisa napenda kutoa pole kwa familia ya Mzee Waheke kwa kifo cha mzee Waheke, lakini pia kwa familia ya Mzee Mantago kwa kifo cha bibi yetu mpendwa Bhoke ambaye amefariki muda mchache katika hospitali ya Benjamin Mkapa. Mwenyezi Mungu azilaze roho hizi mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza tu kwenye hotuba ya Rais ukurasa wa 66 ambao amezungumzia kuhusu elimu. Kama Taifa tunatakiwa kuwekeza kwenye elimu. Ukiangalia tulivyo sasa, elimu ya msingi, sekondari na hata vyyo vikuu bado tuna changamoto kubwa sana na ili tuweze kuwa na elimu bora na kupata wataalam wa fani mbalimbali ambao wamebobeza na kuweza kupunguza umaskini katika Taifa letu na hapo kukuza uchumi, lazima Serikali itoe kipaumbele kwenye elimu. Leo ukiangalia miundombinu bado iko *dhofli-hali*. Tuna shule watoto wanakaa chini ya miti. Watoto wanakaa kwenye mawe, Walimu ofisi zao ni kwenye

miti, leo hatuna madawati, vitabu vya kutosha; Walimu badala ya kupata motisha, wengi hawana mishahara wala hawana nyumba. Sasa haya yote tusipoyaboresha hatutakuwa na watu ambao wameelimika na Taifa lililoelimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchache sana hapo nashauri Serikali itatue tatizo la upungufu wa walimu mashuleni. Serikali iliondoa walimu wengi sana kupitia vyeti *fake* lakini haikuweza kufanya *replacement* na walikuwa tayari kwenye *payroll*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kabla walimu wa vyeti *fake* hawajaondolewa tulikuwa tuna upungufu mkubwa sana wa walimu. Unakuta shule ina mwalimu mmoja au walimu wawili, unategemea watoto wafaulu katika shule hii? Nashauri kwanza Serikali iharakishe ku-*replace* wale wote ambao walitolewa kwa vyeti *fake* maana kuna Watanzania wengi mtaani ambao wana sifa za kuwa walimu wawaajiri lakini pia kuajiri walimu kwa ajili ya shule hizi ambazo hazina walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye vyyo vikuu amesema anaongeza bajeti ya wanufaika wa mikopo ya vyyo vikuu, ni jambo jema sana. Hata kwenye kampeni yake 2015 alisema hata kubali kuona mtoto wa Kitanzania ambaye ana sifa za kwenda chuo kikuu anakaa bila kupata mkopo. Sasa kupata mikopo ni jambo moja na jema lakini hawa wanufaika wa mikopo hii badaye wanakuja kukaa kwenye kaa la moto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Sheria ile ya 2004 na marekebisho ya 2016 makato ni makubwa sana. Huyu Mtanzania unamkata asilimia 15 ya mshahara wake baada ya miaka miwili tu baada ya kuhitimu kama ameajiriwa na kama hajaajiriwa atatakiwa kulipa Sh.100,000/= bila kujali anazipata wapi; unamkata asilimia 6 ya kulinda thamani ya fedha; unakatwa asilimia 10 iwapo amechelewesha kama *penalty*; na unakatwa asilimia 1 ya kusimamia ule mkopo. Mtu huyu unakatwa makato mengine mengi; kuna *NSSF* hapo

asilimia 10, bima, *Pay As You Earn* ambayo tunaipigia kelele, kodi ya wafanyakazi ni kubwa sana haijawahi kurudi hata kwenye *single digit*, huyu Mtanzania atabaki na shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado hapo mtu huyu anatakiwa akope, hata sisi Wabunge tumekuja hapa tumekopa yaani ule mshahara wetu sisi tumekopea. Sasa huyu mfanyakazi ambaye ana mlolongo mwingi wa makato naye atataka kukopa ili aweze kujinufaisha, atakuwa anabaki na shilingi ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza swali hapa na Waziri hakunijibu kifasaha ingawa alisema tunaweka hivi ili makusanyo yawe mazuri, tumekusanya asilimia 46. *I think* tatizo ni *recovery system* ili hii mikopo iweze kurejeshwa na siyo kuongeza *rate* ambazo zinazababisha makato kuongezeka. Kama Taifa *in fact* ilitakiwa tuwekeze kupata wajuzi wa fani mbalimbali *at the level of university*. Tena tungekuwa tunawapa mikopo kwamba warejeshe tu bila hizo riba nyingine na tuwape muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi unakuta wengi, hasa ambao hawajaajiriwa, wanajificha, hawezi akafungua hata *account*, anaogopa. Sasa hivi mtu anajifanyia biashara zake au anaweza akaingia tu mkataba wa ajira siyo za Serikalini ili nisigundulike nisije kukatwa hayo makato ambayo mmeyaweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya kwanza yanasababisha moja, hata benki zetu zinashindwa kupata hawa wateja, kwa sababu, nikiamua kujificha hata akaunti sitafungua. Pili, hata nyie Serikali kwa kufanya hivyo mnakosa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili marejesho ya-*boost* kutoka asilimia 46 tupunguze ije 8 hata tano, watakuwa wengi ambao wanaleta marejesho haya na watoto wetu wengine wengi wataweza kufaidika. Naomba sana Serikali mlichukue hili mlifanyie kazi, *it is a burden to these people* wanaokopa ambao ni watoto wa kimaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kiswaga Jackson, atafuatiwa na Mheshimiwa Aleksia Kamguna, Mheshimiwa Asenga Abubakari ajiandae.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ya kipekee niliyopewa ya kuweza kuchangia hotuba ya Rais. Kwa kweli, kwanza nimshukuru Rais mwenyewe na Chama changu cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi ya kugombea kuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga. Pia niwashukuru wananchi wa Kalenga pamoja na familia yangu kwa kunisimamia, kuniamini, kuniombea, mpaka leo nimesimama hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ameendelea kuliweka Taifa hili katika hali ya amani. Ndiyo maana hata leo Watanzania tunaweza kufanya mambo yetu kwa uhuru ni kwa sababu, tunaye Rais ambaye anapenda amani na kweli ameilinda amani. Pia namshukuru Rais kwa sababu ya nidhamu kubwa ambayo ameileta kwenye Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, George Washington alisema kwamba imani ni roho ya jeshi. Jeshi dogo katika kukaa kwa pamoja linaweza likafanya mambo makubwa. Ndiyo maana sasa kama nchi tumeweza kuingia katika uchumi wa kati kwa sababu ya ile nidhamu kama Taifa ambayo tumejijengea. Kwa hiyo, nimshukuru sana Rais kwa ajili ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi na Watanzania wengi tunamuunga mkono, tuko pamoja naye pamoja na vijembe vinavyoendelea vya watu wasio na macho ya kuona uzalendo mkubwa huu unaofanywa na Rais wetu. Tupo Watanzania ambao tutamtetea usiku na mchana na nchi hii itafika kwenye hatima yake tukufu na sisi tukiwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa habari ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais yako mambo mengi, lakini mimi niliona nianze kujielekeza kwenye kilimo. Upande wa kilimo hii Program ya Pili ya Kuendeleleza Sekta ya Kilimo ukiitizama imejaa majawabu mengi sana ambayo yataleta majawabu makubwa ya upungufu wa chakula katika Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nafahamu kwamba bado haijaanza kupewa pesa. Kama hii Program ya Pili ikianza kupewa pesa tutatutua changamoto nyingi kwenye kilimo. Kwa mfano, tumeleza kwa mapana sana ni namna gani tutakwenda kutengeneza skimu za umwagiliaji. Tukianza kuipatia pesa tunaweza kuanza kuwapa Maafisa Ugani pesa kidogo, kwa mfano Afisa Ugani mmoja kwa kila kata; tukachagua kata fulani kwamba huyu akatengeneze miche ya korosho, huyu akatengeneze kishamba-darasa chake cha miche ya parachichi watu wakaenda kujifunza pale wakapata ujuzi na wakaendelea. Serikali ina-*finance* kwa kumpa ruzuku na yeye huyu Afisa Ugani atapata pesa kwa sababu utakuwa ndiyo mradi wake. Tukifanya namna hii tutakuwa tumetengeneza motisha kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni namna gani tunalinda ardhi. Ardhi yetu imeendelea kufa kwa sababu ya sumu kali. Je, hizi mbolea ambazo tunaleta sijui tunazikaguaje kwa sababu nimepita maeneo mengi yalikuwa mazuri unakuta sasa hakuna kinachoota kwa sababu ya mbolea za sumu. Suala hili tuliangalie sana namna gani tunaweza kulinda ardhi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye mbegu, hata Rais ameendelea kuzungumza. Ndugu zangu sasa hivi biashara kubwa duniani ambayo itakuwa kama ya mafuta ni biashara ya mbegu. Kuna vita kubwa hawa wakubwa kutuletea mbegu, nimeona sehemu fulani walileta migomba ikawa inazaa sana lakini mwishoni inaoza. Kwa hiyo, kama Taifa ni lazima tujielekeze katika kutunza mbegu zetu za asili ili tusifike mahali tukawa watumwa na tukizembea tutakuwa watumwa kwelikweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni linalohusu masoko kwenye kilimo. Watu wamekuwa wakizungumza kwamba tusiuze bidhaa Kenya. Haya ni makosa makubwa na nisingependa mtu azungumzie habari ya kutokuuza bidhaa Kenya. Mimi nalima parachichi pale Njombe, Wakenya wanakuja shambani kwangu wananunua kilo moja Sh.1,500/= parachichi inayobaki naenda kuuza kiwandani kilo moja Sh.300/= sasa wewe unasemaje Mkenya asije kununua, nikauze wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la msingi tulete ushindani. Tuhimize wafanyabiashara wakubwa kama ilivyo kwa Coca washindane lakini usizungumzie habari ya kutokuuza Kenya ni kosa kubwa sana hilo. Kwa hiyo, suala la masoko kwanza tuache kuwazuia Watanzania kuuza bidhaa zao nje kwa sababu tunavyowazuia tunapunguza pia tija mazao yanaendelea kuoz. Kwa hiyo, hilo ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine kwenye kilimo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aleksia Kamguna, atafuatiwa na Mheshimiwa Asenga Abubakari, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo kwa mara ya kwanza katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa

kuniteua pamoja na vyombo vyote vya Chama cha Mapinduzi hatimaye nimefika hapa katika hili Bunge. Nasema ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia wapiga kura wangu wanawake wa Mkoa wa Morogoro ambao wameniwzesha kuja hapa leo na kuwa msemaji wao. Mwisho naishukuru familia yangu ambayo ilikuwa bega kwa bega na mimi hatimaye nimefikia hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima nimesimama hapa kusema Mheshimiwa Rais tuliyenaye leo sio wa kawaida tumepewa zawadi kutoka kwa Mungu. Kwa maana ukisafiri mataifa mengine wanauliza huyu Rais wenu ni nani na amepata wapi ujasiri wa kufanya haya mambo yote? Naamini ni nguvu za Mungu na pia ameamua kuwakomboa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ametukomboa kupitia nidhamu ya kazi. Tanzania nidhamu ya kazi ilikuwa imeshuka lakini yeye ameamua kuisimamia nidhamu hasa katika Serikali. Namshukuru sana na kumpongeza, tunamwomba kwa Mungu aendelee na moyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema sisi wanawake ni wanyonge lakini ninaamini sisi siyo wanyonge, akina mama ni Taifa kubwa. Mheshimiwa Rais ametupigania kwenye uzazi kutoka vifo 11,000 hadi 3,000, tunamshukuru sana. Hii ni kazi tuliyopewa na Mungu kwamba mwaname atakula kwa jasho lakini mwanamke atazaa kwa uchungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke atazaa kwa uchungu lakini ukiliangalia sana katika Taifa letu sasa hivi au katika hili Bara la Afrika mwanamke ana kazi kubwa, yeye anazaa kwa uchungu na bado anakula kwa jasho. Kwa hiyo, ndugu zangu akina mama naomba tusimame kifua mbele hasa Rais wetu kwa jinsi anavyotutetea katika nyanja zote ambazo wenzangu wamezitaja sina budi kuzirudia, upande wa elimu, afya, maji ametutua ndoo, miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nijikite katika sehemu moja ya ukurasa wa 39. Naomba ninukuu: "Tutashughulikia pia kero mbalimbali za wananchi ikiwemo migogoro ya ardhi na mirathi." Mimi naomba nijikite upande wa mirathi. Kwa nini nilisema wanawake ni Taifa kubwa, wanawake tuna nguvu? Anayepata shida katika miradthi ni mwanamke ndiyo maana namzungumzia mwanamke na mtoto. Mwanamke ni nani? Mwanamke ni mama mzazi, ni mlezi, ni daktari, ni mwalimu na ni hakimu kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke anapendeza anapoolewa tunamvisha nguo nyeupe, lakini mwanamke huyu siku akifiwa ananyanyasika, hasa wa Kitanzania. Kwa nini huyu mwanamke ananyanyasika kiasi hiki ambapo yawezekana ile mali waliyoichuma wakati mume wake akiwa hai yeye alichuma zaidi kuliko mume wake? Yawezekana alikuwa na kipato kikubwa kuliko mume wake lakini mwanaume akifariki mwanamke yule anakuwa si kitu wala si chochote? (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imegonga Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuiangalie hii sheria ili tubadilishe mwanamke aweze kuthaminiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asenga Abubakari, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Festo Sanga ajiandae.

MHE. ABUBAKARI D. ASENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu, Mheshimiwa Rais, Chama changu cha Mapinduzi na

wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kunipa imani ya mimi mtoto wa fundi charahani mwenye nywele za kipilipili leo kusimama hapa kuwawakilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu ya dhati kaka yangu Mheshimiwa Polepole atanisaidia kufikisha shukrani zangu zote kwa chama kwamba sisi vijana tunawashukuru sana. Sisi vijana wadogo ambao tumepata nafasi ya kuingia katika Bunge hili tuna imani kubwa na *ma-senior* mliokuwepo humu mtatusaidia sana kutufundisha na kutuelekeza bila kutuacha tuharibikiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Wabunge wenzangu wengine wamechangia, nami nitumie fursa hii kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwa vijana na katika maendeleo ya nchi yetu. Nitachangia katika sekta mbili au tatu, ya kwanza miundombinu ambayo ameizungumzia katika ukurasa wa 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 mimi nilikuwa mgombea wa Ubunge wa Chama cha Mapinduzi japokuwa sikutangazwa, Mheshimiwa Rais alifika jimboni kwetu, tulimuomba ujenzi wa barabara ya lami ya Ifakara – Kidatu kwa kiwango cha lami. Barabara hii haikuwapo kwenye Ilani lakini kwa mapenzi yake Mheshimiwa Rais aliahidi ataijenga na akaleta mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba wasaidizi wa Mheshimiwa Rais kuifuatilia barabara hii kwa ukaribu. Namshukuru sana Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Eng. Chamuriho alifika ameona changamoto za Mhandisi Mshauri (*consultant*) ambaye amekuwa aki-*delay* katika mambo ya *GN* na *designing* ili ahadi hii ya Mheshimiwa Rais iweze kutimilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jambo hilo kwa kuongezea kidogo ni kwamba katika swali langu la msingi Mheshimiwa Waziri amejibu hapa kwamba barabara hii itakamilika Oktoba 2021. Sisi ambao tuko *site* kule ukitazama

unaona muda huu ni mfupi sana. Kwa hiyo, naomba Wizara ifuatilie kwa makini barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni katika elimu. Mheshimiwa Rais akituhutubia hapa Bungeni aliahidi jambo la msingi kwa dada zetu, wasichana wa nchi hii kwamba atajenga sekondari za watoto wa kike kila mkoa. Naomba Wizara husika iliharakishe jambo hili lifanyike kwa wakati. Mkoa wetu wa Morogoro, Jimbo la Kilombero liko katikati ya Mkoa mzima. Pendekezo langu Wizara itakapojenga shule hizi ijenge katikati ya Mkoa ili kutoa nafasi kwa majimbo na wilaya zote kupeleka watoto pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika elimu, mjadala umekuwa mwingi sana hapa kuhusu suala la elimu ya chuo kikuu. Mheshimiwa Rais amesema katika hotuba yake ukurasa wa 33 mabilion ambayo Serikali inatoa kwa mikopo ya elimu ya chuo kikuu. Pendekezo langu ni kwamba vile vyuo vya umma, mathalani *University of Dar-Es-Salaam*, Chuo Kikuu cha Dodoma, Serikali inalipa mfagizi, dereva mpaka anaepeleka karatasi pale, kwa nini tusifikie hatua ya kusema kwamba vyuo vya umma wanafunzi wasilipe ada kwa sababu Serikali inapeleka pale kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mjadala huu wa mikopo, Bodi ya Mikopo, asilimia za kukatwa kuja kulipa ni kubwa, anapata huyu huyu hapati, lakini kwa sababu Serikali inapeleka huduma zote katika vyuo vya umma kwa kuanzia nilikuwa nashauri tuanze kulifikiria hilo. Mheshimiwa Rais amefanya vizuri sana katika elimu bure lakini tunakokwenda tufikirie vyuo vya umma ambavyo Serikali inahudumia kila kitu kwa nini mtoto wa Kitanzania asiende kusikiliza *lecture* akapata ufahamu? Kuwe na mjadala baadaye ama anatokea nyumbani ama anatokea wapi lakini afike apate nafasi ya kusoma chuo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mjadala hapa kuhusu kazi nzuri ambazo Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli amefanya. Mimi kubwa kuliko yote ni suala la kunifanya nijiamini kama Mtanzania. Mimi kama kijana wa

Chama cha Mapinduzi nimezunguka katika nchi za Afrika na tulikuwa na mafunzo ya vijana wa Afrika, hasa Afrika ya Mashariki, kuna nchi hapa walikuwa wanajisifia na Marais wao, leo sisi tukienda tunaheshimika kwa Rais wetu, ndiyo salamu yetu ya kwanza. Kubwa kuliko yote ni hilo Rais amenifanya mimi najiamini kila sehemu na kila wakati amekuwa akirudia kusema Watanzania tuwe makini tunaweza, Tanzania ni tajiri, ile imani inatufanya tunashinda vita. Hilo ni kubwa kuliko yote na ndiyo maana linakuza mjadala hapa.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Aboud Hassan, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila ajiandae.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hii aliyotupa Chama chetu cha Mapinduzi kushinda ushindi wa kishindo na baadhi yetu kuturejesha Bungeni. Nampongeza sana Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwani leo Chama cha Mapinduzi na wanachama wake kinatimiza miaka 44 tangu kuzaliwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kauli yake aliyotoa ndani ya Bunge hili kwamba atashirikiana bega kwa bega na Rais wa Zanzibar pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kwamba Zanzibar inasonga mbele kiuchumi na wananchi wake wananyanyuka kiuchumi. Amedhihirisha hilo kwa kusema kwamba kwenye uvuvi wa bahari kuu anapeleka meli nne Zanzibar ambapo meli nne hizo zitasaidia Zanzibar katika dhana yake ile ya uchumi wa *blue*. Zanzibar sasa imejipanga

kuingia kwenye uchumi wa *blue* na hapa Mheshimiwa Rais wa Muungano ameonesha dhamira yake ya dhati Zanzibar kuingia kwenye uchumi wa *blue*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najihusisha sasa kwenye sekta ya kilimo. Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake ameonesha dhamira ya dhati kwamba sasa anataka kumnyanyua mwananchi mdogo mdogo na mkulima mdogo mdogo, mvuvi pamoja na wafugaji ili waweze kupata tija ya kilimo chao, tija ya uvuvi wao na tija ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali, Mheshimiwa Rais aliahidi kuwapunguzia kero wakulima na wavuvi na ameonesha kwamba tumepunguza tozo na kodi mbalimbali 114 ambazo zinamlenga mvuvi, mkulima na mfugaji na amesema wazi kwamba ataendelea kuangalia kero na tozo mbalimbali ambazo zinawagusa wakulima, wavuvi na wafugaji. Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira ya dhati kuwasaidia wakulima wa bustani ambapo wakulima wa bustani walikuwa na changamoto kubwa sana katika usafirishaji wa mazao yao. Kwa hivyo sasa Serikali imepanga kununua ndege ambayo itasaidia kupunguza changamoto za kusafirisha mazao hayo ya bustani ambayo mazao ya bustani yana soko kubwa katika nchi za nje, tatizo ilikuwa jinsi ya kuyafikia masoko hayo. Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira kwamba sasa masoko hayo yatafikiwa na wakulima watapata faida ya mazao yao wanaozalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakuwa bora na endelevu na chenye tija, lazima sasa tuwekeze kwenye mbegu bora, mbegu ambazo zitalingana na udongo wa nchi yetu na mazingira yake na maeneo husika, lakini mbegu ambazo zitaangalia mazingira yanayohusika linapolimwa zao husika. Ni vema sasa tukaziimarisha taasisi zetu zinazohusiana na uzalishaji wa mbegu pamoja na viuatilifu ili viweze kutatua changamoto ya mbegu na viuatilifu kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea katika kilimo, naunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais za kutaka sasa

kilimo kiwe kilimo cha kisasa, kilimo chenye tija ambacho kitakuwa kilimo cha umwagiliaji. Sasa ili kuhakikisha kwamba kilimo cha umwagiliaji kinafanikiwa ni vyema sasa tukaimarisha pia kwenye sekta ya maji ambayo itasaidia kwenye viwanda, ukulima, uvuvi na ufugaji. Tukipata maji ya kutosha kwa wananchi lakini pia maji ya kuimarisha kilimo chetu, nashauri Serikali Mfuko wa Maji uongezewe fedha ili kukidhi mahitaji hayo ya wananchi. Nasema hivi kwa sababu fedha ambazo zimetumika kwenye Mfuko wa Maji zimeonesha kutoa mafanikio makubwa katika kutatua changamoto za maji na hivyo tukiongeze fedha kwenye mfuko wa maji, tutaisadia sasa TAWASA ili iweze kukabiliana na changamoto za maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumaliza, naomba nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano, wasaidizi wake wote, Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe kwa kulisimamia Bunge letu hili tukaweza kutekeleza yote ambayo tumefikia kwa sababu kazi ya Bunge ni kuishauri Serikali na kuisimamia. Bunge hili Bunge hili lilifanya kazi hiyo na ndiyo maana maendeleo haya yakafikiwa na nategemea wataendelea kufanya hivyo na sisi Wabunge tuko pamoja na wao na Serikali yetu kuhakikisha tunafikia pale tulipokusudia, kumpa Rais wetu imani na kumpa Rais wetu hamu ya kututetea na kutuletea maendeleo. Ameonesha dhamira ya dhati kwamba yeye ni Rais wa wanyonge na anatetea wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Gerad Mwandabila, muda wetu ukiwa unaturuhusu atachangia Mheshimiwa Atupele Fred Mwakibete.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge hili, nipende kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa nafasi niliyoipata. Pia niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la

Makete kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao. Kubwa zaidi nimpongeze Mheshimiwa Rais na Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa walioupata, ni kitu ambacho mimi kama Mbunge kwa kweli niseme hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais naomba kuchangia mambo matatu. Jambo la kwanza naomba kuchangia kwenye sekta ya barabara. Tumeona jitihada za Rais akipambana kuhakikisha kwamba barabara zinajengwa kwenye kila kona ya nchi hii, wilaya na kila mkoa. Kwa kule Makete sisi tumepata barabara kutoka Njombe kuelekea Makete ambayo imekamilika kwa kiwango cha lami. Naomba kuishauri na kuiomba Serikali tuna barabara ya kutoka Makete kuelekea Mbeya, moja kati ya barabara ambazo zimebeba msingi wa uchumi wa Wilaya ya Makete, nawaomba na nawasihani sana wahusika ambao ni Wizara ya Ujenzi waiangalie barabara hii kwa jicho la karibu ili wananchi wa Makete waweze kupata huduma hiyo ya barabara ya lami, kwa sababu uchumi wa Makete unakua lakini unakwamishwa na barabara hiyo ambayo kwa kweli ni barabara muhimu wa Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba nichangie kwenye sekta ya kilimo. Sisi Makete ni wilaya ya kazi kama ambavyo wananchi wengi wa Tanzania wanafahamu wananchi wa Makete ni watu wa kazi. Kwenye kilimo Mheshimiwa Rais ameonyesha kwenye hotuba kwamba ana lengo la kuboresha kilimo. Changamoto ya kwanza kwa wananchi wa Makete tunalia na lumbesa kwa ajili ya wananchi wetu na wakulima wetu wa Makete. Wakulima wanalima lakini tatizo la lumbesa kwa wananchi wetu ni kubwa. Naishauri Serikali mambo matatu; ushauri wa kwanza kwenye Serikali ni jambo moja, kwanza Wakala wa Vipimo waoneshe kipimo kipi ni rasmi kwa ajili ya kuuzia mazao yetu ya mahindi pamoja na viazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba Wizara husika ya Kilimo waanzishe *sales point* (vituo vya

kuuzia) ili wakulima wetu waweze kuwa *controlled* kwenye biashara kuondokana na suala la lumbesa. Lumbesa ni kilio, wananchi wangu wa Matamba, Makete na Ujuni wanalia na lumbesa, tunaomba sana ili tuweze kumboresha mkulima huyu lazima tuondoe suala la lumbesa na nawasihi na kuwaomba sana Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la tatu, naomba kuchangia kwenye suala la mapato. Rais amezungumza mambo mengi sana; hapa tuna mambo ya ujenzi wa barabara, tuna mambo ya umeme, tuna mambo mengi ya kiuchumi ambayo yanahitaji fedha, lakini kuna eneo moja ambalo tumeliacha kwa muda mrefu fedha nyingi zinapotea, nako ni kwenye suala la tozo, kwa maana ya kwamba *non tax revenue*. Rais amepambana kwa *level* yake, kwa maana ya kwamba ukiangalia kwenye eneo kama la vitambulisho vya wajasiriamali, mambo ya magawio saa hizi tumeanza kuyapata, naiomba na kuishauri Serikali waanzishe *authority* kwa maana *non tax revenue authority* ili iweze kukusanya tozo hizi ambazo zimekuwa zikipotea. Mambo ya *fees* na mengine yanapotea huko na wafanyabiashara wetu wengi wanahangaika kuona kwamba wanafuatwa fuatwa sana na watu ambao ni wa tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ili tuwasaidie wafanyabiashara, ukifuatilia wafanyabiashara wengi ndani ya nchi yetu ya Tanzania wanaotaka kuanzisha biashara ndogondogo, wanafuatwa na watu wa tozo wengi wengi sana, mtu anaanzisha biashara, hajatulia anaingia mtu wa *TBS*, anaingia mtu wa *NEMC*, anaingia mtu wa *OSHA*, anaingia mtu wa *Fire*, anaingia mtu wa *TFDA*, mfanyabiashara huyo ambaye tunatamani awe bilionea kama Rais anavyotaka, atawezaje kama hatuwezi kuanzisha kitu ambacho ni kimoja, tuweza kuweka *single point*, huyu mtu akilipa kwa pamoja Serikali itafute jinsi gani inaweza ikagawana hayo mapato, siyo kufunga safari kwa kwa mfanyabiashara mmoja watu 20 kwenye Serikali ile ile. Naisihi na naiomba Serikali ianzishe *Non Tax Revenue Authority* ili tuweze ku-*control* hizi tozo ndogondogo ambazo zinapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo niendeleo kumpongeza Rais hata kwa wenzetu tulionao humu ndani ya Bunge, wa upande wa pili, ni kwa sababu Rais aliruhusu demokrasia kwenye nchi hii ndiyo maana na wao wapo. Ninachowasihi ni jambo moja, wawe watulivu, walikotoka wanalaumiwa na hapa wanatulaumu sisi, sasa hawajielewi walipo, wafanyiwe *counseling* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Neema Gerad Mwandabila, atafuatiwa na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete na tutamalizia na Mheshimiwa Esther Maleko.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kipekee kuweza kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa kibali kuingia mahali hapa, hakika nimeona ni kwa namna gani jinsi Bungeni kulivyo pazuri kiasi kwamba kweli ukiwa umeingia humu kutoka lazima utamani kutoa roho ya mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikishukuru Chama Cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wetu kipenzi kwa kuweza kuhakikisha uchaguzi huu unakuwa wa haki, lakini pia kusimamia wanyonge wote wa nchi hii waweze pia kushiriki katika maamuzi ya kutunga sheria katika nchi hii. Niweze kushukuru familia, wadau, rafiki, jamaa, viongozi wa dini na marafiki zangu wote wana maombi wote walioweza kunisaidia kuweza kufika mahali hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu nishukuru Wanasongwe, niwashukuru wanawake wa mkoa wa Songwe kwa kuweza kuwa wazalendo na kunipa nafasi ya kuweza kuingia mahali hapa, bila kura zao haikuwa rahisi, lakini waliweza kusimama imara na kunipa kura na leo niko ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujielekeza katika hotuba hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kipekee niseme

hii ni hotuba ambayo imejaa matumaini mengi kwa Watanzania. Watanzania tunayo imani kubwa na Mheshimiwa Rais kulingana na namna ambavyo ameweza kufanya kazi kubwa ndani ya miaka mitano iliyopita, aliyofanya ni mengi kila mtanzania anajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite katika kipembele cha elimu ya ufundi, nikirejea vyuo vya *VETA* na *DIT* ambavyo viko katika Mkoa wangu wa Songwe. Serikali imeweka pesa nyingi sana katika hivi vyuo vya *VETA* na *DIT*, ni vizuri vinavutia na vina mazingira mazuri sana kwa watoto wetu kuweza kupata mafunzo ya ufundi pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyopo ni kwamba, hivi vyuo havitumiki ipasavyo, havitumiki kwa kiwango kinachostahili. Ukienda katika maeneo yale idadi ya wanafunzi waliopo katika vyuo ni wachache. Kama Serikali imeweka pesa basi tutafute namna ambayo itakuwa nyepesi kwa vyuo hivi kuweza kupata wanafunzi na mchango wangu kwa Serikali, ningependa kushauri mambo yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kungekuwa na *direct enrolment* ambayo wale wanafunzi ambao wanakuwa hawajapata nafasi ya kuingia Sekondari, wapewe nafasi, wachaguliwe kama wanavyochaguliwa wale walioenda sekondari, waweze kupangiwa vyuo vya ufundi. Hii itasaidia wale wazazi wa wale watoto waone kama watoto wao nao pia wamepata *opportunity* na wakawajibika kuwapeleka watoto katika hivyo vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niombe kwa halmashauri kwa sababu tayari tunayo 10% ambayo tunatoa kama mkopo, tungetumia pesa hii kuweza kusababisha mafunzo kwa vile vikundi ambavyo vimekuwa vimeanzishwa. Kumekuwa na changamoto ya utoaji wa pesa nyingi kwa vikundi lakini wanavikundi wanashindwa kubuni miradi yenye tija, wanaishia kubuni pikipiki, wanaishia kubuni bajaji, lakini pia wanaishia kubuni kubuni miradi ya ufugaji kuku, kitu ambacho kinasababisha washindwe kufanya marejesho mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuongezea na kumalizia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umeshaisha Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, tutamalizia na Mheshimiwa Esther Maleko

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kufika mahali hapa. Pili nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniamini na zaidi pia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Busokelo kwa kunichagua kwa awamu nyingine tena ya pili, maana wanasema imani huzaa imani, nami nitawatumikia kwa moyo wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba zote mbili za Mheshimiwa Rais, ya kwanza nilishiriki 2015 na sasa ni 2020 na ndiyo maelekezo, ndiyo maagizo, ndiyo mtazamo wa nchi na hakuna ambaye anaweza kupinga hotuba hii kwamba ndiyo mwelekeo wetu wa nchi ya Tanzania kwa miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie hasa suala la ajira kwa vijana. Vijana wetu, wanafunzi wengi wanamaliza lakini ajira kwao ni changamoto. Ajira hizi zina uhusiano hasa hasa na sekta mbalimbali, si sekta tu ya kusoma, kama elimu ya Vyuo Vikuu, lakini na sekta zingine za kilimo, uvuvi, mifugo na sekta zingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na sekta ya uvuvi wa bahari Kuu; Bunge lako Tukufu mwaka 2018 lilitoa ripoti kuonyesha ni kwa namna gani ambavyo uvuvi wa Bahari Kuu hatuutumii vizuri, tunaita *blue zone*. Kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Rais ukisoma ukurasa 17, amehandika hivi: “Nchi yetu pia imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yanayofaa kwa shughuli za uvuvi ikiwemo ukanda wa pwani, maziwa, mito na mabwawa. Hali hii inafanya sekta hii kuwa na nafasi ya kutoa mchango mkubwa kwenye kukuza pato la Taifa na pia kupambana na umaskini na tatizo la ajira. Hata hivyo kwa sasa mchango wake bado ni mdogo”.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake ni nini? Bunge lako mwaka 2018 liliunda tume ambayo ilishughulikia masuala ya uvuvi wa Bahari Kuu na ikatoa ripoti kwamba hivi sana kwa miaka tisa Serikali imekusanya takriban bilioni 29.7, kwa wastani wa mwaka maana yake ni sawasawa na bilioni 3.3. Hotuba ile pamoja na ripoti ile imeonyesha Tanzania tukiutumia vizuri kina kirefu cha bahari tuliyonayo, tuna uwezo wa kukusanya mapato kwa mwaka takriban bilioni 353. Hapa mimi nakuja na taarifa muhimu na natamani Waziri wa Mifugo pamoja na Uvuvi azisikilize takwimu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kina cha Bahari ya Hindi kama tutakitumia vizuri kwanza kuna samaki wanaoitwa *tuna* ama jodari kwa wale ambao wanatoka maeneo hayo wanafahamu. Samaki huyu sasa hivi inakadiriwa kwamba kwa kina chetu cha bahari ya hindi wako samaki milioni 50. Katika hao samaki wanavuliwa na meli zinazotoka nje ya Tanzania na samaki hawa wana uwezo wa kutaga mayai mmoja mmoja milioni moja moja kila samaki huyu mmoja, tafsiri yake ukizidisha hesabu rahisi tu pale, maana yake ni milioni 50, ukizidisha kwa samaki hao milioni 50 na kwa mayai milioni moja moja unaweza ukapata zaidi ya trilioni 50 mayai ambayo yanaweza yakatagwa ama vifaranga katika huo uchumi wa bahari kuu. Tafsiri yake nyingine pia ni kwamba kwa miezi mitatu baada ya kutagwa mayai samaki huyu anakuwa na urefu na uzito wa takribani kilo 10 mpaka kilo 20 na akizidi zaidi ya miezi minne mpaka mitano anakuwa na uzito wa takriban kilo 80 na *maximum* kabisa ni kilo 95.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuchukue tu hawa ambao wanakuwa na kilo 80; sasa kilo 80 kwa samaki mmoja ambaye anauzwa kwa dola za Kimarekani 18,000 kwa *rate* ya leo ya Kitanzania ya Sh.2,320, ni sawasawa na kusema samaki mmoja ana uwezo wa kuuzwa kwa Sh.41,760,000 za kitanzania. Huu ni uchumi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukulia sasa hao samaki milioni 50 zidisha kwa samaki mmoja mwenye thamani ya Sh.41,760,000 ni zaidi ya trilioni mbili ambazo zilitakiwa ziingizwe kupitia uchumi wa bahari kuu. Hii hatuifanyi, hivyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi na Mifugo asimamie hili na nitampa taarifa zote na ripoti zote ambazo zinaonesha ni kwa kiwango gani Tanzania tunaweza kufikia trilioni mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tumezungumza hapa habari za elimu yetu ya Tanzania...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, nitaleta maandiko lakini nitachangia zaidi kwa suala la elimu ili tuone namna gani wenzetu wa South Africa wameweza kuepokana na suala hili zima la ajira kutumia mfumo wao unaoitwa *YES*. *YES* maana yake *Youth Employment Service*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Maleko.

MHE. ESTHER E. MALEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, niwashukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi kwa kuteuliwa kugombea. Zaidi niwashukuru akinamama wa Kilimanjaro kwa imani

kubwa waliyonipa, wakanipa kura za kishindo na mimi nikaweza kuwa Mbunge wao na kuja kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Pia nisiwasahau wazazi wangu, mume wangu, watoto wangu, ndugu jamaa na marafiki, kwa namna walivyonisaidia kwa maombi na kwa ushauri mpaka leo niko hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa wakati anafunga Bunge la Kumi na Moja, lakini wakati anafungua Bunge la Kumi na Mbili Novemba 13. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais ambayo imetoa dira, mwelekeo na mustakabali wa Taifa, Mheshimiwa Rais alisema katika ukurasa wa 10 kwamba wataongeza jitihada za kuwasaidia wananchi kiuchumi kwa kuwapa mikopo ambayo haina riba au yenye riba kidogo. Naomba basi niende moja kwa moja kuishauri Serikali yangu sikivu, ifanye utaratibu wa namna gani hiyo mikopo ambayo inatolewa na halmashauri 4% kwa wanawake, 4% kwa vijana na 2% kwa wenye walemavu, iangalie basi ni namna gani mikopo hiyo inaweza kuongezwa. Zaidi ya hapo iangaliwe ni namna gani mikopo hiyo haitatolewa kwa masharti ya kupewa kwa vikundi, ikatolewe kwa mtu mmoja mmoja kwa sababu ni wanawake wengi ambao wanahitaji mikopo hiyo lakini wakati mwingine wanakosa kwa sababu ya masharti ambayo yamewekwa kwamba ni lazima mkakope kwa vikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu najua Serikali yangu ni sikivu naamini itazingatia suala hilo na kwasababu akinamama wa Kilimanjaro wengi ni wakulima, lakini wengi ni wafanyabiashara wakipatiwa fursa hiyo adhimu wataweza kukwamua familia zao. Kama unavyofahamu mwanamke ndiye anayeinua uchumi wa familia, hivyo mwanamke akiguswa familia itaguswa lakini pia na Taifa litakuwa limeguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiache kulisema hili pia, kule kwetu Kilimanjaro akinamama wengi wanauza ndizi lakini ndizi haina bei kabisa inapopelekwa sokoni. Mwanamke

anapopeleka ndizi sokoni anaenda kuiuza kwa shilingi elfu moja na wakati mwingine wanunuzi wanamkopa, anaweza kukaa na hiyo ndizi ikaiva kwa hiyo hivyo inabidi aitoe kwa wale wanunuzi ambao wao wakienda kuiuza wanaenda kuiuza kwa zaidi ya shilingi elfu ishirini na tano. Basi tuone ni namna gani tunaweza kuwapatia akinamama hawa elimu ya namna gani wanaweza kuchakata ndizi hizo na wakaweza kupata kipato zaidi na siyo kuonewa kwa namna ambavyo wanaonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya hewa ya Kilimanjaro tunaweza kulima kilimo cha mbogamboga, kilimo cha bustani. Naiomba Serikali yangu Tukufu iweze kuongeza bajeti kwenye Wizara ya Kilimo ili sasa wanawake hawa ambao ni wakulima wapate elimu bora juu ya kilimo hicho wanacholima kwenye matunda, kwenye mbogamboga na tukaende kuongeza pato la Taifa. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais amesema leo Tanzania iko nafasi ya 20 kidunia kwa kuzalisha mazao haya, lakini imeingiza zaidi ya dola milioni 412 kwa mwaka 2015; mwaka 2018/2019 imeingiza zaidi ya dola milioni 779. Je, hatuoni...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa.

MHE. ESTHER E. MALEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. Naamini itasaidia upande wa Serikali wakati wanatayarisha mipango yao ya kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi watakuwa wakitumia michango yenu muhimu kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa na Wabunge kadhaa ambao watachangia mchana nitaje baadhi yao, Mheshimiwa Mariam Omar Said, Mheshimiwa Profesa Patrick

Ndakidemi, Mheshimiwa Rehema Migila, Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamwo, Mheshimiwa Frank Mtega, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Anthony Mavunde na wengine tutaendelea kuwataja kadri michango itakavyokuwa inatolewa.

Baada ya kusema hayo, nitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

(Saa 7.04 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge liliudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Maryam Omar Said atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo ajiandae.

MHE. MARYAM OMAR SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza katika kipindi hiki cha pili cha leo cha kujadili hoja ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu, Bunge la Kumi na Mbili, nichukue fursa hii kutoa pongezi na shukrani zangu za dhati kwa makundi matatu ambayo yalishiriki katika kuhakikisha leo Maryam nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu, Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za pekee ziende kwa familia yangu kwa jumla. Pia nikishukuru Chama cha Wananchi CUF kupitia Mwenyekiti wake shupavu, Mheshimiwa Prof. Ibrahim Lipumba kwa kuweza kunisimamisha nikawa mgombe katika Jimbo la Pandani kule Pemba. Pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa wananchi wangu wa Jimbo la Pandani kwa kunipa ushindi wa asilimia 56.6 ambazo zimenifanya leo hii nasimama kifua mbele ndani ya Jimbo huku nikijidai kuwa ni mwanamke pekee katika majimbo 18 ya Pemba niliyepata nafasi ya jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, naomba nichangie hoja ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nikisimama zaidi katika miundombinu ya viwanja vya ndege pamoja na bandari kwa upande wa Pemba. Nilifurahi sana pale Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliposema atashirikiana na Rais wetu wa Zanzibar bega kwa bega katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo. Naamini tumepata majembe mawili, tunamuamini Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi kwa sababu amelelewa na Rais wetu ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunaamini yale yaliyoko Tanzania Bara basi na Tanzania Visiwani yatafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa kumtaka Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli aongeze kasi zaidi katika kushirikiana na Rais wetu wa Zanzibar katika suala la miundombinu hususan viwanja vya ndege pamoja na bandari, Wapemba wanalalamika, wananung'unika. Tufahamu kwamba Pemba imo katika sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini tupo nyuma. Leo hii nikitaka kusafiri nikiwa Pemba basi nianze kuweka *booking* ya *ticket* ya ndege siku mbili kabla nikikosa hapo ndege ya asubuhi ama jioni naikosa. Wapemba wanaomba pia ndege ya *Air Tanzania* kama jina lilivyo *Air Tanzania* kiwanja cha ndege kiboreshwe na iweze kufika Pemba pia, wana ndoto, wanaota kila siku ndege ya *Air Tanzania* ipo Pemba lakini bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa upande wa bandari tumechoka wananchi wa Pemba kutumia saa kumi na mbili tukiwa ndani ya Bahari tu tunaitafuta Unguja. Tunahitaji tuboreshewe miundombinu ya bahari kwa kupata boti za kisasa kwa hali yoyote ile kama ambavyo Unguja na Bara ama Unguja na Dar es Salaam inaunganishwa kwa saa kadhaa tu unatoka Unguja unafika Dar es Salaam. Ni ndoto zetu na sisi Wapemba, tunataka tutumie saa chache kutoka Pemba kuja Unguja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais tunakuamini, ni jemedari mzuri, unaweza kuleta maendeleo

kwa kiasi fulani lakini tunaomba umshauri vizuri Rais wetu wa Zanzibar hususan atuangalie kwa jicho la hurumu Pemba kwa miundombinu ya usafiri. Wapemba bado tuko nyuma, wananchi wanalalamika na ndiyo maana ukakuta kwamba siasa kali inahamia Pemba, kimaendeleo bado tupo nyuma. Tunahitaji kuangaliwa kwa jicho la tatu wananchi wa Pemba mbali na mawili, tuangaliwe kwa jicho la tatu, tuko nyuma katika sekta zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Maryam, Mbunge pekee wa CUF kutoka Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Rehema Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi ajiandae.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi jioni ya leo kuchangia hotuba ya Rais. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuiona siku leo. Pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwepo hapa leo katika Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kukishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kunikubali na kunipokea na kuwa mwanacha wa Chama cha Mapinduzi kwani awali nilikuwa upande ule wa pili. Hivyo, nikishukuru sana Chama cha Mapinduzi kwa mapenzi yake mema kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wa Jimbo la Ulyankulu ambao walikuwa na imani na mimi wakiamini kabisa ni mwakilishi wao mzuri. Naamini nina deni kubwa kwao na nitahakikisha nawatendea kulingana na uwezo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais kama ifuatavyo. Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake amesisitiza jambo kubwa sana kuhusu amani lakini hii amani kwa baadhi ya wananchi wa Jimbo langu hususan kata zile tatu ambazo zilikuwa zikikaliwa na wakimbizi amani inaweza ikatoweka endapo hatua stahiki hazitachukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa mwaka 2015 wakiwa wakimbizi walipewa uraia wa Tanzania lakini bado wanakuwa *treated* kama wakimbizi. Hakuna jambo lolote la maana linalofanyika kule, shughuli za kimaendeleo hazifanyika lakini bado wanachangia shughuli kubwa za ulipaji wa kodi, wanateseka kwa kiasi kikubwa. Niiombe sasa Serikali kupitia Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Mambo ya Ndani na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria waweze kuiangalia hii Sheria Na.9 ya Wakimbizi ambayo inawabana sana hawa watu ili waweze kufanya shughuli zao kwa amani na waishi kama wananchi wengine wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa jimbo hili hawawezi kufanya shughuli zozote, hivi sasa hata kujenga nyumba pale hawajengi, hata choo kikidondoka pale ni lazima wapate kibali kutoka kwa mkuu wa makazi ndiyo waweze kujenga. Tunaiona Serikali inafanya jitahada sana kuhakikisha inapeleka maendeleo pale lakini bado sheria ile inazidi kukwamisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetupelekea shilingi milioni 600 kwa ajili ya kujenga nyumba kwenye Chuo cha Ufundi VETA, lakini sheria ile imebana zimekataliwa kujengwa. Pia shughuli za maendeleo kama kujenga madarasa na miundombinu mingine zimekataliwa. Hivyo nawaomba Mawaziri wanaohusika na suala hili mtupe mwongozo leo ili hao wananchi wetu wapate nafuu na wajue hatima yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwenye nishati ya umeme. REA huko vijijini kwetu imekuwa ni mkombozi mkubwa, sasa hivi vijiji vingi umeme unawaka lakini

kuwaka kwa umeme huko bado kuna changamoto. Umeme huu umepita kwenye vijiji tu haujaenda kwenye vitongoji. Hivi navyoongea baadhi ya kata zangu kama mbili Silambo na Kata ya Uyowa hazijapata umeme kabisa, hivyo naomba zipate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikibakia hapo hapo kwenye umeme wa *REA* suala la nguzo imekuwa ni tatizo, tunauziwa nguzo kwa kiasi cha shilingi laki tatu na zaidi. Mimi mwenyewe ni muhanga wa kuuziwa nguzo kwenye eneo langu. Tunaambiwa kwamba umeme wa *REA* ni Sh.27,000 lakini tunapohitaji kuingiziwa umeme, nyumba ikiwa umbali kuanzia mita mia moja na kuendelea mwananchi unahitajika ulipie nguzo ya umeme. Hii hali haikubaliki na wananchi walio wengi ni maskini hawawezi ku-*afford* kununua nguzo hizi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aweze kuliingilia kati suala hili na ikiwezekana kama ni suala la kununua nguzo basi itolewe bei elekezi ambayo ni rafiki kwa hao wananchi ili waweze kumudu gharama hizi na kuingiza umeme kwenye nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni afya. Jimbo langu la Ulyankulu lina kata 15 lakini vituo vya afya vilivyoko na vinavyofanya kazi ni kituo kimoja tu cha Barabara ya 10, hivyo msongamano ni mkubwa sana kutoka sehemu mbalimbali ambapo watumishi wa ile hospitali wanazidiwa. Niombe sasa bajeti ipangwe ili vituo vingine vya afya kama Kituo cha Mwongozo, Uyowa na Kashishi na vyenyewe viwekwe kwenye mpango ili vipatiwe pesa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi, Mheshimiwa Frank Mtega ajiandae.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyo Wabunge wenzangu kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge hili, naomba

nichukue fursa hii kukishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kunipatia nafasi ya kuwa mwakilishi wa Jimbo la Kibaha Vijijini. Kwa namna ya peke kabisa niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini kumpatia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kura za kutosha, kunipatia mimi Mbunge wa Chama cha Mapinduzi kura za kutosha na kuwapa Waheshimiwa Madiwani wa kata mbalimbali katika jimbo langu kura za kutosha. Nawaahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kwao na nitajitahidi kuwatumikia kwa kadri ya uwezo Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda kuwa mchache, naomba nijielekeze kwenye hoja chache ambazo nimezisoma katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa tarehe 13 Novemba, 2021 wakati anafungua Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, najielekeza kwenye ukurasa wa 13 wa hotuba hiyo. Katika hotuba hiyo Mheshimiwa Rais alijaribu kuonesha hisia zake na kuonesha ni namna gani na sekta zipi anaamini kwamba zitalifikisha Taifa hili kwenye uchumi mkubwa na kuwaondoa Watanzania kwenye umaskini na kuwafanya wawe wanaishi maisha mazuri na salama kabisa.

Katika maeneo hayo, naomba nichangie kwenye sekta mbili; kilimo na ufugaji. Hawa wakulima ambao tunawazungumza kwenye Bunge hili, ukiangalia kwa haraka haraka katika Wabunge wote tuliopo hapa tunao wakulima wa kawaida kabisa na wafugaji wadogo kabisa ambao wako kwenye mazingira ya vijijini kabisa ambao ndiyo tunatakiwa tuwaelekezee nguvu zetu kuhakikisha kwamba wanafuga na walima katika mazingira yaliyo bora.

Naomba nieleze kwamba katika jimbo langu na nafikiri na kwenye majimbo mengine, makundi haya mawili ni rafiki lakini ndiyo makundi ambayo yanagombana kila siku. Ukikaa unasikia mkulima amevunjika mkono kapigwa bakora na mfugaji, ukikaa mfugaji kaumizwa yaani ni vita siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri kidogo katika suala hili, kwa kuwa hawa ni wakulima na wafugaji ambao tunawategemea kwa ajili ya kukuza kilimo na mifugo yao, nafikiri tungetumia maeneo yetu yaliyotunzwa kuwaondoa wafugaji walio katikati ya vijiji ambavyo vinalima kwenda kukaa kwenye maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya shughuli za ufugaji na wakasaidiwa mbinu mbalimbali wakafuga vizuri na hatimaye mifugo hiyo ikawasaidia. Kwa mfano, kule kwetu Kibaha Vijijini, tunayo maeneo ya Kwale yaliyokuwa yanamilikiwa na watu wa kilimo, tunayo maeneo ya MARCO ni msitu mkubwa sana katika Jimbo la Chalinze, ni vizuri wafugaji wa maeneo yale ya karibu wangehamishiwa kwenye maeneo yale wakawekewa miundombinu ili waweze kufuga vizuri na waondoke kukaa katikati ya wakulima waachwe wale wakulima wadogo nao wanaohangaika kulima kilimo kisichokuwa na tija angalau waambulie kupata chakula kidogo ambacho wanakilima kwa kutumia nguvu zao kwa jembe la mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Sika, sambamba na hilo, najielekeza katika ukurasa wa 19 ambapo Mheshimiwa Rais amejaribu pia kuonyesha ili uweze kukuza uchumi wa nchi hii au kuwaendeleza Watanzania hawa ni lazima tuwekeze nguvu kwenye viwanda. Nashukuru sana kwamba Mkoa wa Pwani unatekeleza na unatambuliwa kwamba umefanya kazi kubwa ya kujenga viwanda vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Serikali ijaribu kulifikiria jambo moja, wanafahamu matatizo yanayowakuta watumishi kwenye viwanda vile? Wanajua mishahara ya wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye viwanda hivi ambavyo wawekezaji wetu wamewekeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ingewezekana hata kwa kuanzia na Mkoa wa Pwani watengeneze timu maalum wapite kule, waangalie mishahara ya wafanyakazi hawa ambayo wanalipwa kwenye viwanda vile vya uwekezaji. Pia waangalie mazingira wanayoyafanyia kazi, wana mazingira magumu sana kiasi ambacho huwezi kuamini hali ile inaweza ikatokea kwa

wafanyakazi wale ambao wako kwenye maeneo yale.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo lipo jambo lingine la ujenzi wa miundombinu. Nashukuru kwenye Mkoa wetu wa Pwani, kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2025 inatajwa barabara mkakati na nzuri kabisa inayoweza kwenda kutoa huduma nzuri kabisa inayoanzia Bagamoyo pale Makofia, inapita Mlandizi, inakwenda kwa kaka yangu Mheshimiwa Jafo, mpaka inatokea Kimara Misale huko.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri barabara hii ishughulikiwe kwa haraka zaidi. Wananchi wamekaa kwa muda mrefu wakisubiri matengenezo barabara hii, naiomba Serikali ifike kwenye maeneo yale ikiwezekana iwaeleze wale ambao wanaathirika na mradi huu mara utakapokuwa unaanza utekelezaji wake wawape taarifa sahihi, bado wananchi hawaelewi na wanashangaa. Pamoja na kwamba tumeeleza vya kutosha kwenye Ilani lakini bado wanapata shida ya kuamini kwa sababu ni barabara iliyotajwa kwenye Ilani hii na hata ile iliyopita. Niiombe Serikali kipindi ambacho tunajiandaa kwenda kufanya utekelezaji wa barabara hii na nina imani kwamba kwa uwezo wa Serikali iliyopo na kwa jinsi inavyojipanga kutekeleza miradi hii itakwenda kuitekeleza, basi itenge muda sasa iende ikazungumze na wananchi wa maeneo yanayoanzia Bagamoyo na kuendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi atafuatiwa na Mheshimiwa Frank Mtega, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii. Kwa kuwa ni mara yangu kwanza kuchangia katika Bunge lako Tukufu, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kunipa

nafasi ya kuongea hapa nikiwa mwakilishi wa watu wa Jimbo la Moshi Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya. Nataka niwashukuru watu wengi ambao wamenisaidia nikawa Mbunge, nianze kuishukuru familia yangu, namshukuru sana mama pamoja na watoto, nakishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi kwa kunitewa nigombe ubunge, nawashukuru wapiga kura wa Moshi Vijijini kata zote 16 walinipa kura za kutosha kuhakikisha nimeshinda kwa kishindo na Mheshimiwa Rais na Madiwani wote 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambayo amefanya toka mwaka 2015 tangu achaguliwe kuwa Rais na kwa hutoba nzuri sana ya kulizindua Bunge hili. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais aliongea mambo mengi makubwa ambayo sisi kama Wabunge endapo tutayazingatia na kama tutaisimamia Serikali vizuri nina hakika tutaacha alama kama moja ya Mabunge bora katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye mchango, nitachangia eneo la kilimo mifugo na uvuvi na nafasi ikipatikana nitaongelea miundombinu na sekta ya afya. Tukubaliane Wabunge wenzangu wote waliopo huku ni matunda ya watoto wa wakulima, kama siyo mtoto wa mkulima ni mtoto wa mfugaji, kama siyo mtoto wa mfugaji ni mtoto wa mvuvi. Tukubaliane tu Rais ana nia nzuri ya kuhakikisha kwamba katika miaka mitano ijayo anaboresha sekta hii ambayo nimeitaja ambapo sote sisi ndiyo tumetoka huko. Niombe tu kwamba ni wakati wetu sisi kama Wabunge tumuunge mkono Rais, tuhakikishe kwamba tunarudi kule nyumbani tulikotoka kwa kuziunga mkono hizi sekta ili nao waweze kuongeza kipato na kuchangia katika pato la Taifa na katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu sekta hii ina changamoto nyingi sana, changamoto mojawapo ni

kwamba wakulima wengi wafugaji na wavuvi ni wazee, vijana wetu ambao ndiyo wanategemewa warithi hii kazi hawana *interest* na hizi kazi za kilimo ama ufugaji ama uvuvi. Niishauri Serikali ikiwezekana tuchukue hatua muhimu kabisa ya kuhakikisha tunawashawishi vijana wetu ili waweze kuwa wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa kwanza wa Serikali ni kwa Wizara ya Elimu ikiwezekana wabadilishe zile shule zote za kata ambazo ziko karibu na vijijini zifundishe somo la kilimo na Vyuo vya *MATI, LITA, VETA*, Chuo Kikuu cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Mandela ambacho vinafundisha kilimo kwenye mitaala yao waweke *component* ya ubunifu na ujasiriamali. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunawaandaa hawa vijana ili waje wawe waajiriwa kwenye hii sekta ya mifugo kilimo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme tu kwa kuwa Rais amedhamiria kusaidia hii sekta ya uzalishaji ambayo ni kilimo, mifugo na uvuvi, nishauri Serikali iweke pesa za kutosha kwenye utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi ili waweze kuzalisha mbegu za kutosha na teknolojia ambazo zitatumika kuongeza tija katika kilimo. Tukishazalisha mbegu bora na tukiziwezesha zile taasisi zinazozalisha mbegu kama vile *ASA* kama vile *NIKE* pale Arusha watazalisha mbegu bora za kilimo za mifugo na zamaki ambazo zitatumika kuongeza tija na kuwaongezea wakulima wetu kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine muhimu ni eneo la umwagiliaji; Serikali ina nia nzuri ya kuboresha sekta ya umwagiliaji na tukitaka tuzalishe vizuri naishauri Serikali pia iiongezee Wizara ya Kilimo pesa za kutosha ili sekta ya umwagiliaji iweze kupata mshiko. Tukishapata maji ya kutosha nina uhakika tunaweza tukalima mbogamboga. Mbogamboga ni eneo ambalo linaweza likasaidia sana nchi yetu nitatoa mifano na *figure* kidogo. Ukilima nyanya inayoitwa *tanya* kwa *space* ya 60 kwa 60 unapata miche 11,111 kwa hekari moja na mche mmoja wa nyanya unauzwa Sh.1,000, kilo mbili unaweza ukauza kwa Sh.1,000 na ukiuza kwa hekari moja utapata Sh.22,000,000. Ukiuza kwa Sh.500

unaweza ukapata Sh.11,000,000; ukiuza kwa Sh.250 kwa kilo hiyz nyanya unaweza kupata zaidi ya milioni tano. Sasa...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwa-*support* wakulima wenzetu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ili tuwajiri vijana wakulima na watu wengine. Nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Frank Mtega atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi na Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ajiandae.

Mheshimiwa Frank Mtega, hayupo, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, atafuatiwa na Mheshimiwa Anthony Mavunde na Mheshimiwa Dkt. Alice Kajage ajiandae.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya iliyo bora, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii leo ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu nianze kwa kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Msalala kwa kunipatia imani kubwa hii ya kuweza kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, niseme sisi kama Wanajimbo la Msalala, hotuba hii imeleta mapinduzi makubwa sana katika Jimbo langu la Msalala. Niliarifu Bunge lako Tukufu hili kwenye ukurasa wa 37, lakini pia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ya 2020, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika Jimbo la Msalala ameweza kutupatia miradi mikubwa kabisa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametupatia mradi mkubwa wenye zaidi ya bilioni 13 ambao ni mradi wa maji unaotoka Magu kuja Ilogi. Hata hivyo, hajaishia hapo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ametupatia mradi mkubwa kabisa wa maji unaotoka Kagongwa kwenda Isaka unaogharimu kiasi cha bilioni 23. Pia hajaishia hapo, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ameweza kutupatia mradi mwingine wa maji ambao unatoka Nduku Mtobo kwenda Busangi, ambao unagharimu kiasi cha shilingi bilioni nne nani kama Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli tumeona azma yake ya kuunganisha mikoa kwa mikoa, wilaya kwa wilaya. Katika Jimbo langu la Msalala, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ameweza kutupatia barabara mbili zenye kiwango cha Lami, barabara hizi ni barabara inayotoka Solwa kuja kupita Kata ya Ngaya na Kata ya Bulinge kuja Kahama lakini pia ametupatia barabara nyingine inayotoka Bulyanhulu kuja Segese mpaka Kahama. Naiomba Wizara ya Ujenzi iweze kuona namna gani inaweza kuanza utekelezaji wa barabara hizi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala nzima la afya, niseme tu mbele yako Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa sisi Wanabulyanhulu alianza kupambana juu ya kupitia mikataba upya ya madini na mikataba hiyo sisi kama Wanamsalala tumeweza kunufaika pakubwa sana na mikataba hii. Leo hii ninapozungumza tunapokea fedha za *CSR*. Nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini aweze kufanya ziara na kuona namna gani sasa Wanamsalala tunaweza kunufaika na fedha hizi za *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ucheleweshwaji wa miradi mbalimbali inayopangwa kwa ajili ya kutekelezwa na watu hawa wa mgodi zinazotolewa na fedha za *CSR*. Nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Doto aweze kufika katika Jimbo langu la Msalala ili tuweze kufanya kikao na watu hawa tuone namna gani wanaweza kutekeleza miradi hii ya *CSR* ili iweze kuleta tija kwa wananchi wa Jimbo la Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imeweza kutufanya Jimbo la Msalala kuhama kutoka uchumi wa chini na kuhamia uchumi wa kati. Ninavyozungumza hapa tuna vituo vinne vya afya katika Jimbo langu la Msalala, lakini pia tunaenda kujenga kituo kingine kwa fedha zetu za ndani za jimbo, tunaenda kujenga kituo cha afya katika Kata ya Isaka. Niiombe TAMISEMI na Waziri Mheshimiwa Jafo, kaka yangu aweze kutusaidia kutupatia vifaa tiba ili kituo cha afya kinachokamilika kiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu sio hilo tu, lakini tumekuwa na uhaba wa watumishi katika sekta ya afya katika Jimbo la Msalala; nimwombe Mheshimiwa Jafo aweze kutuangalia kwa jicho la huruma Wanamsalala, tuna uhaba wa Walimu pia, naomba ndugu yangu atusaidie katika suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya kauli yake ya kuhakikisha kwamba tunaenda kuongeza madarasa katika nchi nzima. Katika Jimbo langu la Msalala napenda nimhakikishie Mheshimiwa Waziri Mkuu tulilipokea wazo lake hilo na maagizo yake hayo kwa kutekeleza ujenzi wa madarasa na tumeweza kuongeza madarasa katika kila kata mawili. nami kama Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie Mheshimiwa Waziri Mkuu nilitoa lori la *cement* kuhakikisha kwamba naunga juhudi za ujenzi wa madarasa hayo. Kwa sasa tunavyozungumza tuko katika hatua nzuri na baadhi ya shule tayari madarasa hayo yameanza kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la ajira..

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umeisha Mheshimiwa.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, atafuatiwa na Dkt. Alice Kaijage na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

MHE. ANTHONY P. MAVUNDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyeniwezesha kusimama siku ya leo. La pili, nakishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi, chini ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuiteua kupeperusha bendera ya CCM katika Jimbo la Dodoma Mjini na Wanadodoma wakaniamini na kunichagua tena. Jimbo hili watu wanakwenda msimu mmoja mmoja, mimi nimerudia namshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma hotuba ya Rais, Mheshimiwa Magufuli ya mwaka 2015 na mwaka 2020, inakupa dira, inakupa dhamira na upendo mkubwa ambao Rais wetu anao katika kuipeleka Tanzania kwenye maendeleo. Ni dhahiri kabisa kupitia hotuba hizi, mtu yoyote anaweza akaona Tanzania ilipotoka na inapokwenda, tunakwenda pazuri sana, tumuunge mkono Rais wetu mpendwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza maeneo mawili ya kipaumbele ambayo Mheshimiwa Rais ameyagusia katika hotuba. La kwanza ni la uunganishaji wa Mifuko ya Uwezeshwaji Wananchi Kiuchumi. Hoja hii ni muhimu sana katika kuwasaidia wajasiriamali wa Tanzania kwa sababu Mifuko hii ilikuwa ni mingi, kila mmoja anatowa mikopo na ruzuku kwa wakati wake, lakini kwa kuunganishwa Mifuko hii maana yake ni kwamba itatoa wigo mkubwa zaidi kwa watu wengi kuweza kupata fursa ya mikopo hii. Imani yangu ni kwamba katika zile ajira milioni nane, ni rahisi sana kuzifikia kupitia katika Mifuko hii na naamini kabisa kwamba, Mifuko hii ikiunganishwa itasaidia pia katika mfumo wa ukopeshwaji, badala ya vikundi iende kwa mtu mmoja mmoja ili Watanzania wengi zaidi waweze kupata fursa hii ya mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nashauri Serikali kwamba Mifuko hii iende sambamba na program za kukuza ujuzi. Ofisi ya Waziri Mkuu wana programu nzuri sana ya kukuza ujuzi kwa vijana ambayo inaitwa *RPL*. *RPL* ni *Recognition of Prior Learning*, ni mfumo wa urasimishaji ujuzi kwa vijana wenye ujuzi ambao hawajapitia mfumo rasmi na mafunzo ya ufundi yaani wako vijana mtaani wanajua kuchonga vitanda, wanajua kuchomelea, hajawahi kusoma *VETA*, hajawahi kusoma *Don Bosco*, Serikali inachokifanya inakwenda kuwajengea uwezo na kuwapa uwezo na kuwapa vyeti vya kuwatambua. Programu hii iendelee na naamini itawagusa vijana wengi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri pamoja na kuunganisha hii Mifuko tusimamie pia ile program ya *ODOP* (*One District One Product*) itatusaidia sana kwenye kuimarisha na kukuza shughuli za vijana na akinamama na watu wenye ulemavu katika maeneo tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili na la mwisho, mimi ni Mbunge wa Dodoma Mjini na sisi tumepata heshima ya Dodoma kuwa Makao Makuu. Mwanzoni wakati wakati inasemwa watu walijua ni maneno ya utani, lakini Rais Magufuli amefanya kwa vitendo. Nachukua fursa hii pia kulishukuru sana Bunge letu kwa kutunga Sheria Maalum ya Dodoma *Capital City Declaration Act* ya mwaka 2018 ambayo haiwezi kubadilisha maamuzi ya Makao Makuu mpaka pale itakapoletwa tena Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia maendeleo makubwa ndani ya muda mfupi, Dodoma imechangamka, uchumi umeongezeka, maisha ya watu yamebadilika. Tunategemea mradi mkubwa wa uwanja mkubwa wa ndege wa Msalato, lakini barabara za mzunguko ambao zitaondoa msongamano katika Jiji la Dodoma. Hii ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Rais Magufuli katika eneo la Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, mwaka 1989 ilitungwa sheria ya Dodoma *Special Investment Area* ambayo ilikuwa inatoa unafuu kwa wawekezaji wanaokuja

kuwekeza Dodoma. Naomba sheria hii ipewe *extension* kwa sababu ime-*expire* mwaka 2019 ili kila mtu anayekuja kuwekeza Dodoma, apate unafuu na Dodoma iendelee kujengeka. Naamini kupitia sheria hii Dodoma itakua zaidi na zaidi na ile azma ya Mheshimiwa Rais kuwa Dodoma kuwa ni kati ya majiji bora Afrika itatimia kupitia sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, naunga mkono hoja na nashukuru sana kwa nafasi, tuendelee kumsaidia Rais wetu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Salum Musa Omar ajiandae.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa name ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kufika kwenye Bunge hili leo. Pia naomba nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi, Jumuiya ya Wanawake pamoja na wanake wema sana wa Mkoa wa Pwani ambao waliridhia kunisindikiza na kunifanya niweze kuwa Mbunge wao kuwawakilisha. Navishukuru Vyama vya Wafanyakazi; pia nashukuru familia yangu, Mama yangu, ndugu, jamaa na marafiki kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijielekeza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, nimesoma hotuba zote za 2015 na 2020; Mheshimiwa Rais ameonyesha nia njema na dira katika kuiendeleza Tanzania, lakini ameonyesha dhamira ya wazi kwenye kulinda amani yetu na pia kuudumisha Muungano wetu. Nina sababu zote za kushukuru Vyombo vya Usalama na Ulinzi ambavyo kwa pamoja na wananchi wenye nia njema wameweza kushirikiana kuendelea kulinda amani ya nchi yetu. Wanastahili pongezi kubwa sana vyombo vya Ulinzi na Usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, tumeona suala nzima la huduma za jamii katika ujumla wake,

wenzangu wamezungumzia, lakini naomba nijikite kwenye suala la afya. Ukiangalia kwenye Ilani na hotuba yake, Mheshimiwa Rais ameeleza nia njema kabisa ya kuboresha huduma za kibigwa na pia kuongeza miundombinu pamoja na vifaa vya kutosha vya kisasa. Siyo suala la kupinga kabisa lipo wazi kwa jinsi ambavyo huduma za kibigwa zimeimarika. Ukiangalia taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, halina ubishi wote tunafahamu. Muhimbili hiyo hiyo mpaka sasa wanapandikiza figo, wanaweka masikio, *cochlear implant*, wanafungua kichwa ubongo bila kufungua fuvu. Kwa hiyo, huduma nyingi zimeimarishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema hayo kwa sababu nina jambo moja la kulisema. Katika suala nzima la magonjwa la kiharusi (*stroke*) imekuwa ni tatizo ambalo ni kubwa sana kwa siku *admission* au wanalazwa wagonjwa watano mpaka sita Muhimbili, acha Mlonganzila au hospitali zingine za rufaa. Kwa hiyo nina wazo moja, tunaomba taasisi ya *Stroke* ianzishwe; wagonjwa wale wanakaa muda mrefu, wanachangwanywa na wagonjwa wengine, *immunity* yao ni ndogo. Kwa hiyo kuna uwezekano kama wakianzisha *stroke center* kama wenzetu South Africa na Egypt wanafanya pawe na *stroke nurse*, pawe na wataalam, kwa hiyo itakuwa ni kitengo kinachojitegemea, kitafanya *outreach*, elimu kwa jamii pamoja na kuwa na Manesi katika hospitali zingine ambazo ni kubwa ili kupunguza tatizo la *stroke* ambayo sisi wote ni wahanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Hospitali yetu ya Mirembe. Hii ni hospitali ya muda mrefu, ina miaka 93, imeanzishwa mwaka 1927. Hii hospitali inachukua Watanzania wa kawaida na sisi ni wahanga hatuwezi kukwepa kuingia pale siku moja. Hii hospitali ni ya muda mrefu ina miundombinu chakavu, mikongwe, lakini inasababisha kupata taswira nzima ya huduma njema inayotolewa pale. Pili ipo katika Makao Makuu ya Nchi. Mazingira mazuri yanawatia moyo wafanyakazi kufanya kazi kwa bidii na Watanzania wale ingawa afya yao ina matatizo lakini wanastahili kukaa kwenye mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, *bed state* kwa siku wagonjwa hawapungui mia tano, kuna Isanga, kuna Mirembe *Proper* na vituo vingine vya kutolea dawa za kulevya, vyote hivyo viko chini ya Mirembe. Naomba sasa ufike wakati bajeti yao iongezwe, ikiwezekana sasa iwe taasisi, kwa mwezi wanatumia zaidi ya milioni 280, kwa maana ya huduma za kila siku kwenye taasisi ile. Naomba iangaliwe taasisi ya Mirembe kwa sababu sisi sote ni wahanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mussa Omar na Mheshimiwa Katani Katani ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Rais. Kama ilivyo ada na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza naongea kwenye Bunge hili la Kumi na Mbili, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, nitoe shukurani kwa wapiga kura wangu wa Liwale, nitoe shukurani kwa Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniwezesha kuwepo hapa sasa hivi na kulitumikia Taifa na nawaahidi utumishi uliotukuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Rais naomba nijikite katika sehemu moja au mbili; sehemu ya kwanza kabisa nizungumzie suala la kilimo. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Rais amedhamiria kufufua kilimo, kwa maana ya kwamba kwenda na kilimo cha kisasa na kufanya mapinduzi ya kilimo. Hata hivyo, hatuwezi kwenda na mapinduzi ya kilimo kama hatujawekeza kwenye utafiti. Ni lazima tuhakikishe tunafufua au tunaimarisha vyo vyetu vya utafiti, vile vile kujikita kwenye bajeti kwa kuongeza zaidi katika sehemu hiyo ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri kwenye zao letu la korosho mwaka juzi kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Liwale, kulikuwa na ugonjwa wa mikorosho, ilikuwa

inanyauka mizima mizima, ilikuwa inanyauka mpaka inafikia kukauka. Kwenye msimu wa mwaka huu, korosho zile zimezaa vizuri, lakini ukibangua ile korosho yenyewe tayari ndani unakuta imeharibika, kwa maana korosho zimeharibika, kitendo ambacho kimeilazimu Wilaya ya Liwale kuuza korosho zake kwa kiwango kikubwa kwenye *grade* ya pili. Jjambo hili naiomba Serikali kupitia Waziri wa Kilimo ihakikishe tunapeleka wataalam kwenye mashamba haya ya kilimo ili tuweze kugundua tatizo ni nini. Hii ni kwenye upande huo wa utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake alizungumzia suala la miundombinu. Ni kweli kabisa jambo la miundombinu huwezi kutenganisha na maendeleo ya watu kama hatujawahi kuunganisha miundombinu. Hapa naunganisha na Sera ya Taifa letu ya kuunganisha mikoa yetu kwa barabara za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niiambie Serikali Mkoa wa Lindi bado haujaunganishwa na Mkoa wa Morogoro kwa barabara za lami. Mkoa wa Lindi tunayo barabara moja tu inaitwa Kibiti – Lindi ambayo ni kama *trunk road*. Hata hivyo, barabara hii isiposaidiwa na *regional roads* hatutapata tija yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naizungumzia barabara inayotoka Nachingwea kwenda Liwale, Nachingwea kwenda Masasi, Ruangwa kwenda Nachingwea, Ruangwa kwenda Kilwa, barabara hizi zisipofunguliwa bado manufaa ya hii *trunk road* ya Kibiti – Lindi hayataonekana. Naiomba Serikali, pamoja na kwamba tumejikita kwenye kuunganisha mikoa, hizi *regional roads* tunaweza kuziita *feeder roads*, ndizo barabara zinazowezesha mazao ya wakulima kufika kwenye masoko kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na sera ya kuunganisha mikoa Mkoa wa Lindi wauangalie kwa jicho la huruma kwa sababu ni mkoa pekee ambao una barabara moja tu yenye lami ambayo hiyo ni *trunk road*, *regional roads* zote ni za vumbi. Naomba sana

Mheshimiwa Waziri au Serikali kwa ujumla tuifikirie barabara ya Nangurukuru – Liwale. Barabara hii ni ya kiuchumi na siyo ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande huohuo wa miundombinu, tunalo tatizo kubwa sana upande wa wakandarasi. Tunatekeleza miradi mikubwa sana lakini wakandarasi wanachelewa kulipwa. Jambo hili linafanya miradi yetu mingi itumie hela nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, barabara inaweza kujengwa labda kwa shilingi bilioni 200, lakini kwa sababu tu mkandarasi amechelewa kulipwa, barabara imeisha ina miaka mitatu, minne mkandarasi hajalipwa, utakuta ile barabara badala ya kujengwa kilometa moja kwa bilioni 1.2 tunajenga mpaka bilioni 1.8 au bilioni 2. Hii yote ni kwa sababu tunachelewa kuwalipa wakandarasi. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuhakikisha kwamba wale wakandarasi ambao wanamaliza miradi kwa wakati basi miradi hiyo iishe kwa wakati na wakandarasi waweze kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, hayo tu mawili yananitoshia kwa mchango wangu kwenye hotuba hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salim Mussa Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Katani, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana ajiandae. Mheshimiwa Katani Katani.

WABUNGE FULANI: Hayupo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana.

WABUNGE FULANI: Hayupo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taska Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dorothy George Kilave.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa sababu ni mara yangu

ya kwanza kusimama ndani ya Bunge letu Tukufu, Bunge la Kumi na Mbili, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai, afya njema na leo tuko hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi Taifa na Mkoa wangu wa Katavi kwa kuniamini na kunituma tena kuja hapa Bungeni. Napenda kuwashukuru sana akina mama wa Mkoa wa Katavi kwa kuniamini tena kunipa nafasi kwa kipindi cha pili, leo hii tena nimekuja Bungeni kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi nzuri aliyofanya kwa kuwatumikia Watanzania na kwa kuwapa moyo wa kufanya kazi mpaka nchi yetu imetoka kwenye lile *group* la nchi maskini na imeingia kwenye *group* la nchi ambazo zina uchumi wa kati. Ni wajibu wetu sote sisi Watanzania kushirikiana na Mheshimiwa Rais lakini na kumpongeza kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu na Mawaziri wote. Nawapongeza Wabunge wote mliorudi kwenye Bunge la Kumi na Mbili; hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, nimeisoma hotuba yake aliyokuja kutufungulia Bunge letu la Kumi na Mbili, lakini pia aliyofunga kwenye Bunge la Kumi na Moja. Mimi nakwenda kwenye *page* ya 16 pale mahali ambapo Mheshimiwa Rais ameongelea jinsi ya kuleta nidhamu ya kazi maofisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema wazi, katika umri wangu huu ina maana nilisoma katika Serikali ya Awamu ya Kwanza, nikafanya kazi kwenye Serikali ya Awamu ya Pili, ya Tatu na ya Nne na hii ya Tano nikaingia Bungeni. Niliona mmomonyoko wa maadili katika maofisi kwa awamu zote hizo tano. Kwa hiyo, bila kuuma maneno napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kurudisha

nidhamu kazini. Awamu ya Tano oyee, nidhamu kazini ilikuwa imeshuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee mfano kwenye sekta ya afya. Mama anakwenda kujifungua unakuta wale manesi wanashona vitambaa. Mtu anaweza akawa anaumwa uchungu anaita nesi njoo nisaidie anaambiwa mtapike mtoto. Hizo zilikuwa ni lugha za zamani, siku hizi hazipo, sasa hivi nidhamu imerudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho napenda kukizungumzia hapa ni suala la amani. Suala la amani katika nchi yetu hii tunatakiwa sisi Wabunge tuliomo humu ndani tulihubiri, tuilinde hii amani ili watoto wetu wanaokuja waje waikute amani hii. Ni wajibu wetu kuitunza, kuilinda na kuiendeleza amani kwa faida yetu na kwa faida ya wajukuu zetu. Sisi tumekuta nchi hii ikiwa na amani, lugha zetu ziwe za kuendeleza na kudumisha amani, zisiwe za kubomoa, ziwe za kujenga kwa sababu sisi sote ni Watanzania, Tanzania ni moja lakini ina Tanzania Visiwani na Tanzania Bara.

Naomba Wizara ya Muungano itoe elimu ya Utanzania kwenye redio. Mtu ukiwa Zanzibar jisikie kwamba wewe ni Mtanzania, ukiwa Tanzania Bara...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. TASKA R. MBOGO: Ukiwa Tanzania Bara jisikie kwamba wewe ni Mtanzania. Tanzania ni moja, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dorothy George Kilave, atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Qwaray, Mheshimiwa Samweli Hhayuma Xaday ajiandae.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyeniwezesha kusimama katika Bunge hili la Kumi na Mbili. Pia nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo waliweza kupendekeza jina langu na kunisababisha nikawe Mbunge wa Jimbo la Temeke kwa kura nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape shukrani sana ndugu zangu wananchi wa Temeke, wenyewe tumezoea kujita TMK Wanaume kwa kunipa kura nyingi za kishindo hata leo nimeweza kusimama hapa na kuitwa Mbunge wa Jimbo la Temeke kama mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuishukuru familia yangu pamoja na marafiki zangu. Pia nisiwasahau wanangu; Matrona Kilave pamoja na Samuel Kilave kwa sababu walinitia moyo sana katika kipindi kile kigumu, naamini sasa wanafurahia matunda ya maombi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niunge mkono hotuba ya Rais, Dkt. John Pombe Magufuli aliyoitoa hapa Bungeni na kitabu cha miaka mitano ambacho nimeweza kukisoma. Namuunga mkono sana kwa jinsi ambavyo hakika mambo mengi ya miaka mitano iliyopita yameweza kufanyika na hata sasa naamini kwa miaka hii mitano mingine yote yaliyoandikwa katika kitabu kile pamoja na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi yanakwenda kufanyika sawasawa na Ilani yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika elimu. Nishukuru sana Wizara ya Elimu kwa jinsi ambavyo Rais, Dkt. Magufuli, ameweza kutoa elimu bure kuanzia darasa la kwanza mpaka

kidato cha nne. Hata hivyo, lipo moja ambalo napendekeza waweze kulisikia na kuweza kuliweka sawa, nashauri kwamba wajikite kuweka vifaa vya TEHAMA ili hata walimu wetu wanapofanya kazi zao wafanye kazi kwa bidii na tuweze kupata kwa wakati majibu yote ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizingumzie suala la afya. Nimpongeze sana Rais, Dkt. Magufuli, kwa jinsi ambavyo ameweza kuweka sekta ya afya kwa namna ya kipekee kabisa. Sasa akina mama tunajidai, tunajifungua bure pamoja na kwamba zipo changamoto chache ambazo naamini Serikali yetu ni sikivu na inakwenda kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika afya hakika mimi nishukuru sana katika kata zangu 13 ni kata chache tu ambazo hazina zahanati. Namshukuru sana Rais, Dkt. Magufuli, pamoja na Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yote hayo niombe kusema kwamba ipo changamoto ndani ya jimbo langu, sina uhakika kwa wengine, lakini pale ambapo tunakuwa tunauguza na inapofikia yule mgonjwa amefariki, tunapokwenda kuchukua maiti tunadaiwa fedha. Niombe Wizara ya Afya suala hili kidogo linaleta utata ndani ya hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe basi kama Wizara ya Afya itaweza kutoa tamko kwamba tufanye nini pale ambapo tunakuwa tumefiwa tunapohitaji kwenda kuchukua maiti yetu. Labda kama inawezekana tupewe elimu wakati tunapouguza tufanye nini ili tusifikie kudaiwa fedha. Niombe sana Wizara ya Afya iliangalie hili na naamini Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake, wajina wangu Mheshimiwa Dkt. Dorothy ataliangalia hili na kuweza kuona tunapata majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia ni mhanga wa miundombinu katika Jimbo langu la Temeke. Kama nilivyosema tuna hospitali nyingi, tumejengewa na masoko mazuri lakini katika kupita kwenye barabara zile za ndani

hakika *TARURA* sasa waweze kupewa angalau ongezeko la fedha ili tuweze kuona tunapita kwa usalama na kufikia zile sehemu ambapo Serikali yetu imeweza kujenga zahanati pamoja na masoko mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais na nimpongeze sana na Mungu ambariki kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Regina Qwaray, atafuatiwa na Mheshimiwa Samweli Hhayuma Xaday, Mheshimiwa Martha Mariki ajiandae.

MHE. REGINA N. QWARAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipa. Nami niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi aliyonijalia hadi siku ya leo nimeweza kuwepo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee pia nikishukuru chama changu kwa kuniteua na kunipendekeza katika ngazi zote na hatimaye leo niko hapa. Pia niwashukuru kwa namna ya pekee sana akina mama wa Mkoa wa Manyara kwa imani kubwa waliyoonesha juu yangu na kuniona natosha kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niishukuru pia familia yangu; mume wangu na watoto wangu ambao wamekuwa bega kwa bega na mimi muda wote wa mchakato na hata sasa wamekuwa wavumilivu kipindi chote ambacho niko katika majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa iliyoifanya kwa miaka mitano ya kuhakikisha Tanzania inasonga mbele kimaendeleo. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa hotuba nzuri iliyosheheni matumaini kwa Watanzania ambayo inaonesha dira kwa

nchi yetu. Kwa namna ya pekee, tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, busara na hekima ili yale yote aliyohidi na aliyoyasema katika hotuba yake yaweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite katika kipengele cha elimu. Kwanza niipongeze sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo imeona ni vyema kuwa na Watanzania wenye elimu na kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania ambaye ana umri wa kwenda shule anaweza kwenda shule na kupata elimu bure kuanzia darasa la awali mpaka kidato cha nne; si kazi rahisi. Ndugu zangu, Tanzania imesonga mbele. Ukiangalia miaka ya nyuma waliokuwa wanapata elimu walikuwa wachache sana lakini leo kila Mtanzania ana uhakika wa kupata elimu na anasoma bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zote za Serikali bado tuna changamoto ndogo ndogo ambazo Serikali yetu inapaswa ione kwa jicho pevu kwamba bado tuna miundombinu mibovu, madarasa ni machache msongamano ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna upungufu mkubwa wa madawati na wataalam kwa maana kwamba walimu ni wachache. Kuna shule ambazo wanafunzi ni wengi darasani, unaweza kuwa na wanafunzi 200 lakini walimu ni wachache sana. Kwa hiyo, uwiano kati ya mwalimu na mwanafunzi bado haujazingatiwa. Hii inabidi Serikali iangalie uwiano huo ili utendaji kazi kati ya ufundishaji na ujifunzaji uwe mrahisi na wanafunzi wetu waweze kufanya vizuri huko madarasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri Wizara hii ya Elimu iangalie upya mtaala wa elimu unaotumika. Elimu yetu inayotolewa kwa sasa haimuandai mwanafunzi kwenda kusimama mwenyewe na kujitegemea. Kwa hiyo, napendekeza Wizara ione namna gani elimu inayotolewa kwa sasa inaweza kumuandaa mwanafunzi ili aweze kujitegemea. Kwa maana ya kuboresha vyuo vya ufundi,

wanafunzi wapate ujuzi wa kutosha ili waweze kujianzisha maisha kwa maana ya kuwa na ujuzi wa kwenda kujitegemea na kuanzisha ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi nashauri Serikali iboreshe vyuo vya ufundi vilivyopo, lakini ihakikishe inaanzisha vyuo vya ufundi katika kila wilaya vikiwa na taaluma na ujuzi ambapo kila mwanafunzi anaweza kupata ujuzi tofauti tofauti. Kwa hiyo, wanafunzi wetu wanapomaliza kidato cha nne ni vyema akaamua kujichagulia kuingia kidato cha tano na cha sita ama kwenda kwenye vyuo vya ufundi kujipatia ujuzi hatimaye aweze kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Wizara ya Elimu inapaswa sasa kuanzisha au kusimamia kuwepo na kitabu kimoja cha kiada. Kwa maana kwamba tuwe na kitabu kimoja cha kiada kuanzia shule za msingi za Serikali pamoja na shule za msingi za binafsi. Hii itasaidia kuwa na *uniformity* katika elimu badala ya kuwa na vitabu tofauti vya kiada mwisho wa siku wanafunzi wanafanya mtihani unaofanana lakini wakiwa wanawezeshwa kwa kutumia vitabu tofauti tofauti. Angalizo kwa Serikali pia iangalie vitabu vinavyotumika katika shule za *private* viwe na ithibati za Kamishna wa Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Samweli Hhayuma Xaday, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mariki, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ajiandae.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Awali ya yote, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima. Pia nikishukuru chama changu, Chama cha

Mapinduzi na Wanahanang kuniwezesha kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nitumie nafasi hii kuishukuru familia yangu kwa jinsi wanavyoniunga mkono katika kufanikisha majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kukupongeza wewe na Mheshimiwa Spika kwa jinsi mnavyotuongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote, nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali yangu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ikiongozwa na Jemedari, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kwa muda wa miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake ameeleza mambo mengi ya msingi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Nitajikita kwenye maeneo matatu kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameeleza mafanikio yaliyopatikana kwenye sekta ya maji, kwamba kwenye eneo la vijijini kumekuwa na ongezeko la upatikanaji wa maji kwa asilimia 47 mpaka asilimia 70.1 na mjini asilimia 74 mpaka asilimia 84; hayo ni mafanikio makubwa sana. Mheshimiwa Rais pia alibainisha kwamba wakati wa kampeni kulikuwa na malalamiko mengi kwenye eneo la maji.

Niombe Wizara ya Maji wawasimamie kwa karibu wataalam wetu ili miradi mingi ya maji ikamilike. Wenzangu waliotangulia waliiongelea, wengine walifikia hatua ya kusema miradi mingine isianzishwe lakini mimi nasema kwamba usimamizi uimarishwe ili miradi hii iweze kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano wa Mradi mmoja wa maji Katesh, mradi huu ni wa muda mrefu lakini

mpaka sasa bado haujakamilika. Ukienda Mji wa Katesh watu wanatembea na mikokoteni mjini haipendezi sana. Tunaomba ule mradi ukakamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Mradi wa Maji wa Lambo ambao ulitakiwa ukamilike mwezi Mei, 2020, lakini mpaka sasa umefanyika asilimia 45 tu. Wananchi wanasubiri maji na ndiyo malalamiko mengi ambayo tunayapata kwa wananchi wetu. Naomba huo mradi uweze kukamilishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba Wizara inafanya kazi nzuri na kubwa. Mheshimiwa Waziri Aweso na Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer MaryPrisca*, wanafanya kazi kubwa sana. Kuthibitisha hilo, toka Uhuru, Kata ya Gehandu imekuwa ikilia maji, kwa sasa kisima kimechimbwa, maji yamepatikana mengi. Wameshafanya *pump testing*. Ninachoomba, usanifu ukamilike haraka ili mradi uweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo eneo la kilimo. Mheshimiwa Rais alibainisha wazi kabisa kwamba nchi yetu ina upungufu mkubwa wa ngano ya chakula na akamwelekeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atakayemteua kwamba hiyo ndiyo iwe kazi yake ya kwanza. Nampongeza sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Profesa Mkenda na Naibu Waziri Mheshimiwa Bashe kwa kazi waliyoanza nayo. Wamekuja Hanang, tumetembea nao kwenye mashamba ya *NAFCO*, mashamba ya ngano ambapo Hanang ndiyo ilikuwa inaongoza kuzalisha ngano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaahidi wananchi wale wakusanye ngano, kwa sasa zimeshakusanywa zaidi ya tani 480, zile ngazo zikanunuliwe ili wananchi wapate fedha za kurudi mashambani ili tuweze kuzalisha ngano zaidi. Pia tuliwaahidi wananchi wale mbegu; na sasa ni wakati wa msimu wa kupanda, tunaomba zile mbegu zipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la *NAFCO* yale mashamba yalikuwa ya mwekezaji kabla. Maeneo yale mengi yamebinafishwa kwa wawekezaji wengine ambao uwezo wao ni mdogo.

Naomba sana Wizara ya kilimo ifanye tathmini ya kina ya wale wawekezaji ambao wako kwenye lile eneo ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa tupate wawekezaji au Wanahanang wenye uwezo tuweze kutumia yale mashamba na wazalishe kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba niishie hapo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Martha Mariki atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, tutamalizia na Mheshimiwa Almas Maige.

MHE. MARTHA F. MARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kuniona. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema. Kipekee sana napenda kuwashukuru baba na mama yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuniadini mimi kama binti na kama kijana kuweza kuwawakilisha akinamama wa Mkoa wa Katavi. Pia napenda sana kuwashukuru akinamama wote wa Mkoa wa Katavi na UWT kuanzia ngazi ya Mkoa mpaka Taifa. Pia kipekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi anavyoendelea kuchapa kazi na jinsi anavyoendelea kulipeleka Taifa letu la Tanzania mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeisoma sana hotuba ya Mheshimiwa Rais, hotuba hii imebeba maono na dira ambayo inaonyesha ni jinsi gani Tanzania itakwenda mbele katika uchumi endelevu; kutoka uchumi wa kati mpaka uchumi wa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana nijikite katika sekta ya afya. Naishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa jinsi ambavyo inaendelea kupambana kuhakikisha kwamba huduma za afya zinaboreshwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu kuiomba sana Wizara ya Afya, watuboreshee Hospitali ya Wilaya ambayo kwa sasa inatumika kama Hospitali ya Mkoa wa Katavi, kutokana na kwamba mkoa wetu una fursa nyingi sana ikiwemo kilimo, biashara ambazo zinasababisha kuwepo na mwingiliano wa watu wengi. Hivyo, tunaomba sana Serikali yetu sikivu itusikie kwa kutuboreshea Hospitali ya Mkoa wetu wa Katavi ili iweze kuwahudumia wananchi wanaoingia kwa wingi kufuata fursa nyingi za kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda sana nichukue nafasi hii katika kuchangia suala la kilimo. Katika hotuba hii Mheshimiwa Rais ameelezea kuhusu suala la kilimo kwamba atahakikisha kinasonga mbele katika nchi yetu ya Tanzania. Nikiwa kama mwakilishi wa akinamama Mkoa wa Katavi, wananchi wamenituma kwamba katika sekta ya kilimo, kumekuwa na sintofahamu kuhusiana na wakulima wetu. Wakulima wamekuwa na changamoto ambapo wanailalamikia Serikali kuhusu mambo ya Stakabadhi ghalani. Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuja mkoani kwetu alisema Mkoa wa Katavi wakulima wake hatujakidhi vigezo vya kuungwa katika Stakabadhi Ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sekta ya kilimo iweze kutoa maelekezo na tamko: Je, wananchi wa Mkoa wa Katavi tumefikia hadhi ya kuungwa katika Stakabadhi Ghalani? Kama siyoy, basi waweke utaratibu ili wananchi wetu wa Mkoa wa Katavi ambao ni wapiga kura wetu waliotuamini sana waweze kuondokana na sintofahamu hiyo, kwa sababu wanategemea sana kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Elimu kwa jinsi ambavyo

inaendelea kupambana. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi ambavyo anapeleka elimu yetu mbele kwa kutoa elimu bure kuanzia *form one* mpaka *form four*. Katika Mkoa wetu wa Katavi nasi tungependa kuwa na vyuo vingi kama ilivyo katika mikoa mingine. Vyuo hivyo vimwezeshe mtoto wa kike katika Mkoa wa Katavi aweze kwenda kupata elimu kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nawakaribisha sana Waheshimiwa wenzangu mje mwekeze katika Mkoa wa Katavi wenye fursa nyingi zikiwemo za kiutalii na kilimo. Karibuni sana, Katavi imenoga jamani, karibuni. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Erick Shigongo ajjandae.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na nawashukuru wote kila mmoja kwa nafasi yake aliyechangia uwepo wangu mahali hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kupokea Hotuba ya Rais kwa mikono miwili na nampongeza sana kwa sababu sisi kama Wabunge, tumepokea dira na tumepata kitendea kazi cha kufanyia kazi katika uwakilishi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naanza na sekta ya utalii, katika ukurasa wa 46, Mheshimiwa Rais ameongea kwamba ni sekta ambayo itawekewa mkazo mkubwa kutokana na umuhimu wake katika Taifa letu; kwanza, katika mchango wake mkubwa katika kuongeza pato la Taifa, pia ni sekta ambayo itatoa ajira kwa vijana wetu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza upande wa Serikali; wenzetu hili wameshalianza, nasi watu wa Kanda ya Kusini au *Southern Socket Tourism* tunawashukuru sana kwa

sababu tumeletewa mradi mkubwa wa *REGROW* ambao umetengewa dola milioni 150 kwa ajili ya kuendeleza utalii kusini; Iringa pia haikuachwa, itakuwa *hub* ya utalii huo, nasi tumepewa dola milioni sita kwa ajili ya kuanzisha *Tourist Resource Center* pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana kuhusu msitu wa Kihesa Kilolo. Namshukuru Waziri wa Maliasili, tumeongea hili na amelifanyia kazi kwa haraka sana. Naamini ujenzi unaanza pale mara moja ili nasi *southern socket* au ukanda wa kusini tuwe sehemu ya kuchangia pato la Taifa kupitia utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba, ili utalii uweze kuwa mzuri, tunahitaji kuboresha huduma zetu kwa watalii. Kwanza, naomba tuboreshe huduma ya upatikanaji wa ubadilishanaji wa fedha za kigeni. Watalii wetu wengi wanapokuja kwenye *zones* za utalii wanakosa huduma hii kutokana na mchakato ambao ulipitishwa kwenye maduka yetu ya kubadilisha fedha za kigeni. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iangalie hasa kwenye hizi nyanda za utalii, ni namna gani inalegeza masharti ili tuweze kuwahudumia watalii na lile neno lao, watakaporudi tutapata watalii zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusu kuboresha huduma za miundombinu, tunaomba barabara. Tumeshaanza kuboreshewa kiwanja cha ndege, sasa tunaomba barabara ile ya *National Park*, watakaposhuka pale ile barabara ya kutoka Iringa mpaka *Ruaha National Park* ya kilometa 104 basi nayo iboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala la elimu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ukarabati mkubwa uliofanyika kwenye Shule za Sekondari kongwe, tunaomba juhudi zile zile zielekezwe kwenye shule zetu za msingi kwani nazo zimechakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mtaala haliepukiki, tunaomba Wizara ya Elimu tujipange kubadilisha mtaala kwa watoto wetu ili watoto wetu waweze kuajirika na kujajiri nje

na ndani ya nchi yetu. Tunaomba sana elimu ya kujitegemea irudishwe kwenye shule zetu ili watoto hawa wanapotoka waweze kujifunza kujitegemea. Vile vile tunaomba kuwe na masomo *compulsory* kama ya ujasiriamali kuanzia kwenye *level* ya shule ya msingi ili watoto waweze ku-*develop visions* zao wenyewe tangu wakiwa wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana kwamba kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais pia amesema kutakuwa na *program* mbalimbali za mafunzo ya ujuzi na maarifa ili kukuza uchumi. Tunaomba sasa vyuo vikuu vilivyoko kwenye *zones* zetu na mikoa yetu, kama kile Chuo Kikuu cha Mkwawa, kiwe *independent*, kiweze kusimama chenye ili kisaidie kutengeneza *program* zao kwenye kanda zetu zile ili kuwasaidia watoto wetu waweze kupata maarifa ya kufaidika na mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiendelee kuwa ni Vyuo Vikuu Shirikishi halafu vinaendelea kupokea *program* zinazopangwa Dar es Salaam wakati kule kule zinge-*scan* mazingira ya kule, zingepanga *program* za kule kule, zitawasaidia wananchi wetu. Tunaomba sana hili lichikuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la uchumi, tunashukuru kwa ajili ya uzalishaji, lakini tunaomba sana mafunzo ya ujasiriamali yatiliwe mkazo kwa sekta binafsi lakini kwa *informal sector* na *formal sector*. Tunaomba makundi yale ya Madereva, Wamachinga, makundi ya bodaboda, yapewe mafunzo ya ujasiriamali ya kimkakati kutokana na kazi zao. Mafunzo ya ujasiriamali yasiandaliwe tu kwa ujumla, lakini yaende *specific*. Kwamba hawa ni Mama Ntilie, katika sekta yao tunawaboresha vipi? Hawa ni madereva wa bajaji, katika sekta yao tunawaboresha vipi? Tusitafute kupeleka mafunzo ambayo ni mafunzo...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kengele imeshagonga.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja. Kulinda tunu za Taifa, naomba hili niliseme. Hapa yameongelewa masuala...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesca kuna majina mengi hapa mbele. Ahsante sana.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Shukurani.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Erick Shigongo na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hotuba hizi mbili za Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli, lakini leo naziite alama za Mheshimiwa Dkt. Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amechora ramani ya maendeleo ya nchi yetu na katika ramani hiyo, ameweka alama na alama hizi ndizo tunazozifuata sisi. Alama ya kwanza ni umeme wa *REA*. Anasema ameweka umeme katika vijiji 9,884 na vimebakia vijiji 2,000 tu. Alama ya pili pia anajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere kule Rufiji; pia ameweka miradi ya maji 1,422 na vijijini asilimia 70 na mijini asilimia 80. Mfano huu ni Mradi Mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria katika Mji wa Tabora, Igunga na Nzega na mradi huu umekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alama nyingine ni elimu bure kwa Watanzania. Watoto wote wa Kitanzania, darasa la kwanza mpaka *form four*. Pia anajenga vituo vya *VETA* na hivi vinakuza uchumi. Zamani ilikuwa ukiharibikiwa na gari vijijini unamtafuta fundi kutoka mjini aje atengeneze gari, lakini anaondoka na hela, vituo hivi sasa vinajenga mafundi vijijini.

Majokofu, vitu vya umeme, wanachomelea ma-*grill* na fedha zinabaki kule, kwa hiyo, zinazunguka badala ya kurudi mjini. Kwa hiyo, tunakuza umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, alama nyingine kubwa ni ununuzi wa ndege 11 kwa ajili ya Shirika la *Air Tanzania*. Pia kuhusu alama ya huduma ya afya, amesema katika hotuba zake hizi, Mheshimiwa Rais amejenga vituo vya kutolea huduma za afya 1,887; zahanati 1,198, Vituo vya Afya 487, Hospitali za Wilaya 99, Hospitali za Rufaa 10, Hospitali za Kanda tatu na wagonjwa kwenda nje wamepungua na kufikia asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, Jimboni kwangu kuna changamoto. Kwa mfano, Jimbo zima lina Kituo kimoja tu cha Afya na tungependa viongezwe. Kuna vituo vile tunajenga sisi wenyewe, tunaomba vituo hivi visaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kitaifa liko suala la Kiswahili. Wiki hii Kiswahili kimepandishwa hadhi kabisa kwamba Wizara moja tu Tanzania ilikuwa inatumia lugha ya Kiingereza katika maandishi yake, Mahakama. Juzi umetoka Mwongozo kwamba Mahakama sasa zitumie lugha ya Kiswahili kwa ajili ya kutoa hukumu zake. Naona haitoshi tu hiyo, kwa sababu Kiswahili kitaanzia juu tena. Waswahili wanasema mtaka unda haneni, lakini mimi leo nanena hata kama litaharibika, watu wenye roho mbaya, ndiyo maana methali hii ipo. Nina nia ya kuleta tena hoja ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika shule zetu za msingi na sekondari. Hili litakuwa jambo zuri kwa sababu sasa hivi tutajenga Kiswahili kuanzia shule za msingi, sekondari na matumizi yake yatadumu vizuri katika taasisi zote katika mihimili yote mitatu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitasema hayo tu, nilikuwa nimekusudia kutaja hizo alama za Mheshimiwa Rais. Nakushukuru sana kwa kuniruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Eric Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Mheshimiwa Geoffrey Mwambe ajiandae.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge hili. Naishukuru familia yangu, Wajumbe wote na wananchi wote wa Buchosa walionipa nafasi ya kuwa hapa, Chama changu Cha Mapinduzi, Mwenyekiti, Katibu wa Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wa nchi yetu waliotangulia ambao kwa uwepo wao, maisha yangu leo ni bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi yetu leo hapa ni kujadili hotuba mbili za Mheshimiwa Rais. Nami nimepata bahati ya kuzisoma kama walivyozisoma wenzangu wote, nimezisoma na nimezielewa. Katika kuzisoma kuna kitu kimoja kikubwa nilichokigundua kwamba Mheshimiwa Rais anawaamini sana Wabunge wake na anaamini kwamba hakuna kiongozi duniani anayefanikiwa peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Musa alichagua wazee; Yesu Kristo alikuwa na wanafunzi wake 12; na Mtume Muhammad alikuwa na Maswahaba wake. Kwa hiyo, sisi hapa ndani ni Maswahaba wa Mheshimiwa Rais, ametuamini, amekuja kutusomea hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusoma, nimekumbuka kitabu kimoja nilikisoma kinaitwa *Checklist Manifesto*. Kwa wale ambao wamekisoma watagundua kwamba hotuba hizi mbili za Mheshimiwa Rais ni *Checklist Manifesto* mbili; ya kwanza ilikuwa ya 2015 – 2020 ambayo inaonyesha mambo ambayo Mheshimiwa Rais alitaka kuyafanya kwenye kipindi cha miaka mitano. Nikiwauliza kwenye *Checklist Manifesto*, kazi yako ni ku-*list* mambo yako, unatiki moja baada ya lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikikuuliza wewe na Waheshimiwa Wabunge kwamba kwenye miundombinu, Mheshimiwa Rais ametiki au hajatiki?

WABUNGE FULANI: Ametiki! (*Makofi*)

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwauliza kwenye umeme, Mheshimiwa Rais ametiki, hajatiki? Kwenye barabara, ametiki hajatiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mengi yametikika. Sasa tuna *Checklist Manifesto* ya pili ya mwaka 2020 – 2025, ni *checklist* ngumu zaidi ya *checklist* tuliyomaliza. Ni ngumu kwa sababu nchi yetu iko kwenye uchumi wa kati. Ni *checklist* ambayo siyo rahisi kama iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuja kwenu na nazungumza mbele yako na mbele ya Watanzania wote kuwakumbusha kwamba kazi tuliyonayo ni kubwa. Mengi yamefanyika, kazi kubwa imefanyika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, lakini nataka niwakumbushe kwamba kazi tuliyonayo mbele ni kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu mmoja aliwahi kusema kwamba *the smallest of implementation is better than the biggest of intensions*. Kama hatutatekeleza hotuba hii, tukabaki na mazungumzo ya hotuba nzuri, hakika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais itabaki ni *intensions* peke yake, hakuna matokeo yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea *private sector*. Kwenye *private sector* hatuna hotuba nyingi sana, tuna utendaji peke yake. Nazungumza hapa nikiwaomba Waheshimiwa Wabunge, katika *Checklist Manifesto* ya pili 2025, tufanye kazi, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, tusimvunje moyo Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma katika hotuba yake, ukurasa siukumbuki vizuri, lakini amesema kwamba mazao ya bahari yangeweza kuiingizia nchi yetu shilingi bilioni 320 na kitu hivi kwa mwaka. Tunazozipata ni kidogo mno kwa sababu tulishindwa kudhibiti na kusimamia vizuri, *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia nyuma ya *statement* hiyo kwa mimi mwanafasihi, nagundua kwamba Mheshimiwa Rais alikuwa na manung'uniko, alikuwa na masikitiko. Nawaomba Waheshimiwa Mawaziri walioko hapa ambao mmepewa jukumu, mmefanya kazi nzuri sana kwenye *checklist manifesto* ya kwanza. Mameaminiwa, fanyeni kazi, tumikeni, tengenezeni historia, tuko hapa kujenga historia yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wetu watakapokuja baada ya miaka 20 waseme maisha yao ni bora sana kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa kaka yangu Majaliwa. Watoto wetu wasimame waseme maisha yao ni bora kwa sababu sisi tulioko ndani ya ukumbi huu leo tutafanya maamuzi sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuwaomba ndugu zangu, Watanzania wanatuamini, dunia inatutazama, tutakachokifanya hapa ndani katika kipindi cha 2025 ni kufanya maamuzi ambayo tutatekeleza ndoto ya Mheshimiwa Rais wetu. Viwanda ni ndoto ya Rais wetu lakini hakuna viwanda bila kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikomee hapo. Ahsanteni sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. SOUD MUHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake amesisitiza kuziendeleza na kuhifadhi maliasili za nchi. Katika kumuunga mkono na ili kumsaidia kufikia malengo ni vyema

changamoto za sekta za maji, ardhi, kilimo na mifugo ambazo zinachangia moja kwa moja uharibifu wa maliasili zishughulikiwe kwa ushirikiano wa kissekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ripoti ya Mawaziri saba kuhusu ardhi iletwe Bungeni na kujadiliwa, kwani kuna michango mizuri ya kujenga kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali iwe makini katika kumega hifadhi na mapori ya akiba kwa lengo la utatuzi wa changamoto za sekta za ardhi, mifugo na kilimo. Huu hauwezi kuwa ufumbuzi wa kudumu.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais akifungua rasmi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma, tarehe 13 Novemba, 2020 naomba kutoa mchango wangu wa maandishi baada ya kubaini kwamba wachangiaji wamekuwa wengi na naomba niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hotuba zote mbili ya mwaka 2015 na ya 2020; kama Mheshimiwa Rais alivyotuasa Wabunge kwamba lengo la kufanya hivyo ni ili tuweze kupima utekelezaji wa vipaumbele alivyokuwa navyo Mheshimiwa Rais katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ni dhahili kwamba Mheshimiwa Rais amewafanyia Watanzania kazi nzuri mno na ni utendaji uliotukuka ambao umekiinua chama chetu (CCM) na hata kutubeba Wabunge tulioshinda katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, 2020 na kuwepo Bungeni leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Ilani ulikuwa wa ufanisi mkubwa kila sekta; kwanza, utawala bora. Tumeweza kuwa nchi ya kwanza Afrika katika kupiga vita

rushwa. Pia tumekuwa nchi ya 28 kati ya 136 duniani katika matumizi mazuri ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uchumi umekuwa kwa 7% na kufanya pato ghafi kupanda toka shilingi trilioni 94.349 2015 hadi kufikia shilingi trilioni 139.9 mwaka 2019 na Taifa kupanda chati kiuchumi na kuwa Taifa la uchumi wa kati 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, umeme wa *REA* toka vijiji takribani 2000 mwaka 2015 na kufikia vijiji 9000 mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, upatikanaji wa maji safi na salama kuongezeka kutoka 47% mwaka 2015 hadi 70.1% mwaka 2020 kwa vijijini na kwa mjini toka 74% hadi 84%.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, barabara za lami zimejengwa, madaraja yamejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, watoto wetu wameendelea kupatiwa elimu bila malipo darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Kila sekta Serikali imefanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, miradi mkakati imeendelea kutekelezwa, mfano Bwawa la Mwalimu Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha umeme megawati 2115 linaendelea kujengwa na mradi unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* unaendelea vizuri na *section* ya Dar es Salaam/Morogoro itamalizika mwaka huu wa 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATCL*; ndege zimenunuliwa nane na zinaruka; tatu ziko njiani; kwa kifupi mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano kipindi cha kwanza cha miaka mitano (2015 – 2020) ni makubwa sana na pongezi na shukrani nyingi zimuendee Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufuli kwa uongozi uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ya Novemba 13, 2020, kimsingi kwenye hotuba hii ameweka dira kwa Taifa kwamba ni mambo gani amepanga kutekeleza na ameweka wazi kwamba itakuwa ni utekelezaji Ilani ya Uchaguzi yenye kurasa 303 na ahadi alizotoa majukwaani wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mengi ya kuboresha maisha ya Watanzania lakini naomba kuchangia kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara; zitajengwa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 2500 na lengo ni kufikia kilometa 6006 kuunganisha Wilaya na Mkoa yote nchini. Nashauri utekelezaji uanze na ahadi za Mheshimiwa Rais alizozitoa hadharani kwa mdomo wake na mbele ya wapiga kura wengi ukizingatia kwamba pia mikutano yake ilikuwa na watu wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Meru aliahidi kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Malula Kibaoni kwenda King'ori; Maruvango, Leguriki hadi Ngarenanyuki na mpaka Oldonyosambu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; kwenye hotuba ya Rais kilimo kitaboreshwa na kubadilishwa sura kiwe kilimo cha biashara ili kuongeza uzalishaji. Nashauri Wizara ya Kilimo iongeze nguvu kwenye miundombinu ya umwagiliaji ili tuondokane na kilimo cha kutegemea hali ya hewa ambapo mvua zikikosekana basi wakulima wanapata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eleimu; elimu itaendelea kuboreshwa na mpango ni kujenga shule za sayansi za wasichana moja kila Mkoa. Huu mpango mzuri na kule Meru kuna shule ya wasichana ilibuniwa na aliyekuwa Mbunge wetu kwa tiketi ya CCM Marehemu Jeremiah Solomon Sumari ambaye alitangulia mbele ya haki Januari, 2012 kabla ndoto yake haijatimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni shule hiyo ijengwe maana ilishaanza tayari na eneo la ujenzi lipo. Nilikwenda kutembelea mradi huo nikaridhika na kuamua kwamba nitaishawishi Serikali iendelee na mradi huo kumuenzi ndugu yetu huyo ambaye mema yake sasa yanaingia kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa 2021 – 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe, Naibu Waziri wa Kilimo atafuatiwa na Mheshimiwa Geofrey Mwambe, Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Uwekezaji ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa hii. Vilevile nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya asilimia 93 ya Wabunge waliochangia wameongelea sekta ya kilimo. Hii inaonesha ni namna gani sekta hii inagusa maisha ya watu na umuhimu wake. Sisi kama Wizara ya Kilimo tunakiri na kupokea baadhi ya changamoto ambazo wamezisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Wizara na Serikali kwa ujumla imejipanga kuhakikisha tunaondoa hizi changamoto zinazotukabili katika sekta ya kilimo. Changamoto ya kwanza ni mbegu na viuatilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siri na *future* ya sekta ya kilimo ni *research and development*. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo lani imetupa *targets* za ku-*attain* katika kila zao ambazo ni lazima tuzifikie na *target* hiyo siri yake ni mbegu. Kwa hiyo, kama Wizara tutakapokuja katika mpango hatua ya kwanza tuliyoamua suala la mbegu litakuwa ni suala la uzalishaji wa mbegu kwa *solution* za ndani. Kwa kipindi cha

miaka mitano ijayo tutawekeza shilingi bilioni 179 kwa ajili ya *research and development and seed multiplication*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakaelewa. Tunapozungumzia mbegu kwanza hili ni suala la dunia na Tanzania ni sehemu ya dunia na sisi hatuwezi kujiondoa katika hiyo seti. Kwa hiyo, tunawekeza katika *research* kwa ajili ya *ku-develop* mbegu za aina ya *OPV* na *hybrid* lakini wakati huo huo kutunza mbegu zetu za asili na sisi kama Wizara tunakuja hapo mbele Mwenyezi Mungu akitujaalia na sheria maalum ya kulinda *traditional seeds* ili ziweze kufanyiwa *purification* na ziweze kufanyiwa maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi mbegu tunazojadili ni nne, ni *traditional seed* (mbegu zetu za asili), *OPV*, *hybrid* na sasa kuna teknolojia ya *GMO*. Sisi kama nchi tumesema hatutumii mbegu za *GMO* na hatutaruhusu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka utaratibu wa wazi kwamba *hybrid seed* ambayo inajulikana *parent seeds* wake (wazazi wawili), labda nitumie lugha rahisi, tunapozungumzia mbegu za *hybrid* tunazungumzia mbegu mbili za kiume na kike zenye sifa mbili tofauti zinazofanyiwa *cross breeding*. Hapa msingi wake ni mbegu za asili. Unaweza ukakuta mbegu ya mahindi ya asili A ina sifa ya kuwa na uzalishaji mkubwa lakini haina uwezo wa ku-*resist* magonjwa. Mbegu B ina sifa ya ku-*resist* magonjwa lakini uzalishaji wake ni mdogo. Wataalam wetu wanafanya kazi ya kuzi-*breed* hizi mbegu mbili ili kupata mbegu ambayo inaweza kuwa na sifa zote mbili na kumsaidia mkulima. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama nchi *potential demand* yetu ya mbegu ni tani 371,000. Hii ndiyo *potential demand* yetu lakini mbegu tunazozalisha za kisasa ni tani 76,000 na tani 11,000 ni mbegu tunazoagiza kutoka nje na mbegu zinazobaki ni mbegu zetu za asili ambazo tumekuwa tukizitumia katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano zao kama alizeti, tunakiri kama Wizara tumechukua hatua katika suala la kupambana na *gap* ya mafuta. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa Kigoma kuzindua usambazaji wa miche ya michikichi. Tumegawa miche ya michikichi zaidi ya 1,000,000. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi kama Wizara tunahitaji uzalishaji wa tani 5,000 za *hybrid seed* na *OPV seed* za alizeti ili tuweze kufikia uzalishaji tunaohitaji wa mbegu za mafuta. Ni kweli viwanda vya kuchakata mafuta vinakabiliwa na changamoto kubwa sana katika suala la uzalishaji wa mbegu. Nilitaka nitoe tu *commitment* ya Wizara katika eneo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili ambayo tunachukua, Rais katika hotuba amesema suala la ngano. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge wa Hanang, hivi sasa tunavyoongea Wizara ya Kilimo imesaini *MoU* na wanunuzi na wachakataji wa ngano ndani ya nchi. Tunatengeneza utaratibu ambao tumekubaliana na *private sector* kwamba hatoagiza ngano kutoka nje kabla ya kununua ngano yote ya ndani. Sasa tunavyoongea tumejiwekea lengo la kuzalisha *metric tonnes* 150,000 katika msimu huu unaokuja na tutagawa jumla ya tani 36,000 ya mbegu kwa ajili ya kuzalisha ngano katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Dodoma tumefanya *pilot project* hapa Bahi ambapo ndiyo sehemu ambayo mbegu ya ngano imeonekana ina-*mature* kwa muda mfupi kuliko wakati wowote, katika Wilaya ya Bahi na Mkoa wa Rukwa tunagawa hizi mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichokubaliana na wanunuzi ni nini? Kilimo ni biashara, lazima u-*define volume and price*. Kwa hiyo, tulikaa na wanunuzi tukawauliza wananunua ngano kutoka nje kwa bei gani? Tukapiga mahesabu na tukakubaliana watanunua kilo moja kutoka kwa mkulima kwa shilingi 800 bei ya chini mpaka Sh.1,000 kilo moja ya ngano. Sasa hivi wakulima walikuwa wanauza kati ya shilingi 500 na shilingi 600 na walikuwa hawana uhakika

wa soko. Nataka nimhakikishie Mbunge wa Hanang hivi sasa tunavyoongea Kampuni ya Bakhresa wako Wilaya ya Hanang, awasiliane na DC wake wanachukua zile tani 400 zilizoko pale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *secret* ya kilimo ni *economies of scale*. Mimi nataka niseme sisi wote ni wajumbe wa Baraza la Madiwani, niwaombe sana tusipokuwa makini tutajenga Taifa la wachuuzi badala ya Taifa la wazalishaji. Wizara tuko tayari kuwasaidia kwa ajili ya kuanzisha *block farming* na katika bajeti ijayo tengeni maeneo kama Wilaya ya Manyoni kama kwenye suala la korosho tuweze kuzalisha mazao mbalimbali na sisi tutawasaidia mbegu, wataalam, vitendea kazi ili tuweze kulifikia lengo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kama Wizara ya Kilimo tumejiwekea *target*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia tu. Tumejiwekea lengo la kukua kwa asilimia 10 katika kipindi cha miaka mitano ijayo badala ya asilimia 5. Tunawaomba *support*, ushirikiano wenu na ni lazima tukubaliane kama nchi kuwekeza katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, Waziri wa Viwanda na Biashara atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Waziri wa Mifugo ajiandae.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunifanikisha kuwa hapa leo. Pili nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa imani yake kubwa aliyokuwa nayo kwangu kunipa utumishi wa kusimamia jukumu la Wizara yetu ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nisisahau chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa imani kubwa waliyokuwa nayo wajumbe wetu wa Mkutano Mkuu wa Jimbo la Masasi Mjini. Pia niwashukuru wananchi wa Masasi kwa kunipa kura nyingi na kunipa jukumu la kuwawakilisha kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuishukuru sana familia yangu akiwemo mke wangu Tumaini Jasson Kyando na watoto wangu King King, Caren, Catherine kwa imani kubwa waliyokuwa nayo na kunivumilia kwa kipindi kirefu cha utumishi wangu ambapo muda mwingi nakuwa nje ya nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa tumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Kimamlaka *presidential speech is a policy speech*. Rais anapata *absolute powers* kutoka kwenye Katiba, ana mamlaka yote. Mamlaka ya mwananchi mmoja mmoja yote yamekusanywa kupitia kura wakampa yeye. Kwa hiyo, tamko lake ni tamko la wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi watumishi ambao tunatumikia kwa nafasi zetu za kuongoza Wizara kwa niaba yenu, ni maelekezo na ni maagizo. Kwa hiyo, mwanzo kabisa napenda kusema kwamba naunga mkono hoja na sisi tumejipanga kutekeleza. Kazi yetu kubwa ni kutekeleza na tumeshaanza kuifanyia kazi hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sana napenda nikumbushe kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais zote mbili ikiwemo hii ya terehe 13 Novemba 2020, zinawiana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 - 2025. Yote ambayo ameyaongea ni yale ambayo yako kwenye kurasa 303 ya Ilani ya CCM ambayo wengi wetu hapa tulikuwa tunainadi

na bahati nzuri pia kila mmoja humu ndani hakuna ambaye amesema kwamba hotuba ile kuna maeneo hakubaliani nayo isipokuwa msisitizo ni namna sisi kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mlituambia wiki ijayo tutakuwa na mjadala wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Rais inajikita huko pia. Baada ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ambao tulikuwa tunajikita kwenye kutengeneza miundombinu ikiwa ni kama *capillaries* za uchumi, wa pili tukasema tujenge viwanda lakini Mpango wa Tatu tunachukua sasa mafanikio ya kipindi cha kwanza na cha pili tunaunganisha kwenye mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia hotuba ile ukurasa wa 10 – 26 kuna maeneo mengi ambayo Mheshimiwa Rais ameyaelekeza ambayo yanagusa kwa namna moja au nyingine maeneo ya viwanda na biashara. Hivyo napenda kupitia hotuba hiyo kuangalia michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kujua namna ambavyo sisi kama Wizara ya Viwanda na Bishara tumejiandaa. La kwanza, ni utekelezaji wa *blue print*. Kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walionesha kama vile tunahitaji tuanze kutekeleza lakini naomba niwahakikishie kwamba *blue print* tumeanza kutekeleza tangu mwaka juzi na baadhi yenu mnafahamu hata ile iliyokuwa *TFDA*, sasa hivi inaitwa *TMDA* kutokana na utekelezaji wa *blue print*. Kwa hiyo, tutaenda kuhakikisha kwamba ile *comprehensive action plan* ya *blue print* tunaitekeleza ipasavyo na kuja na mbinu mpya zaidi ya kuweza kutekeleza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa upande wa masoko imezungumzwa sana hapa kwamba bidhaa nyingi zinakosa masoko. Naomba niwahakikishie tunaenda kuiboresha taasisi/ mamlaka yetu ya Maendeleo ya Biashara (*TANTRADE*) ambayo kimsingi imebeba jukumu la *Board of Internal Trade (BIT) and Board of External Trade (BET)*. Bodi hizo mbili ziliunganishwa zikatengeneza *TANTRADE*, lengo lake kubwa au majukumu yake makubwa ni kutafuta masoko ya

mazao yetu na bidhaa zetu kwa masoko ya ndani kuunganisha kutoka mkoa mmoja na mwingine, masoko ya kanda na masoko ya Kimataifa kupitia *multilateral trading system* ambayo sisi ni Wajumbe. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwenye hili tutaenda kupambana kuhakikisha masoko ya bidhaa zetu yanapatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maboresho ya taasisi zetu. Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kiko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, nimewaambia kwamba tuangalie *course content*. Tusingependa na kwa kipindi hiki sio vyema kutengeneza *business administrators* yaani tunatengeneza wasimamizi wa biashara, biashara ya nani? Mimi nimewaambia wakae, waje na mpango mpya tutengeneze *course content* ambazo zinamjenga asilimia 70 yule mtoto yeye ndiyo akawe mfanyabiashara halafu asilimia 30 iwe ndiyo kusimamia biashara. Unakuwa *business administrators* wengi wanasimamia biashara ya nani? Kwa hiyo, tunaenda kuiboresha hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Viwanda na Biashara, tutakuja na Programu ya Miliki Kiwanda ambayo nitaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake ametamani nyie muwe sehemu ya mabilionea mshiriki. Tutakuja na Programu ya Miliki Kiwanda ili kokote ulikokuwa kwenye Jimbo lako, wilaya yako tutengeneze utaratibu wa kuanzisha kiwanda wewe Mbunge ukiwa ni *champion* kwenye eneo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna masuala ya sekta binafsi. Sekta binafsi yetu ni changa sana tunahitaji kujenga kwenye maeneo mawili. La kwanza, kuwapa fursa ya kuweza kufanya biashara. Hii tumezungumza mara kwa mara na nashukuru pia Mheshimiwa Waziri Mpango mara baada ya kuapishwa tu alikutana na uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania aliwasisitizia, kufunga biashara au kiwanda cha mtu iwe ni baada ya *Commissioner General* kutoa kibali. Biashara zote ziko chini ya leseni za viwanda na biashara, napenda

kusisitiza sana, tuilee sekta binafsi lakini pia tuwaelimishe kwa upande wa *integrity*, lazima na wao wawajibike upande wao kuwa na *integrity* kwa Serikali ili iweze kuwaamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Uwekezaji atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ajandae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UWEKEZAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni yao mazuri sana kuhusu Sekta ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu baadhi ya hoja, naomba niseme mambo mawili ya kihistoria. Moja, naomba nichukue nafasi hii kukipongeza sana Chama cha Mapinduzi kwa kuadhimisha miaka 44 tangu kilipozaliwa na ukijumlisha na wazazi wake, miaka 60 leo mambo ambayo yanakifanya kuwa chama kikongwe kabisa Barani Afrika. Historia ya leo inakiweka Chama cha Mapinduzi kuwa chama ambacho kimekaa madarakani kwa muda mrefu kuliko vyama vyote Afrika. Mwaka juzi kulikuwa na chama ambacho kilikuwa kimekizidi sitaki kusema nchi gani lakini kimeondolewa madarakani kwa hiyo kimebaki Chama cha Mapinduzi na nakipongeza sana kwa historia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Bunge hili zimeshatolewa hotuba hapa za kufungua Bunge na hotuba za wakuu wa nchi zaidi ya 20 lakini zipo hotuba tano ambazo ni za kihistoria ikiwemo hizi hotuba mbili ambazo tunazijadili leo. Kwa ruhusa yako kwa haraka sana, hotuba ya kwanza ya kihistoria ambayo inajulikana katika nchi hii ndani ya Bunge hili ni hotuba ya Desemba, 1962 iliyotolewa na Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere. Hotuba hiyo ndiyo iliyozaa Jamhuri ya Tanganyika. Lengo lake kubwa ilikuwa ni kujenga Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya pili ni ya tarehe 25 Aprili, 1964 iliyotolewa katika Bunge hili. Lengo la hotuba hiyo Mwalimu alitumia kuomba ridhaa ya Bunge kuridhia Mkataba wa Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar. Hotuba hiyo ndiyo iliyozaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya tatu muhimu ya kihistoria katika nchi hii ya tarehe 29 Julai 1985. Hotuba hii alitumia Mwalimu Nyerere kuaga...

WABUNGE FULANI: Uwekezaji.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UWEKEZAJI): Tulia wawekezaji unakuja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya nne ni ya tarehe 20 Novemba, 2015 iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Hotuba hii lengo lake kubwa ilikuwa ni kujenga msingi wa kupambana na ufasadi na kuimarisha maadili ya utumishi wa umma na matokeo yake wote tumeyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya tano ya kihistoria ni iliyotolewa tarehe 13 Novemba, 2020. Lengo lake kubwa ni kulinda na kuendeleza *status* ya nchi ya uchumi wa kati. Hotuba hii imetoa mwelekeo wa kiuchumi wa nchi na imejengwa katika uwekezaji kama njia ya kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunipa nafasi kuwa sehemu ya Serikali yake ili kutekeleza maono makubwa ambayo yapo ndani ya hotuba hii ya tarehe 13 Novemba, 2020. Lengo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais ametuelekeza na ambalo tunalisimamia kwa bidii na kwa maoni ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa ni mambo matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tuhamasishe uwekezaji wa ndani nan je ya nchi. Katika kuhamasisha

uwekezaji Waheshimiwa Wabunge wanairudia ile kauli ya Mheshimiwa Rais, tunapozungumzia uwekezaji sio lazima moja, iwe kutka nje, lakini sio lazima uwe bilionea. Unatumia nafasi yako ndogo uliyonayo unaweka akiba, unapata mtaji, unawekeza unajenga uchumi, unaanza kujitengenezea mazingira kutoka kuwa elfunea kwenda milionea na hatimaye kuwa bilionea. Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani waende kuhamasisha katika halmashauri zao ili halmashauri zetu zitengeneze mazingira ya uwekezaji, ikiwemo kutenga maeneo ya uwekezajikwa wawekezaji wetu wa ndani, lakini pia wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tumepewa kazi ya kuwezesha wawekezaji ndani ya nchi waliokwisha kuwekesha hapa kwa sababu, balozi mkubwa sana uwekezaji ni yule muwekezaji ambaye tayari yupo ndani ya nchi. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuendeleo kuhamasisha halmashauri zetu ili ziweke mazingira mazuri ya kuhudumia wawekezaji ambao wapo. Pale ambapo kuna changamoto za wawekezaji tuzishughulikie kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika uwekezaji, ni muhimu sana kuwahudumia. Kwamba, pale ambapo mwekezaji ameshaweka, amewezeshwa, kiwanda kipo pale, ni muhimu sana mamlaka zilizopo kuanzia ngazi ya halmashauri wawekezaji hawa wahudumiwe kwa kupatiwa mahitaji muhimu. Tunafanya mawasiliano ya karibu na wenzetu katika Wizara mbalimbali ili kuhakikisha kwamba, huduma muhimu zikiwemo umeme, maji na barabara zinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, kwa sasa katika nchi yetu huduma za msingi za kufanya uwekezaji mkubwa zipo vizuri ikiwemo katika eneo la miundombinu. Kama ni barabara maeneo yote makubwa yameshaunganishwa kwa mtandao wa barabara za lami. Kama ni usafiri wa majini karibu maziwa yetu yote makubwa ikiwemo na bahari tayari kuna vyombo vya usafiri vya kutosha, lakini pia usafiri wa anga umeimarika sana. Kama ni hali ya kisiasa ambayo ni ya msingi

sana katika uwekezaji Tanzania ndio inaongoza kwa utulivu wa kisiasa Afrika. Kwa hiyo kwa kweli Waheshimiwa Wabunge tuendeleo kuhamasisha wawekezaji waje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, tupo katika mchakato wa kuifanyia mabadiliko Sheria ya Uwekezaji ili kuiboresha zaidi ikiwemo kuimarisha taasisi yetu ya TIC ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wametoa maoni mazuri namna ya kuiboresha. Pia tunatengeneza mkakati wa kuhamasisha uwekezaji katika ngazi ya kitaifa, lakini pia katika ngazi ya mkoa hadi katika ngazi ya halmashauri na ndio maana tumekuwa tukipita Mheshimiwa Waziri Mkuu akituongoza kwenda kuzindua Miongozo ya Uwekezaji katika ngazi ya mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwaalika sana Waheshimiwa Wabunge katika mikoa yenu. Pale ambapo tumekuja kuhamasisha na kuzindua miongozo hii naombeni sana mshiriki. Niwapongeze sana Mkoa wa Iringa, tulikuwa huko juzi, imefanyika kazi kubwa na nadhani mikoa mingi inaendelea kuzindua na hivi karibuni tutakwenda kuzindua katika mikoa mingine chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tumeaswa kila unapopata nafasi ushukuru watu ambao wamefanya tofauti katika maisha yako. Sasa nataka nichukue nafasi hii kwanza kukishukuru sana Chama Cha Mapinduzi kwa fursa kilichonipa ya kugombea nafasi ya ubunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Ubungo kwa kunipa nafasi ya kuwa Mbunge wao, hatimaye tukakomboa Jimbo la Ubungo lililokaa Misri kwa miaka 10 sasa lipo Kaanan, tumetoka Misri sasa tupo Kaanan. Niwapongeze sana, tutashirikiana sana kuhakikisha kwamba, mambo ambayo tumeyaahidi tunayafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Waziri wa Mifugo, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ajiandae.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia sehemu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa tarehe 13 Novemba, 2020. Kabla ya hapo nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mungu kwa kuniwezesha kurudi tena kwenye nyumba hii ambayo kwa kweli, sio rahisi kurudi, lakini kwa nguvu za Mungu basi anatuwezesha kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kukishukuru Chama Cha Mapinduzi pamoja na wapiga kura wangu wa Jimbo la Maswa Magharibi kwa kunipa imani tena kurudi ndani ya nyumba hii, lakini nichukue nafasi hii kwa kipekee sana kumshukuru sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kuniadini kwamba, naweza kumsaidia kazi kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na niahidi tu kwamba, sitamwangusha, nitafanya kazi kwa bidii, maarifa, nguvu zangu zote na akili zangu zote ili kusudi tu kusudi ambalo analiona linatakiwa kutimizwa na Wizara hii basi liweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipewa malengo makubwa mawili kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. La kwanza, ni kuhakikisha kwamba, sekta hizi mbili zinachangia kwa sehemu kubwa kuondoa umaskini wa Watanzania wanaoshughulika na mifugo na uvuvi, lakini la pili kuhakikisha sekta hizi zinachangia kwa sehemu kubwa kwenye pato la Taifa na la mwisho kuhakikisha sekta hizi zinachangia kwenye ajira kwa Watanzania, kitu ambacho kimekuwa adimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipewa pia kwenye hotuba hiyo lengo dogo mahususi hasa kuhusiana na uvuvi wa bahari kuu kwamba, sasa uvuvi wa bahari kuu uchangie kwa mwaka bilioni 352 badala ya kuchangia kwa wastani

wa bilioni 3.3 kwa mwaka. Sasa hayo ndio malengo makubwa yaliyoko kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Sasa pamoja na kwamba, tungependa sana kufikia malengo hayo, lakini kuna changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge katika michango yao hapa wamekuwa wakiziainisha, lakini pia ziko changamoto nyingine ambazo hazijaweza kuainishwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini tumeziona katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi tulipoingia hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uvuvi lipo suala la uvuvi haramu. Uvuvi haramu unapunguza rasilimali ya uvuvi katika nchi yetu bila mpangilio wowote. Kwa hivyo, uvuvi haramu unapaswa kupigwa vita kwa namna yoyote ile na kila Mtanzania ili tuweze kulinda rasilimali hii na tuweze kuirithisha hata kwa wenzetu watakaokuja baadaye. Sasa ili kuondoa uvuvi haramu sisi tumekuja na mbinu shirikishi tukitaka kuwashirikisha wadau wote wanaohusika na uvuvi, ili kuhakikisha kwamba, tunakubaliana ni kwa namna gani kwa pamoja tuweze kuondoa uvuvi haramu ambao ni hatari kwa rasilimali hii ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la tozo mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge pia wamezitaja. Tumeliona na tumeliangalia, kwa sehemu kubwa limefanyiwa kazi suala la tozo, lakini tutaendelea kuliangalia suala la tozo zinazotozwa kwa leseni za biashara na tozo nyingine zinazotozwa zinakwaza wavuvi wetu. Tutaliangalia kwa upande wa juu, lakini niombe pia Wizara ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, waangalie pia na wao kwa upande wao tozo wanazotoza kwa upande wa uvuvi ili tuwaondolee mzigo mzito wavuvi wetu kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine katika uvuvi ni suala la uvuvi kwa bahari kuu. Tumejipanga vizuri na suala hili, Mheshimiwa Rais alishasema kwenye hotuba yake, kuna mpango wa meli zile nane; nne Bara na nne Zanzibar, lakini kwa Bara pia tumepata msaada mwingine wa meli moja kutoka Japan kwa hiyo zitakuwa tano. Kwa hiyo, tutakuwa na meli tano zitakazoanza kuvua kwenye uvuvi wa bahari

kuu, lakini pia shirika letu au Mamlaka yetu ya Uvuvi wa Bahari Kuu imeimarishwa sasahivi ina *staff*wanaofanya kazi. Mwaka jana Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu ilipitishwa, sasa hivi tunamalizia Habari ya kanuni zake tuitipitise ili tuweze kuanza kushughulika na uvuvi wa bahari kuu ambao kusudi lake ni kuleta bilioni 352 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, katika upande wa mifugo. Tumejipanga kwa habari ya miundombinu ili kuweza kuhakikisha kwamba, miundombinu ya uvuvi inakamilika katika maeneo ya wavuvi. Hii ni pamoja na malambo au mabwawa, minada, majosho na mambo mengine yanayotakiwa na wafugaji, ili kusudi tu waweze kuboresha mifugo yao ili iweze kuwa na afya bora na afya njema ili iweze kuleta tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la malisho; katika suala hili pia tumejipanga vizuri kama Wizara, tumepanga kwamba tuwe na hekta milioni moja na nusu kufikia mwisho wa mwaka huu, lakini ndani ya miaka mitano tunataka kufikia malisho ya hekta milioni sita. Kwa hiyo, tumepanga ili kufikia lengo hilo, kwanza kwa kushirikiana na zile...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umeisha.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Shukrani sana. Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa mimi, nanyi kuturudisha salama na kutuingiza

katika Bunge hili. Hakika Mungu ametufanyia mambo makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimshukuru Mheshimiwa Rais kunipa dhamana tena kwa mara nyingine ya kuendelea kuhudumu katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Pia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe na familia yangu kwa ujumla kwa mapenzi makubwa ya kunirudisha hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge. Mchango wangu ambao nimepewa katika Wizara hii ya wananchi nitaendelea kushirikiana nanyi kutekeleza yale mambo yote mahususi yanayohusu katika maeneo yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 20 Novemba, 2015, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alitoa *speech* yake hapa Bungeni. Katika *speech* aliyotoa ukienda katika eneo la pili, maana baada ya kusema rushwa aliizungumza Ofisi moja inaitwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Katika *speech* yake alisema hafurahishwi na haridhishwi na mwenendo wa ofisi hii katika suala zima la usimamizi wa miradi isiyotekelezwa ndani ya muda, ukusanyaji wa mapato na mambo mengine ambayo kwa kiwango kikubwa yalikuwa yanamnyong'onyesha Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na niwashukuru Wabunge wote katika kutekeleza *speech* ya Bunge ile ya kuzindua Bunge la Kumi na Moja kipindi kile nikiwa nimepewa dhamana kuhakikisha kwamba, TAMISEMI inahusika na ujenzi wa zahanati, hospitali za wilaya na halikadhalika vituo vya afya. Kutekeleza hotuba ile tulitoka katika vituo 115 vyenye uwezo wa kufanya huduma ya upasuaji mpaka tumefika vituo 487, ni rekodi ya kwanza tumeiweka. tumetoka hospitali za wilaya 77, leo hii tunakamilisha hospitali 102 mpya ndani ya miaka mitano, lakini tumejenga zahanati zetu 1,198. Katika upande wa afya tunasema eneo tulilopewa Mamlaka ya Serikali za Mitaa tumejitahidi kutimiza wajibu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya pili hii sasa ya ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili Mheshimiwa Rais alikazania tena katika suala zima la huduma ya afya, afya iweze kuimarika na hususan afya zetu za msingi. Katika eneo hili tumejipanga ndugu zangu. Kama tumeweka rekodi miaka mitano iliyopita Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli tumeazimia kwenda kuvunja rekodi ya kwetu sisi wenyewe na Waheshimiwa Wabunge naomba niwahakikishie tutapambana kila liwezekanalo kuhakikisha tunamaliza changamoto za wananchi wetu katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nimewaita Wakurugenzi wote wa Halmashauri ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania upande wa Tanzania Bara na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya. Katika mwaka wa fedha unaokuja na niwaombe sana Wabunge ninyi mkiwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani na Kamati za Fedha, tunaenda kuweka rekodi ya kwanza ya ujenzi wa vituo vya afya visivyopungua 185 ambavyo vituo hivi ni matumizi ya *own source* kabla hatujapata *top up* kutoka Serikali Kuu, hii inakuwa ni rekodi ya kwanza tunaenda kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwaambie Wabunge tumeshaazimia kikao cha leo na Wakurugenzi wote, kuna halmashauri zitajenga kituo cha afya kimoja, zenye bajeti ya kuanzia bilioni moja mpaka bilioni tano. Kuna halmashauri zitajenga vituo viwili kwa *own source* zenye bajeti kuanzia bilioni tano mpaka 12, lakini kuna halmashauri zitakazojenga zaidi ya vituo vitatu zenye bajeti kuanzia bilioni 12 na kuendelea. Tutapata zaidi ya vituo 185 ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, ambayo hizi ni fedha za mapato ya ndani kabla hatujaingia katika fedha za Serikali Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyozungumziwa ni kuhusu suala zima la *TARURA* hapa, tumelisia sana. Mnafahamu tumefanya kazi kubwa miaka mitano japo *resource* zilikuwa chache, lakini Serikali tunaendelea kulifanyia kazi hili na nishukuru sana Bodi ya

Mfuko wa Barabara, hivi sasa wanapitia ile *formula* kuangalia jinsi gani *formula* ikae vizuri kwa lengo la kuisaidia *TARURA* ifanye kazi vizuri. Ndugu zangu Wabunge, naomba tuwe na Subira timu inafanya kazi tutapata majawabu kabla mpango wa bajeti haujafika tutakuwa katika sura nzuri ya kuhakikisha jinsi gani *TARURA* inafanya kazi yake vizuri, lakini hiyo ikienda sambamba na kufanya *resource mobilization*, kutafuta vyanzo vingine vya kuisaidia *TARURA* ifanye kazi vizuri, hii ondoeni shaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa elimu ambayo tumepewa mamlaka ya kuhakikisha kwamba, elimu ya msingi tunaisimamia, tunaanza shule za awali mpaka kidato cha sita. Miaka mitano hii tulifanya kazi kubwa, ukiangalia shule kongwe kati ya shule 89 tumekamilisha shule 86 mpaka hivi sasa. Ninyi Wabunge ndio mashahidi, maeneo mlikotoka shule kongwe zilikuwa zimechakaa sana zimechoka, leo hii kazitazame tumetumia zaidi ya shilingi bilioni 89 katika shule kongwe peke yake, lakini tunaenda kufanya kazi kubwa ya ujenzi wa miundombinu katika mpango wetu wa ujenzi wa shule za kata 1,000 ambao tunatumia zaidi ya shilingi trilioni 1.2 ndani ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda kujenga zile shule 26 za wasichana, lakini tutahakikisha kata zote 718 ambazo hazina sekondari za kata, Wabunge naomba niambieni, tunajenga sekondari kata zote ndani ya Tanzania. Tunaenda kusimamia program ya elimu bila malipo ambayo kila mwezi sasa inatumika hivi sasa shilingi bilioni 24. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda katika mradi mwingine unaitwa *TACTIC* katika suala zima la kuboresha miji yetu. umefanya vizuri ndani ya miaka mitano. Halmashauri zenu zote zenye manispaa na halmashauri za miji leo hii mkienda mnashangaa, tumejenga barabara nzuri, kuweka taa za barabarani, kujenga na madampo sehemu nyingine, miaka mitano inayokuja ni miaka ya funga kazi ndugu zangu Wabunge. Tunaenda kushughulika na mradi wa *TACTICS* katika miji 45, tunataka Watanzania walioondoka Tanzania 2010 wakirudi 2025 wapotee miji yao wasiweze kuifahamu.

Hii ndio kazi kubwa tunayoenda kuifanya. Katika eneo hilo ndugu zangu Wabunge naomba niwahakikishie hatutanii na hii miaka mitano ni miaka ya mchakamchaka miaka ya kazi. Naomba niwaambie Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Serikali kwa ujumla itatoa ushirikiano wa kutosha mambo yaende sawasawa bila kikwazo cha aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na *issue* ya suala zima la mikopo ya akinamama, vijana na wenye ulemavu. Tunaenda vizuri, tumenza awamu ya kwanza kutengeneza sheria na juzijuzi nimeshasaini mabadiliko ya kanuni kuhakikisha akinamama na wenye ulemavu waweze kupata fursa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umeniishia, nilishukuru sana Bunge hili, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hata mimi nilikuwa nashawishika kupiga makofi hapa nikijua Mbeya Mjini itabadilika kabisa. *(Makofi)*

Tumalizie na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Awali na yote na mimi nianze kwa kumshukuru Mungu kwa afya na kwa hatua hii.

Nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa upendeleo huu tena wa kuendelea kumsaidia katika nafasi hii ya Waziri wa Katiba na Sheria. Pia niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Iramba kwa kunirejesha tena Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea kwenye hoja zilizojitokeza hapa leo, hoja ambayo iko mbele yetu ni Hotuba ya Rais na sisi kwa upande wa Mawaziri Hotuba ya Rais ni maelekezo na ni dira na sisi tumepokea twende tukaifanyie kazi. Kwa hiyo, kitu pekee ambacho nitazungumzia hapa, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge ambao

wamechangia katika mwelekeo huo wakitambua kwamba jambo hili ni la kisera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitafafanua tu mambo machache yale ambayo yaliguswa katika Wizara ya Katiba na Sheria. Kuna baadhi ya mambo ambayo yameongelewa, niongee huku nikiwa natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge sisi kama viongozi tuwe watu wa kwanza kuzingatia masuala yanayohusu sheria na katiba ya nchi yetu. Kuna hoja hapa zilizokuwa zinatolewa kwa muundo wa nchi yetu na mipaka ya kikatiba iliyowekwa kwenye taasisi zetu na hata kikanuni humu humu ndani ya Bunge hayapaswi kuongelewa. Sitataja moja baada ya lingine lakini kuna masuala ambayo yameongelea kesi ambazo ziko mahakamani ambazo ziko kwenye mhimili mwingine wa kutoa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya aina hiyo Waheshimiwa Wabunge yanapokuwa yako kwenye mhimili ambao unasimamia masuala tena uliopewa mamlaka haya ya kikatiba ni masuala ambayo hayapaswi kuongelewa kwa hisia tu na hayapaswi kuongelewa tunapokuwa hapa kama kanuni zetu zinavyoelezea.

Kwa hiyo, kwa hoja zile zilizojitokeza zilizokuwa zinalenga masuala ambayo yako kwenye mahakama zetu tuache utaratibu wa kikatiba, sheria na kanuni tunazozitumia uweze kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kuna mambo mengine baadhi ya wachangiaji walitaka kuyajenga kama vile yanafanyika kwa hisia kama wao walivyobeba hisia. Wanasema kuna watu wetu wamewekwa ndani, kuna watu wetu wamebandikwa kesi, kuna watu wetu wamekamatwa na wengine wanafika hatua ya kusema tu Waziri anayeshughulikia awaachie. Tunawatengenezea Watanzania hisia kana kwamba kuna watu wanaweza wakawekwa ndani bila makosa na kana kwamba kuna watu wanaweza wakatolewa bila kufuata taratibu zetu za kikatiba na za kisheria tulizoziweka. Huu siyo utaratibu uliosawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanasema ni kesi za uchaguzi, niwaambieni na sote tuwe na uelewa wa pamoja, kesi za uchaguzi ni zile zinazohusu rufaa zinazopinga matokeo ama zinazopinga mwenendo. Makosa yoyote ya jinai yanayotokea wakati wa uchaguzi hayafi kwa sababu ulikuwa ni wakati wa uchaguzi. Jinai si kesi ya uchaguzi ni kesi ya makosa ya jinai na taratibu zake za jinsi ya kufanyiwa kazi tumeweka kwenye Katiba na sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine yako kwenye mamlaka ambayo imepewa mamlaka yake ya kuchunguza kikatiba na kisheria, hatuyafuti kwa hisia. Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iko kikatiba na imepewa mamlaka ya kuangalia kesi ambazo hazifai kuendelea ikazifuta na kesi ambazo zinafaa kuendelea ziendele. Hatuzifuti kwa hisia wala hatuzifuti kwa maelekezo, ni mamlaka inayojitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuyaelewe haya na tuwaelezee wananchi wetu ili waelewe mipaka ya utawala wa kisheria. Utawala wa kisheria unaendeshwa kwa sheria siyo kwa hisia. Tukiendelea na utaratibu huu wa kusema kwa hisia tunaichafua nchi yetu ambapo wengine sisi hatuna mbadala wa nchi, nchi yetu ni hiihii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona mengine yanaibuka watu wanasema haki, haki, haki. Kati ya jambo ambalo nina uhakika nalo hata lisingeandikwa kwenye kakitabu kokote kale kwa Rais Magufuli limeandikwa moyoni ni jambo la haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanasema Tume, Tume. Hivi kwa kazi zote hizi zilizoordheshwa unaenda kushindana kwenye uchaguzi huu na Rais Magufuli utashindaje, unataka Tume ikusaidieje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote tushuhudieni tulipokuwa Majimboni walikuwa wanasema tushindane Udiwani na Ubunge kwa Rais tiki. Wewe unaenda

kwanza huna agenda, pili huna mgombea, mgombea wako ana tiketi ya kuja na ya kuondokea, unategemea Tume ya Uchaguzi ikusaidie, inakusaidia wapi? Lazima uanze kuanzia mwanzo uangalie ulikuwa una agenda gani kwenye uchaguzi huo na ulikuwa na mgombea gani, mgombea anayeangalia tiketi, anaangalia nitawahi vipi ndege hii halafu unategemea umpambanisha na mtu ambaye usiku na mchana anashughulika na maisha ya Watanzania, hili haliko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnaongelea uchumi wa kati eti tumeingizwa uchumi wa kati, ama tumedanganywa, sijui takwimu haziko sawa. Sikilizeni, uchumi wa kati hatuingii kwa kupigiwa kura, hii siyo *Bongo Star Search*, ni jambo la maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama miaka mitano zaidi ya vijiji 9,800 vimepata umeme na wananchi wake wameunganisha umeme ule. Kama ndani ya miaka mitano zaidi ya trilioni tatu zimekwenda kwenye elimu, zaidi ya trilioni mbili zimekwenda kwenye maji, zaidi ya trilioni moja imekwenda kwenye afya, zaidi ya trilioni moja imekwenda kwenye utawala bora, zaidi ya trilioni tisa zimekwenda kwenye miundombinu ya kuunganisha hawa watu wasafirishe mazao yao, wewe unashangaa kwamba eti tumeambiwa tumeingia, hujui hata kama umeshaingia! Wale ambao wanapata mashaka na jambo hili ombeni darasa muelezewe tu masuala ya uchumi wa kati yanaendaje ili tuache kuichafua nchi yetu wakati inapiga hatua. Hata wale wanaoweka vigezo hivi wanatuheshimu ndiyo maana hata kwa lugha yao kila wakipata tatizo wanasema *we need a person like* Magufuli ninyi mnakwama wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, mengine tutaongea kwenye mpango wa maendeleo wiki inayofuata. Ahsante sana, naunga mkono hoja 100%. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa mujibu wa taratibu zetu sasa nimuite Mheshimiwa Kassim

Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia afya njema tunapoelekea kuhitimisha hoja ya kujadili Hotuba ya Mheshimiwa, Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 13 Novemba, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii pia kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa namna ambavyo mmesimamia vyema mjadala huu uliotuchukua siku 4. Hali kadhalika napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumshukuru Mheshimiwa, Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa hotuba yake nzuri aliyoitoa wakati wa kuzindua Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku hiyo ya tarehe 13 Novemba, 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 169 wamechangia mjadala huu. Hivyo natumia nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia mjadala huu na kuunga mkono maeneo mbalimbali yaliyobainishwa katika hotuba ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwanza nakiri kupokea salamu za pongezi, salamu za shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nami nawahakikishia kwamba nitazifikisha baada ya kufunga hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge itasaidia sana Serikali kutekeleza kwa ufanisi maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 sambamba na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano kutoka mwaka 2021/2022 - 2025/2026 ambao

utawasilishwa kwenye mkutano huu na Waziri wa Fedha na Mipango kuanzia wiki ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa upande wake itaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge sambamba na kutekeleza ushauri na michango mizuri waliyoitoa wakati wa kuchangia hoja hii. Nitumie fursa hii pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa maelezo ya ziada na ufafanuzi mzuri kwenye sekta zote zilizochangiwa na kushauriwa kuelekea kwenye utekelezaji mzuri. Maeneo yote yaliyoshauriwa ni muhimu ambapo Serikali haina budi kuyazingatia katika utekelezaji wa mipango na vipaumbele vyake kwa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoona wakati wa mjadala huu, masuala na hoja nyingi zimetolewa maelezo na ufafanuzi wa kina kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri ambao wamemaliza muda mfupi uliopita. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali itazingatia maelekezo na ahadi za Mheshimiwa Rais katika kupanga vipaumbele vyake vya mpango wa bajeti katika kipindi chote hiki cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuibuliwa kwa hoja nyingi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa Hotuba ya Mheshimiwa Rais ni kielelezo tosha kwamba hotuba hiyo imegusa maeneo muhimu na yenye maslahi ya moja kwa moja kwa wananchi wetu. Miongoni mwa maeneo yaliyosisitizwa na Waheshimiwa Wabunge ni kuimarishwa kwa sekta za miundombinu na usafiri na usafirishaji ambapo taasisi zetu za *TARURA* na *TANROADS* nazo pia imeshauriwa namna ya kuziboresha. Sekta ya maji imeguswa, elimu na ujuzi nayo imesisitizwa, uongezaji thamani kwenye bidhaa zetu hususan za kilimo nayo pia imeguswa, uzalishaji mali, masoko, nishati, afya na huduma za kifedha na shughuli za kiuchumi uwekezaji ukiwemo na ujenzi wa viwanda nazo zimeguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote hayo yamefafanuliwa kinagaubaga kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo hoja yake tunaihitimisha leo.

Kadhalika wakati nawasilisha hoja hii, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa tayari utekelezaji wa maelekezo na ahadi za Mheshimiwa Rais ulishaanza mara tu alipowasilisha hotuba yake siku ya tarehe 13 Novemba, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwenye wiki ijayo tutapata nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha na Mipango ambayo nitasheheneza mjadala ninaohitimisha leo. Kama ambavyo unafahamu maandalizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 yanaendelea. Hivyo basi, kutokana na ukweli kuwa maeneo hayo ya vipaumbele yanahitaji kupangiwa fedha za bajeti kwa ajili ya utekelezaji wake, kupitia mijadala na hoja zote mbili, hotuba yangu ya kuhitimisha Mkutano huu wa Bunge nitatoa mwelekeo wa namna ambavyo tutakwenda kutekeleza yale yote ambayo jameshauriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maelekezo kwa Wizara na taasisi nyingine za Serikali kuhakikisha kwamba vipaumbele hivyo vinapangiwa fedha kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022. Kwa msingi huo, nitumie fursa hii kurudia tena kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba maoni na hoja zenu zitazingatiwa wakati wote kwa utekelezaji wa vipaumbele vya Serikali. Vilevile kwa ile miradi inayoendelea kutekelezwa nchini katika sekta za uzalishaji mali ikiwemo kilimo mifugo, maliasili, madini na sekta za huduma ya jamii kama vile elimu na afya zitakamilishwa kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa ikifanya juhudi kubwa katika kuandaa mpango pamoja na mipango ya bajeti na kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele mbalimbali vya Serikali vyenye lengo la kuwaletea maendeleo wananchi. Hata hivyo, awali tulikuwa na changamoto ya baadhi ya viongozi na watendaji kutowajibika na kusababisha kudorora katika kuwahudumia wananchi ipasavyo. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ya Awamu ya Tano ilijikita katika kuhakikisha inarejesha nidhamu katika utumishi wa umma kwa kuweka mkazo katika

misingi ya uadilifu, uwajibikaji, kutoa huduma kwa wakati na kuchukua hatua za haraka dhidi ya watumishi wote wanaokwenda kinyume na misingi ya utendaji wa kazi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyote mtakubaliana nami kwamba kuimarishwa kwa nidhamu ya viongozi na watendaji Serikalini imekuwa chachu ya kufikiwa kwa malengo mengi tuliyojiwekea. Aidha, baada ya kufuatilia kwa karibu michango ya Waheshimiwa Wabunge, nami napenda kusisitiza masuala machache kwa viongozi na watendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni suala la utoaji wa taarifa kwa umma kwa wakati kuhusu miradi na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali. Katika hili, nirejee kauli ya Mheshimiwa Rais mpendwa aliyotoa tarehe 4 Juni, 2018 wakati akizindua Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini (*ASDP II*) kwamba viongozi na watendaji wa Serikali wanao wajibu wa kueleza kwa kina mambo yanayotekelezwa na Serikali kila wanapopata nafasi ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashuhuda kwamba yako mambo mengi ya kujivunia yametekelezwa na yanaendelea kutekelezwa na Serikali yetu. Kwa msingi huo, Watanzania wanayo haki ya kuhabarishwa na kufahamu mipango na mikakati mbalimbali ya Serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu. Nitoe wito kwa viongozi na watendaji kwenye ngazi mbalimbali kuzingatia eneo hilo la mawasiliano kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulisisitiza ni viongozi na watendaji kuwafikia wananchi kwenye maeneo yao kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Katika ziara zangu zote nimekuwa nikisisitiza kuwa viongozi na watendaji wawafuate wananchi kwenye maeneo yao, wawasikilize na kuwahudumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe tu viongozi na watendaji wote kwamba tunao wajibu mkubwa kwa wananchi kutokana na dhamana waliotupatia, hivyo, tunapaswa kuwajibika kwao badala ya kusubiri ziara za viongozi wakuu wa kitaifa. Natumia fursa hii kuwaambia viongozi na watendaji wote wa Serikali kuwa tutapima utendaji wenu kwa namna mnavyotatua kero za wananchi kwenye maeneo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa upande wetu itahakikisha inachukua hatua dhidi ya wote watakaokika sheria, kanuni na taratibu za kazi na kwamwe hatutamvumilia mtumishi mzembe na mwenye kufanya kazi kwa mazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, hotuba yangu ya kuhitimisha mkutano huu itajumuisha mijadala yote miwili; huu ambao tunahitimisha leo na ule wa Mpango wa Wizara ya Fedha ambao utaanza kujadiliwa kuanzia Jumatatu. Nimalizie maelezo yangu kwa kuwasihii Waheshimiwa Wabunge kwamba tunao wajibu wa kuishauri Serikali sambamba na kuwaongoza wananchi katika kusimamia utekelezaji wa ahadi na maelekezo ya Mheshimiwa Rais yaliyomo katika hotuba yake ya kuzindua Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuimarisha ushirikiano wa wananchi na mamlaka mbalimbali za Serikali hususan Serikali za Mitaa kwa lengo la kuhakikisha kwamba wanaunga mkono Serikali na hivyo kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele mbalimbali kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme ni kwamba nimevutiwa sana na michango ya Waheshimiwa Wabunge wakati wote wa kuchangia hoja hii. Nimepokea ushauri wenu kama ambavyo nilieleza wakati tunawasilisha hoja hii na sasa narudia kwamba tutaendelea kushirikiana katika kuboresha yale yote ambayo mmechangia kwenye hoja hii ya kujadili hotuba ya

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo aliitoa tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akifungua Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa hoja.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa mujibu wa taratibu zetu nitawahoji Wabunge kuhusu hoja ya Waziri Mkuu ambayo aliileta tukiwa tukijadili hotuba ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili tarehe 13 Novemba 2020.

Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda.
(Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati huu kwa Wabunge wageni ndio watakuwa wamepata picha maana ya Wabunge walio wengi Bungeni na Wabunge walio wachache.

Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye hoja yake ililetwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge mmefanya kwa sehemu yenu yale ambayo mmeishauri Serikali kama mlivyomsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu wameyachukua.

Michango hii itaendelea kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu kimsingi ni kwamba hoja hii ilikuwa inatoa mwelekeo wa Mpango wa Miaka Mitano wa Serikali hii ambayo ndiyo iko madarakani sasa. Kwa hiyo, tutaendelea kujadili mambo mengi ambayo yameshadiliwa, yatajadiliwa wiki ijayo lakini yataendelea kujadiliwa kwa miaka mitano kwa sababu hotuba hii ndiyo inayotoa dira ya nini kitafanyika katika miaka mitano.

Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote na tunawatakia kila heri katika utekelezaji wa haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema wakiangalia muktadha wa hotuba ya Rais. Waheshimiwa Wabunge kwa maana hiyo hoja hii imepita ama imeshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka asubuhi niliombwa Mwongozo na nilisema nitautoa baadaye, mwongozo huo uliombwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka kuhusu swali lake kutojibiwa kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, leo tarehe 5 Februari, 2021 katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili niliombwa Mwongozo na Mheshimiwa Kaboyoka chini ya Kanuni ya 53(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2020. Wakati akiomba Mwongozo huo Mheshimiwa Kaboyoka alieleza kuwa swali lake la msingi namba 48 alilouliza kwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwamba ni lini wakulima wa tangaziwi Ushirika wa Mamba Miamba, Wilaya ya Same watalipwa hela zao? Alieleza kwamba swali lake lilitokana na Kamati iliyoungwa na Mheshimiwa Waziri Jafo ambayo ilisimamiwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenda kuchunguza matatizo ya wakulima kuhusu kudhulumiwa fedha zao na ripoti ile ilionesha wazi kwamba wakulima hao waliibiwa fedha zao kiudanganyifu.

Hivyo alihoji ni kwa nini Waziri wa Viwanda na Biashara alitoa majibu yanayokinzana na ripoti ya TAMISEMI. Waheshimiwa Wabunge baada ya maelezo hayo Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka aliomba Kiti kiwaagize Mawaziri wa TAMISEMI na Waziri wa Viwanda na Biashara wakae na wapitie ripoti iliyoandaliwa na TAMISEMI ili kuona kama swali namba 48 lilijibiwa kikamilifu na kama halikujibiwa kikamilifu swali hilo lijibiwe upya.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata fursa ya kupitia kumbukumbu ama Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* na kuona kuwa swali la msingi liliulizwa kama ifuatavyo: je, ni lini Serikali itawalipa wakulima wa tangawizi wa Mamba

Miamba, Wilaya ya Same Mashariki ambao walifungiwa na *SIDO* mashine zisizo na kiwango cha kuchakata tangawizi?

Maswali ya nyongeza yalikuwa kama ifuatavyo: Swali la kwanza lilikuwa Serikali imepotosha Bunge lako tukufu kwa kusema uwongo ambao haukubaliki je, Waziri anajua kwamba TAMISEMI chini ya Waziri Mheshimiwa Jafo waliounda Kamati ya Uchunguzi mwaka 2018 na Kamati hii ilitoa mapendekezo kuonesha jinsi *SIDO* ilivyowaibia wakulima pamoja na Halmashauri ya Same ambayo haikufanya kazi yake vizuri kuwashauri wakulima na michango ambayo ilitolewa na Rais wakati ule Mheshimiwa Kikwete karibu milioni 300 haikutumika vizuri na ukaomba hatua madhubuti ichukuliwe na *SIDO* ilipe fedha za wakulima.

Swali la pili, la nyongeza lilikuwa je, Mheshimiwa Waziri ana habari kuwa kutokana na mitambo ile haikufanya kazi ndio maana pia *PSSSF* imenunua mitambo mipya na inaifunga na hawakuona kwamba mitambo ile iliyofungwa ilikuwa batili? Katika Mwongozo alioomba, Mheshimiwa Kaboyoka aliomba kiti kiwaaagize Mawaziri wa TAMISEMI, na Viwanda wakae na wapitie ripoti aliyozungumzia ili waone iwapo swali lake lilijibiwa kikamilifu na kama halikujibiwa basi lijibiwe upya.

Waheshimiwa Wabunge, majibu ya Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara katika swali la msingi na maswali ya nyongeza alionesha wazi kuwa bado zipo changamoto kuhusu masuala yaliyogusiwa na Mheshimiwa Kaboyoka. Katika majibu ya swali la msingi Naibu Waziri alisema sehemu ya hayo majibu nanukuu: "Serikali imeielekeza *SIDO* ishauriane na Halmashauri ya Same pamoja na Ushirika wa Mamba Miamba ili kutathimini na kukubaliana namna ya bora ya kutatua changamoto hiyo."

Majibu yake kwa maswali ya nyongeza yalikuwa kama ifuatavyo; nanukuu: "Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kuhusiana na hasara au gharama ambazo zilikuwa zimeingwiwa na wakulima wale baada ya mtambo ule kutokufanya kazi vizuri kama nilivyosema tunaelekeza *SIDO*

sasa waweze kufanya maushauriano na halmashauri ili waone namna gani ya kuwafidia wakulima wale ambao walipoteza mazao yao kipindi kile ambapo mtambo ulikuwa haufanyi kazi.”

Waheshimiwa Wabunge kwa majibu hayo, Serikali inakiri kuwa bado kuna changamoto ya malipo ya fidia kwa wakulima waliopoteza mazao yao kipindi ambacho mtambo ulikuwa haufanyi kazi kama ilivyokusudiwa na kwamba changamoto hiyo kwa maelekezo yaliyotolewa hapa Bungeni *SIDO* pamoja na Halmashauri ya Same, mnatakiwa kuyafanya kazi hayo maelekezo.

Waheshimiwa Wabunge kutokana na majibu ya Serikali ya swali la msingi, na maswali ya nyongeza nimejiridhisha kwamba Serikali imejibu maswali hayo kwa ukamilifu. Kwa maelezo hayo ya Serikali ni kwamba changamoto ya malipo inapaswa kufanyiwa kazi na *SIDO* na Halmashauri ya Same. (*Makofi*)

Kwa hivyo, ni vyema Mheshimiwa Mbunge asubiri hatima ya majadiliano hayo na ikiwa majadiliano hayo yatachukua muda mrefu basi Mheshimiwa Mbunge ataweza kufuatilia kwa njia za kawaida zilizopo huo ndio mwongozo wangu kuhusu jambo alilokuwa ameliomba Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo hapa linalotoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba kesho kutakuwa na mafunzo ya Wabunge wote yatakayofanyika kuanzia saa nne asubuhi na pia siku ya Jumapili yaani tarehe 7 Februari, 2021, mafunzo hayo yataanza saa nne na nusu asubuhi katika ukumbi wa Msekwa hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge wote mnasisitizwa kuhudhuria mafunzo hayo bila kukosa kesho saa nne na kesho kutwa saa nne na nusu. Mheshimiwa Spika ameagiza Wabunge wote wahudhurie mafunzo hayo. Kwa hiyo, naamini Waheshimiwa Wabunge mtaona hii ni sehemu ya

mafunzo yaliyokuwa yamesemwa kwenye taarifa ya Mheshimiwa Spika kabla Bunge hili halijaanza siku ya Jumatatu.

Kwa hiyo, ni muhimu kuhudhuria kwa sababu vipo vitu vingi ambavyo tunapaswa kuvifahamu. Kwa sababu hapa ndani huwa nikiangalia hivi naona Waheshimiwa Wabunge wengi hawajasoma ile kanuni ya mavazi, mtu anakuja amevaa suti ambayo inapaswa kuwa na shati na tai na yeye amekuja hajavaa tai. Sasa akisimama mtu hapa ukatolewa nje itakuwa mtihani Mheshimiwa Mbunge na ukivaa, ndio hivyo kanuni zetu zipo wazi hapa. Kwa wanaume nadhani hizi kanuni ziko wazi zaidi kuliko wanawake, kwa hiyo, ni muhimu sana kuzifuatilia na matakwa yake.

Pia huwa naona watu wanakatiza katikati ya mtu anayezungumza na Kiti hapa na wako wengine sio kwamba tu ni Wabunge wapya jamani, hili Bunge kama nilivyosema ni jipya, wako hata wa zamani anakatiza tu wala haangalii mtu anayeongea yuko wapi, lakini katika kipindi hiki cha mwanzo huwa kuna uvumilivu kidogo, huko tunakokwenda utaambiwa rudi ulikotoka ili mtu amalize mchango wake halafu ndio uje sehemu yako ya kukaa.

Jambo lingine akisimama mtu hapa yaani Kiti kikiwa kimesimama watu wote mnapaswa kuwa mmekaa, huruhusiwi kunyanyuka hata kama unaenda chooni, inabidi usubiri Kiti kikae, kikiwa kimesimama watu wote mnapaswa kukaa ili Kiti kizungumze kikiwa kimesimama hapa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 8 Februari, 2021, saa tatu asubuhi.

(Saa 1.30 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 8 Februari, 2021 Saa Tatu Asubuhi)